Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA NANE

### Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 11 Februari, 2010

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hati zifuatazo:-

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi na Thamani ya Fedha juu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari kuhusu tatizo sugu la Matokeo duni ya Wanafunzi wa Sekondari katika Masomo ya Hisabati na Sayansi chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi *(A Performance audit Report on School Inspection Programme for Secondary Schools in Tanzania);*

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi na Thamani ya Fedha kuhusu Usimamizi katika kushughulikia tatizo sugu la taka ngumu katika Miji mikubwa na Manispaa – chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikijumuisha, Jiji la Dar es Salaam, Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni, vilevile Majiji ya Mwanza, Mbeya na Arusha *(A Performance Audit on the Management of Solid Waste in Big Cities and Region(s) in Tanzania. Mbeya, Dar es Salaam, Mwanza and Arusha);*

Ripoti ya Ukaguzi Ufanisi na Thamani ya Fedha kuhusu Uandaaji wa Mafao kwa Wastaafu wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa Nchini Tanzania chini ya Wizara ya Fedha na uchumi *(A performance Audit on Processing of Terminal Benefits of Retirees from the Central and Local Government of Tanzania, A Case Study Public Service Pension Funds (PSPF) and Local Authorities Pension Fund (LAPF));* na

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Thamani ya Fedha kuhusu Usimamizi katika kutoa Huduma za Afya na Muda wa Wagonjwa Kusubiri pamoja na Raslimali Fedha na Watu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii *(A performance Audit Report on the Management of Primary Health Care, a Case Study of Health Centres).*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu cha Dodoma kwa mwaka 2007/2008 *(The Annual Report and Audited Accounts of The University of Dodoma for the Financial Year 2007/2008).*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwsilisha Taarifa ya Mapendekezo kuhusu Agizo la Kima cha chini cha Mishahara Pamoja na hali nyingine za Ajira chini ya Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya Mwaka 2004.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati Kamati ya Nishati na Madini ikiwasilisha hoja, moja katika hoja namba 18 ilielekeza kwamba Serikali ichukue hatua za kisheria za kuwashitaki watu wa *Richmond,* na Serikali katika maelezo yake ikasema kwamba uchunguzi wa ndani umemalizika lakini uchunguzi wa nje haujakamilika.

Katika suala la Rada, Serikali ilikuwa ikishirikiana na *Serious Fraud Organisation* ya Uingereza ili iweze kupata matokeo, bahati nzuri wenzetu wa nje wamekamilisha kazi hiyo na wakasema Tanzania imepata *change* katika malipo yale yaliyofanywa; je, uchunguzi wa ndani wa Tanzania utakamilika lini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina jibu kwa swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed lakini kama hoja ni kupata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa TAKUKURU tutafanya hivyo lakini kwa sasa kwa kweli siwezi kusema uongo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** *No answer either supplementary question!*.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, kwa hii *change* ambayo tuliahidiwa kama ipo Serikali iko tayari kutumia Kamati ya Miundombinu ya Bunge ili kuhakikisha kwamba fedha yetu inakuja huku ndani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata hili siwezi kulijibu, siwezi kulijibu kwa sababu sina taarifa juu ya jambo hili ndiyo maana nashindwa kumsaidia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu sahihi, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, karibu!

**MHE. DR. WILLlBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni Serikali kupitia Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, ilitangaza kufuta ada zote za mitihani kwa wanafunzi wa shule za Sekondari, wa kidato cha pili, cha nne na cha sita. Lakini

hivi karibuni vilevile kumetolewa taarifa na imenukuliwa na magazeti ya tarehe 2 Februari, 2010 akinukuliwa Afisa Habari wa Wizara kwamba, ada ziko palepale.

Vilevile hivi karibuni tumepata taarifa kutoka Wilaya mbalimbali kwamba wanafunzi bado wanatakiwa kulipa hizo ada au wazazi au walezi wao. Nini kauli ya Serikali kuhusu utata huu na, je, Serikali inasemaje kuhusu hali hii ya utata ndani ya Wizara?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama kuna utata hasa ndani ya Wizara, sidhani! Alichosema Mheshimiwa Waziri wa Elimu wakati akizungumzia jambo hili kama nilimsikiliza vizuri ilikuwa ni kwamba, utaratibu huu unaanza katika Bajeti ya mwaka unaokuja yaani 2010/2011. *(Makofi)*

Kwa sasa kwa sababu tayari baadhi ya wanafunzi walikwishalipa ada hizo tayari kwa hiyo, kutoa uamuzi kwamba ada zimefutwa bila kujali kwamba wanafunzi wengine wote wengi wameshalipa nayo haiwezi kuwatendea haki, lakini linaweza likatazamwa kwa maana ya *case by case* kuona kama tufanyaje kwa wale ambao *genuinely* wazazi wao hawana uwezo wa kulipa hiyo ada. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu yake ambayo kwa kawaida ni manyoofu. *(Makofi)*

Je, ni lini sasa Serikali itatoa waraka kwa sababu katika uchunguzi wangu mpaka jana hakuna Halmashauri iliyopokea waraka wowote unaotoa maelekezo hayo ili utekelezaji uende sawa kwa sehemu zote na wananchi wajiandae kufuatana na maelekezo ambayo Serikali itakuwa imeyatoa kwa barua?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Slaa ana haraka sana, kwa sababu jambo hili alieleza waziwazi kwamba, sasa utaratibu mzima wa malipo kwa ajili ya ada za mitihani utaingizwa katika fedha ambazo zitakuwa zinalipwa na Serikali katika Bajeti inayokuja.

Kwa hiyo, moja ni kusubiri Bajeti ipitishwe na mimi naamini wakati huo maandalizi yote ya waraka utakuwa unatoa maelekezo na utakuwa umeshakamilika, kwa hiyo, *immediately* baada ya pale taratibu sasa zitafuata.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa waziri Mkuu, Serikali ilifanya uhakiki wa madeni ya walimu, na imejitahidi sana kulipa baadhi ya maeneo lakini sehemu kubwa sana bado walimu wanadai, mfano Misungwi wanadai zaidi ya shilingi milioni 350, Kwimba shilingi milioni 270 na hata Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wake ni zaidi ya shilingi bilioni 1.1.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni nini tatizo la kutolipwa walimu hawa wakati uhakiki ulishafanyika na majina yamewekwa kwenye mbao za matangazo za Halmashauri? Naomba tupate jibu kuhusu hatma ya walimu hawa wanaoidai Serikali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Jacob Shibiliti kwa swali hili zuri, lakini nataka niseme kwamba, walimu ni sehemu tu ya utumishi wa umma, mimi nafikiri tuzungumze makundi yote tuliyonayo na aina ya madeni ambayo yalikuwa yamewasilishwa Serikalini.

Tuna makundi ya aina mbili kubwa yaani walimu na wale wasio walimu na ndani ya walimu wako walimu wa shule za msingi na wale wa sekondari. Katika makundi ya madai yapo madai ya mishahara na yapo madai ambayo yanatokana na malimbikizo ya shughuli nyingine kama matibabu, safari, likizo na kadhalika.

Sasa kwa upande wa walimu, upande wa shule za sekondari na shule za msingi. Shule za msingi tulikuwa tumeshafikia kiwango cha kama shilingi billioni 32 ambazo tulikuwa tunadaiwa. Katika hizi shilingi bilioni 22 zimekwishalipwa tayari na shilingi bilioni kama 10 ndiyo hizo ambazo kulitokea mkanganyiko kidogo wa maelekezo ndani ya Serikali ingawa walihakikiwa lakini ilionekana baadaye maelekezo kidogo ambayo yamewachanganya.

Utakumbuka mara ya mwisho ndiyo jambo moja ambalo niligusia kwamba kwa kweli kwa wale waliohakikiwa ni vizuri wakalipwa pamoja hata kama si walimu ili mradi wako katika utumishi wa umma lakini wamehakikiwa, kwa hiyo jambo lile linashughulikiwa na ninafikiri litakwenda vizuri. *(Makofi)*

Upande wa walimu wa sekondari, nako juhudi zinaendelea kwa maana ya kuwalipa madeni yote ambayo tunafikiri wanastahili, mimi nadhani kundi hili la walimu kwa sehemu kubwa kabisa limeshafanyiwa kazi nadhani tatizo litakuwa pengine ni uwasilishaji wa fedha kwenye Halmashauri na mchakato wa namna ya kuzitoa kuingiza katika maeneo yanayohusika kwa walimu. Lakini kimsingi hatudhani kwamba tatizo ni kubwa sana kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo bado halijawa zuri sana ni la watumishi wengine ambao siyo walimu. Hapa tunadaiwa shilingi bilioni 22, tumekwishalipa kama shilingi bilioni 10 moja kwa moja kwenda kwenye mishahara yao, kiasi hiki kilichobaki hakikuingizwa kwenye mishahara moja kwa moja kwa sababu ni yale malipo yanayotokana na likizo moja moja au usafiri kwa namna moja au nyingine, hizi ndiyo sasa ambazo tunahangaika nazo kuwasilisha kwenye maeneo yanayohusika ili walimu waweze kulipwa moja kwa moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa ujumla naweza kusema kwamba tatizo tunalijua na tatizo lile tunalishughulikia lakini nadhani hatuko mbali katika kuhakikisha kwamba kila mmoja tumemaliza shida ambayo inamkabili kwa maana ya kero. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni kumetokea kauli mbili zinazotofautiana au zinazokinzani kutoka kwa Mawaziri wa Awamu ya Nne kuhusiana na ajira ya Profesa Baregu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wakati Waziri wa Utumishi akisema kwamba ajira yake imesitishwa kwa sababu ya kujihusisha na siasa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tarehe 5 Februari, 2010 akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kunukuu,

alisema kwamba; “Profesa Baregu hakuondolewa kwa sababu eti tu ni kiongozi wa CHADEMA maana wako viongozi wa vyama vingine ambao pia tunao kwenye kazi na ambao hawajastaafu.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kauli hizi zinatofautiana sana kwa sababu mmoja anasema ni sababu za siasa na mwingine anasema kwamba bado kuna watumishi ambao ni wanasiasa Serikalini. Je, huku siyo kujikanganya kwa Mawaziri wako na kuwachanganya pia wananchi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika dada yangu Mheshimiwa Susan Lyimo kama uliusoma ule Waraka wa Utumishi, uliusoma wote kikamilifu? Kwa sababu inawezekana tatizo linaanzia hapo, kama hukupata nafasi ya kuusoma na kuona maudhui ya waraka ule, unaweza ukadhani Mawaziri hawa wawili wamejikanganya. Katika waraka ule yapo mambo mawili yanaelezwa, moja ni mamlaka ya mwajiri ya kumuondoa mtu ambaye yuko kazini kwa utaratibu wa mkataba, hayo mamlaka ni ya kwake kila unapomaliza si lazima urudie tena hata kidogo. *(Makofi)*

Cha pili ambacho kimeelezwa kwenye Waraka ule na ule Waraka kwa sababu umesambazwa kwa umma ndiyo maana ilibidi masuala yote katika ufafanuzi yatolewe, kwamba uko vilevile Waraka na hili linagusa zaidi utumishi wa umma ambao bado tupo katika Serikali au hata wale ambao pengine wameacha lakini bado wangeweza kuendelea zaidi, kwa maana kwamba ukiwa ni mtumishi wa umma wewe hutakiwi kujihusisha na masuala ya kisiasa. Sasa eneo hili la pili kwa kweli linamgusa mtumishi mwingine yeyote yule katika utumishi. *(Makofi)*

Sasa Profesa Baregu yeye kwa upande mmoja yuko kwenye mkataba, tena ni mkataba ambao alikuwa nao akaongezwa tena, ndiyo maana Serikali ikasema kwamba baada ya kupata fursa ya kurudia mara mbili hivi tunadhani inatosha, lakini hata kama asingekuwa ni mtumishi wa mkataba kwa maana hiyo ukawa ndani ya mfumo wa Serikali kama walivyo watumishi wengine, tungeweza na yeye tukamchukulia hatua hiyo hiyo kwa sababu ya kushiriki katika masuala ya kisiasa kama tungekuwa na ushahidi wa namna hiyo. Ndiyo maana nasema pengine hakuna mkanganyiko mkubwa sana inaelekea tu unataka kusisitiza jambo gani katika mtazamo. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kwamba umejibu swali langu na kusema kwamba watumishi umma aidha, yuko kwenye mkataba au hayupo, bado hastahili kuwa katika siasa. Lakini Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, alisema kwamba Profesa Baregu kuondolewa kwake siyo kwa sababu za kisiasa isipokuwa hata sasa hivi wana viongozi wa vyama ambao ni watumishi wa umma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, bado suala langu liko palepale kwamba lipi ni sahihi kwamba, viongozi wa vyama vya siasa wanaruhusiwa kuwa kwenye utumishi Serikalini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hilo ni swali lingine wewe ungelileta tu kama *separate* lakini ukiyachanganya mimi nitakuambia hapana! *(Makofi)*

Kwanza tukubaliane kwamba maamuzi yaliyofanywa na mwajiri ni sahihi! Halafu tuje kwenye swali lako la pili, kama wapo lete majina na useme na huyu yupo na kadhalika ili hatua ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, mtu hawezi kuwa sehemu ya mjadala ndani ya Bunge! Haya Mheshimiwa Godfrey Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa muda mrefu sasa nchi yetu ni kama imevamiwa na madhehebu mbalimbali ya dini. Madhehebu haya mengine yamekuwa yanawatoza wananchi ushuru kama sharti la kuingia Kanisani kusali, kama tulivyoona kule Bagamoyo hivi karibuni. Lakini pia kule Mbeya kuna madhehebu ya dini ambayo yanawazuia watoto kuimba Wimbo wa Taifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inalifahamu jambo hili? Na kama inalifahamu inachukua hatua gani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujaribu kumjibu Mheshimiwa Zambi swali lake kuhusu masuala haya ya madhehebu ya dini.

Kwanza nikiri kwamba yapo madhehebu ya dini mengi na nafikiri Mkoa wa Mbeya wanaongoza. Lakini lipo jambo la msingi ambalo amelisema hapa sina tatizo sana na hiyo tozo kuingia kwenye Makanisa au Masinagogi, kama ndiyo muumini ameona imani yake inamtuma hivyo aah! shauri yake!

Lakini hili la wimbo wa Taifa kwa wanafunzi, pengine jambo ambalo lingekuwa zuri ikasemwa sina hakika ni shule gani, ni seminari ya madhehebu hayo ya dini au ni shule *public* kwa maana shule za misingi au sekondari ambazo zinaendeshwa kwa mfumo na kutambuliwa na Serikali? Kwa sababu kama ni shule ambazo zimeandikishwa kwa mujibu wa taratibu za Serikali, inatambulika na wanafunzi wanaokwenda pale si kwa mfumo wa ubaguzi na hata kama ingekuwa kwa msingi wa kibaguzi kwamba ni dini moja tu, bado zile taratibu zinazotawala shule zote zinapaswa kuheshimika. *(Makofi)*

Sasa mimi nadhani kwa hili tukuombe tu kwamba kama una *case* mbili au tatu za aina hiyo basi nikuombe tu uziwasilishe kwa Waziri wa Elimu, tuone na tufanye uchunguzi kidogo halafu hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nashukuru kwa majibu mazuri, lakini nilitaka pamoja na kunielekeza nimuone Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kwa maana ya kumpa taarifa zaidi, sasa baada ya Waziri wa Elimu kupata taarifa kutoka kwangu na ikithibitika kwamba kuna wageni kutoka nje wanaoanzisha madhehebu haya wanahusika katika kuwafanya watoto wetu wasiimbe Wimbo wa Taifa, kwenye shule za msingi na hili pia nitampa

Mheshimiwa Waziri wa Elimu, je, Serikali itakuwa tayari kuwafukuza wageni wa aina hiyo nchini kwetu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri tukubaliane tu kwamba tupate maelezo juu ya hawa walimu, tumwelekeze Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alifanyie kazi ili kama itabainika kwamba amevunja taratibu za kiuhamiaji hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao wote na ninafikiri tukifanya hivi tutakuwa tumetenda haki vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, miezi mitatu nyuma yaani Novemba, 2009 baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI tulipata bahati ya kwenda kutembelea Rwanda, kujifunza na kubadilishana mawazo na kuona ufanisi mkubwa walioupata katika vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Lakini mbali ya masuala ya UKIMWI, tulijifunza mengi mazuri waliyoyapata kule, nchi ambayo imepita katika tanuri la mauaji ya Kimbari miaka 15 tu iliyopita. Moja katika mambo hayo ni usafi, tangu Kigali mpaka Wilayani mpaka Vijijini na mpaka mabondeni kwa wakulima, ni kusafi kabisa, hukuti karatasi, mifuko ya plastiki wala uchafu wowote unazagaa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi leo tuko miaka 48 ya Uhuru, tuna Sheria nzuri tu kuhusu mazingira lakini miji yetu ni ya mwisho kwa uchafu katika Bara la Afrika. Lini tutafika huko?

**NAIBU SPIKA:** Ikiwa ni ya mwisho kwa uchafu basi ni safi! *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, kama anasemaje hapo, kwa sababu unaposema Tanzania, *well* umegeuza tu namba nadhani ulitaka kusema ni ya kwanza kwa uchafu, sina hakika hizo takwimu umezitoa kwenye *source* ipi maana hiyo ni muhimu sana, hizo takwimu zimetokana na chanzo gani?

Lakini kwa upande wa pili pengine ni changamoto kwa Watanzania wote kwa ujumla, kwamba kama mmeweza kufika mpaka vijijini huko mkakuta ni kusafi sana sasa leo unasema kwamba unashangaa kuona usafi mpaka vijijini na mimi nasema aah! Sasa hili ni la Waziri Mkuu au letu wote! *(Makofi)*

Lakini mimi najua viko vijiji vingi ambavyo ni visafi sana, *planning* ni nzuri sana mfano mzuri nenda maeneo ya Kigoma ukatembelee baadhi ya maeneo utapenda, nenda Mbeya, Songea - Ruvuma *well planned and very clean*. Lakini kwa sehemu za mijini yako mambo mawili makubwa; moja ni utamaduni wetu sisi wenyewe wananchi. Kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kutambua wajibu wake wa kuweka mazingira yake katika hali ya usafi, kwa sababu wakati mwingine inakera unapokwenda kwenye nyumba ya mtu haoni tatizo kabisa kwamba nyumba yake imezingiwa na uchafu palepale alipo na wala usishangae unaona mtu anafagia anasogeza uchafu kwenye mlango wa jirani yake ni vitu ambavyo vinataka tu mmoja mmoja ajue na kutambua wajibu wake wa kutunza mazingira. *(Makofi)*

Lakini upande wa pili tunakubali kwamba uzalishaji wa taka ngumu katika miji yetu ni mkubwa mnao ukilinganisha na huduma zinazotolewa kwa ajili ya kudhibiti uchafuzi huo. Sasa ndiyo maana unaona hata leo katika taarifa iliyowasilishwa hapa moja ya jambo ambalo utaliona katika taarifa ile ni hali halisi na hatua zinazochukuliwa.

Kwa hiyo, mimi nataka niziombe tu Halmashauri zote nchini na Watanzania wote, tukishirikiana kwa pamoja katika kudhibiti uchafu katika maeneo haya uwezo upo ni kiasi tu cha kujipanga vizuri na kuongeza uwekezaji katika maeneo haya. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, wenzetu wana siku maalum wamejiwekea sheria, wana siku maalum kwa mwezi wanasafisha miji yao. Je, sisi hatuwezi kuweka sheria kama hizo tukafanya usafi katika miji yetu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitarudi pale pale tu, sheria na taratibu mbalimbali ziko katika maeneo mengi tu wamejitengenezea taratibu hizi lakini nadhani bado jambo lenyewe hili linataka utashi wa namna fulani ndani ya jamii. Kwa hiyo, mimi nadhani tukazane kujenga utashi mkubwa utaona tutaweza kufanya hili jambo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu moja muhimu sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yetu katika kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha ustawi kwa watu wake, katika Bajeti ya mwaka 2010 ilitenga fedha kwa ajili ya kuwanusuru wakulima wetu kufuatia athari za mtikisiko wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukame uliokuwa umeendelea kwa miaka mitatu mfululizo katika Kanda ya Kaskazini mwa nchi yetu, umepelekea wafugaji wengi kupoteza mifugo yao hususani katika Wilaya za Longido, Ngorongoro, Simanjiro, Monduli, Kiteto, Hanang, Same na Mwanga na hivyo kusababisha umaskini uliotopea.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inasema nini sasa katika kuhakikisha kwamba watu hawa wanaanza maisha mapya kwa kuwapatia au kuwafanyia *restocking* au kuwapatia mifugo mingine ili waweze kuanza maisha sawa sawa na Watanzania wengine, ukizingatia kwamba wengine sasa hata watoto wao hawaendi shule nikichukua mfano wa Wilaya ya Longido? (*Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba ukame umeathiri sana maeneo ya Kanda ya Kaskazini. Nilipata nafasi ya kwenda Longido, Monduli na mara ya mwisho nilifanya ziara hata kwenye jimbo lake la Simanjiro na maeneo mengine. Ni kweli kabisa kwamba ukame ule umeathiri sana uwezo wa wananchi wa maeneo yale. Ng'ombe wamekufa wengi kiasi kwamba hata michango yao katika shughuli za maendeleo kama ujenzi wa madarasa sasa karibu umesimama kwa sababu hawawezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mawili hapa, jambo moja ni tufanye nini kujaribu kuona namna ya kuwasaidia wale wafugaji ambao kimsingi maisha yao kwa sehemu

yao yanategemea mifugo, kwa upande wa pili ni hizi huduma za jamii ambazo sasa zimeathirika sana kutokana na uwezo kupungua kutokana na wanyama wale wengi kufariki.

Mheshimiwa Ole-Sendeka, sina jibu la haraka kwa sasa hivi, lakini nimeshapokea maoni yanayofanana na ya kwako na sasa hivi tunayafanyia kazi kujaribu kuona katika mazingira haya Serikali inaweza ikafanya nini. Hatujafika mwisho lakini tulikuwa tumeomba kwamba tumepata maelezo kutoka Monduli na nilikuwa nimeagiza nipate maelezo kutoka Longido, Ngorongoro na baadhi ya maeneo ya Manyara ambayo yalikumbwa na ukame kama huo. Kwa hiyo, tukishapata maelezo na takwimu zote tukaziweka pamoja tutalipeleka rasmi ndani ya vikao vya Serikali kama tulivyofanya kwenye maeneo mengine ili tuweze kulizungumza na kuona tufanye nini mapema kwa kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na majibu yako mazuri yenye matumaini makubwa, nina swali moja lingine dogo tu kwamba kufuatia vifo vingi vya mifugo iliyotokea katika kipindi hiki cha miaka mitatu na hasa kwa mwaka 2009/2010 sababu mojawapo imetokana na miundombinu dhaifu na hasa kutokuwepo kwa maji, mabwawa na visima vya maji kwa ajili ya mifugo na wakati mwingine unakuta eneo linaimarishwa lakini halina maji. Serikali inaonaje ikiamua kutenga fedha sasa ili kuhakikisha kwamba mabwawa yanapatikana katika maeneo haya ya wafugaji ambapo kuna malisho lakini hakuna maji?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake ni mzuri kabisa. Ila tu nitashindwa kutamka kwamba fedha zitatengwa sasa kwa sababu kama nilivyosema wacha tulitazame *in totality.* Tutatazama na masuala yote ya miundombinu, lakini yako maeneo mengine vilevile ambayo itabidi yaangaliwe kwa maana ya kuwa na mfumo wa ufugaji endelevu utakaoweza kuwasaidia wafugaji hawa kuweza kuhimili matatizo ya ufugaji kwa hali ambayo itawaletea stahili nzuri zaidi. Kwa hiyo, tutaliangalia lote Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa sababu limeshatufikia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante tulikuwa na muda wa dakika tano ambayo tuliwasilisha hati mbalimbali kwa hiyo tunaendelea na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, moja ya kazi za Serikali ni kulinda Watanzania na mali zao. Kwenye mpaka wetu wa Ziwa Tanganyika ambao tunapakana na Congo, Watanzania wanaotoka Kigoma maeneo ya Kibirizi na Katonga na maeneo yote ya Mwambao wa Ziwa lile wanaibiwa sana mali zao hasa za uvuvi na mali hizo zinakwenda ng'ambo ya Tanzania. Naomba kujua Serikali inafanya nini ili kuwasaidia Watanzania hawa wanaohangaika na wanaibiwa mali zao kila siku lakini hatuoni juhudi zozote kusaidia kutatua tatizo hili ambalo ningeomba kujua kwa nini sasa Jeshi la Polisi lisianze kutumia hata helikopta kutafuta maharamia hawa wanaotumia silaha za kivita kuwavamia Watanzania hawa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba lipo tatizo la kiulinzi katika maeneo ya mipaka. Kusema kweli si eneo tu la Kigoma, lakini tunalo tatizo hili vilevile upande wa Mkoa wa Kagera, tunalo tatizo hili vilevile

Mkoa wa Rukwa na Kigoma yenyewe. Kwa hiyo, sasa hivi tulishapata maombi kutoka Mikoa hiyo mitatu ili kuweza kutazama uwezekano wa kuwa na operesheni maalum ya kuwasaka kwanza halafu kuweka misingi ambayo inaweza ikalinda usalama katika maeneo haya. Suala hili liko kwenye Wizara ya Fedha tunalihangaikia tuone kama tutaweza kupata fedha kwa ajili hiyo. Lakini nadhani kubwa ni hili alilolitaja kwamba tunatakiwa vilevile kuwa na mfumo endelevu wa kiulinzi ambao utawezesha muda wote kuwaweka Watanzania katika hali ya amani badala ya kungoja matukio ndipo mnaondoka kwenda kujaribu kukabiliana nao. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kabla sijauliza swali langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kutoa salaam za rambirambi na pole kwa ndugu zangu wananchi wa Mpanda Mjini kwa moto uliotokea jana usiku na kuunguza soko la Buzogwe. Kila jitihada zitafanywa ili kuhakikisha kwamba majanga haya tunajaribu kuyapunguza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mwezi Aprili, 2009 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alitoa kauli kwa niaba ya Serikali ya kusitisha zoezi la kuhamisha mifugo katika mikoa ya Rukwa na Morogoro kwa maana ya kusimamisha zoezi hilo. Na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu uliunda Tume ya kufuatilia kama taratibu zilikuwa sahihi na hakuna ukiukwaji wowote. Leo ni zaidi ya miezi kumi bado wananchi hawa wakulima na wafugaji wanaishi kwa uhasama. Serikali itatoa lini ufumbuzi wa tatizo la kudumu baina ya wafugaji na wakulima katika maeneo hayo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niungane nae, ni kweli kwamba soko limeungua pale Mjini Mpanda, taarifa hizo tulizipata jana usiku tunasema pole kwa Wanampanda, lakini Serikali imelisikia tutajaribu kufuatilia tuone chanzo na baadaye tujiulize tunafanyaje kwa sababu lilikuwa ni soko muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, ni kweli kwamba baada ya kuonekana kulikuwa na mvutano na matatizo mengi katika operesheni zilizofanyika, Serikali ilisitisha lile zoezi likaamua kwanza kuchukua hatua za kujaribu kusimamia utaratibu ambao utakuwa ni mzuri zaidi, lakini wakati ule ule kubaini hasa kilichotokea ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi ule ulikamilika taarifa ikaletwa Serikalini na hatukuchelewa tukawa tumepeleka kwenye mikoa husika kwa sababu kulikuwa na mambo mengine ya kiutekelezaji tu ambayo tulitaka yafanyike moja kwa moja ili tuweze kuwa na kitu ambacho sasa ni kamilifu. Wako watu walioonekana walikiuka taratibu na sheria tukasema wapelekwe Mahakamani na wewe unajua Mpanda tayari wengine wapo Mahakamani. Kwa hiyo, kazi ile ilishakamilika, lakini kwa maana ya zoezi hili kwa ujumla wake yako mambo matatu makubwa.

(i) Ni kuendelea kuwasihi Watanzania kwamba mkulima na mfugaji wote ni Watanzania na lazima tujitahidi kuona namna tunavyoweza kuishi kwa pamoja bila ya uhasama na kwa kuheshimiana. Kwa sababu hili ni jambo la msingi sana.

(ii) Serikali ilichofanya, imeamua kwamba badala ya kukaa tunazungumza matukio tutazame mkakati au mpango ambao unaweza ukawa ni suluhu ya muda mrefu ya tatizo hili. Kwa hiyo, tumeandaa kwanza mkakati ambao utazungumzwa na wadau, mkakati ambao unajaribu kuweka mawazo pamoja wakulima na wafugaji namna ya kusuluhisha migogoro inapotokea kati ya mkulima na mfugaji.

(iii) Lakini la tatu, tumeamua kama Serikali kwamba tufanye sensa ya mifugo nchi nzima kwa kila Mkoa, Wilaya, Tarafa mpaka kwenye vijiji ili tuweze hasa kujua idadi ya mifugo tuliyonayo ni kiasi gani unapolinganisha na uwezo wa malisho ya mifugo katika maeneo yote hapa Tanzania. Kwa sababu mpaka sasa kusema kweli tunakwenda kwa takwimu ambazo hatuna uhakika nazo sana. Kwa hiyo, zoezi hili tumeamua tulifanye mwaka unaokuja kwa kujua kwamba mwaka huu tuna mzigo mkubwa wa uchaguzi utatupa picha nzuri sana.

(iv) Lakini la nne, tumeona kwamba pengine tusingoje sana Serikali kwa kutumia vyombo vyake tuangalie maeneo yale sasa ambayo yana matatizo makubwa, bahati nzuri Mheshimiwa Ole-Sendeka ameliweka vizuri.

Tuanze kushughulikia maeneo hayo ili kuondoa uwezekano wa mifugo kutaka kuhama kutoka eneo moja kwenda lingine kwa sababu tu hakuna miundombinu ya msingi. Sasa naamini tukiyachanganya yote kwa pamoja na mpango endelevu na hasa baada ya mkutano ule wa mifugo tunaweza kabisa tukashughulikia jambo hili kwa upana na likatupunguzia tatizo tunaloliona leo. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelezo fasaha uliyoyatoa lakini yalitolewa majibu na Serikali kwamba zoezi lililofanywa Kilosa na Mbarali lilikusanya zaidi ya shilingi bilioni 1.2. Lakini katika fedha hizo zaidi ya shilingi 758,000,000/= zilitumika kama gharama za uendeshaji yaani ile operesheni na kiasi kidogo katika zile zilizobaki ndio zikapelekwa kwenye maendeleo. Je, unaridhishwa na matumizi makubwa kiasi hicho katika kuendesha operesheni na operesheni hizo zitakuwa na maana kama fedha zote zinatumika katika uendeshaji tu peke yake?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ile iliyotolewa kwenye Serikali haya maeneo yote yametazamwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana katika maelekezo yaliyokwenda viko vitu tumehoji mahsusi ili tuweze kupata maelezo ya msingi juu ya matumizi ya hizo fedha na yako mambo mengine makubwa zaidi juu ya matumizi ya hizo fedha ambayo tungependa vilevile na yenyewe yashughulikiwe katika kukamilisha maelekezo yale ndipo tuweze ku-*frame up* sasa uamuzi wa msingi kwa kila Halmashauri hasa kwenye matumizi ya fedha. Sababu tunaweza baadaye kuja kulizungumza pengine wakati wa Bajeti hata kama zile fedha zilipatikana lakini kama kusema hazijakwenda kujenga miundombinu kwa ajili ya mfugaji maana yake ni kwamba zoezi lote ulilolifanya halina maana hata kidogo kwa mfugaji umemtia hasara tu kwa upande mmoja. Kwa hiyo, nadhani lote litaangaliwa kwa pamoja halafu tutajaribu kuona namna nzuri ya kuweza kulikabili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana muda wa maswali umekwisha. Haidhuru leo maswali mengine yalikuwa mazito sana, lakini ufundi wako wa kujibu bado umejibu vizuri. Tunakushukuru sana na kukupongeza sana. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 158

### Mahitaji ya *Ambulance* - Kagera

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inapanga Bajeti kukidhi mahitaji ya Wizara husika kwa kuzingatia umuhimu wa Wizara hiyo; na kwa kuwa Serikali inapata misaada mbalimbali kutoka kwenye sekta ya afya vikiwemo vitanda, mashuka, dawa, pamoja na magari ya kubebea wagonjwa yaani *ambulance*:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusaidia wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa kuwapatia *Ambulance* ya kubeba wagonjwa kwa kuzingatia vijiji vilivyo mbali na hospitali ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipokea misaada na kununua magari ya kubebea wagonjwa na kisha kuyagawa katika Mikoa na Halmashauri kwa awamu kutegemeana na upatikanaji wa magari hayo. Migao hiyo imekuwa ikifanyika kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mazingira ya kijiografia na ukubwa wa tatizo. Kuanzia mwaka 2006 hadi 2008 jumla ya magari 63 yamegawiwa katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali Tanzania Bara. Mkoa wa Kagera umekwishapata magari matatu katika Halmashauri za Wilaya ya Ngara, Biharamulo na Bukoba. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha, Serikali haijaweza kugawa magari katika Halmashauri zote hivyo mpaka sasa jumla ya Halmashauri 67 katika Mikoa mbalimbali hazijagawiwa magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutenga fedha katika Bajeti za mwaka ili kuhakikisha kuwa Mikoa na Halmashauri zote nchini zinapata magari ya kubebea wagonjwa, Serikali itahakikisha kuwa jitihada hizi zinaendelea mpaka Halmashauri zote zipate magari. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 5.0, na mchakato wa manunuzi unaendelea ambapo inakadiriwa magari 50 yatanunuliwa na kugawanywa. Katika awamu hii baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Kagera zitafaidika na mgao huo, hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira mpaka magari hayo yatakapopatikana. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bukoba hatuna gari la kubebea wagonjwa, tulipata magari ya misaada yakaja yameharibika mpaka sasa hivi yako kwenye mawe. Ukilinganisha na Mkoa wa Kagera ulivyo mkubwa hatuna hospitali ya Wilaya tunategemea hospitali ya Mkoa peke yake na kwa kuwa Wilaya nyingi ziko mbali sana na Mkoa, lini Serikali itaona kuwawekea kipaumbele angalau wakapata magari mawili kulingana na Mkoa ulivyo mkubwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mbunge siwezi kupingana nae hapa. Ninachosema mimi naangalia katika *inventory* na naangalia kwamba ni nini kilichopelekwa kule. Inawezekana kabisa kwamba magari yamekwenda kule lakini kwa sasa hivi tunavyozungumza hayafanyi kazi.

Wewe kwa vile unatoka kule utakuwa unajua zaidi kuliko mimi ninayezungumza hapa. Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba tunachojua ni kwamba kuna magari 50 ambayo yatakuwa yamegawanywa kwa vigezo ambavyo tutakuwa tumejiwekea na kama wanataka kujua kwamba ni vigezo gani, tumesema wale watu ambao wako katika Halmashauri ambazo ziko katika mazingira magumu na zile ambazo zinaonekana kabisa hazina magari hayo hizo ndizo zitakazopewa kipaumbele. Kwa hiyo, wakati huo utakapofika tutafanya hivyo kama alivyokuwa ametushauri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na majibu mazuri ambayo amejibu Mheshimiwa Naibu Waziri kitambo kidogo kwa taarifa ya Bunge ni kwamba Manispaa ya Bukoba Mjini hivi juzi tu wamepata magari mapya ya wagonjwa ambayo yanafanya kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru kwa taarifa ya ziada labda ilikuwa bahati mbaya Mbunge alikuwa bado hajarudi kule. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 159

**Kuanzisha Umeme wa "*Biogas*" na "*Solar Energy*" Mashuleni**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya umeme nchini haijasambazwa katika sehemu zote za nchi na hivyo kufanya wanafunzi katika baadhi ya shule za msingi na sekondari kutumia vibatari, koroboi na mishumaa kujisomea usiku:-

Je, Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu wa kuhimiza shule husika kutumia malighafi walizonazo vijijini kuanzisha miradi ya umeme utokanao na *biogas* na *solar energy* kama ilivyofanywa katika baadhi ya shule katika Wilaya ya Serengeti kwa msaada wa Kampuni ya Hoteli ya Kitalii ya *Grumeti Reserves Co. Ltd.?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa huduma ya umeme nchini haijasambazwa katika sehemu zote. Aidha, ni kweli kuwa katika baadhi ya shule za msingi na sekondari wanafunzi wanatumia vibatari, koroboi na mishumaa wakati wa kujisomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali inatambua tatizo hili na ufinyu wa Bajeti katika nchi yetu ndio kikwazo kikubwa, ingawa juhudi zinaendelea ili kuhakikisha kuwa maeneo mbalimbali yanafikiwa na gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuhimiza teknolojia ya *Biogas* na umeme wa jua, Serikali inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na imeshaanza kufanya hivyo. Kama mtakumbuka katika Bajeti ya mwaka 2009/2010, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kusaidia maeneo yenye mazingira magumu kuhakikisha kuwa umeme wa jua unakuwepo katika shule na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti pamoja na Taasisi nyingine mbalimbali ambazo zimeonyesha juhudi za kueneza teknolojia hizo katika maeneo yao. Aidha, naomba kutoa wito kwa Taasisi mbalimbali kuangalia uwezekano wa kutumia teknolojia hiyo wakati Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa umeme wa gridi ya Taifa unafikia maeneo mengi hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali na Wizara imeandaa mpango wa kuweka maabara katika kila sekondari na kila Kata. Sasa kwa kuwa lazima maabara yaendane na umeme na umeme ni gharama. Je, Serikali imeandaa mpango gani wa kuhakikisha umeme wa aina zote tatu unafika katika sekondari hizi?

La pili, kwa kuwa suala la gridi alilojibu sasa hivi ni sahihi lakini suala la gridi ni suala ambalo linachukua muda mrefu sana mpaka lije lifikie maeneo ya kata zote na kwa sababu ni gharama na hilo tunaelewa na swali langu lilizidi kukita zaidi katika eneo la *solar energy* na *biogas* ambayo inatokana na kinyesi cha wanyama lakini pia na kinyesi cha binadamu. Sasa hizi sekondari ambazo zina watoto wengi wanasoma hivi tunaachia hiyo *waste product* iende hivi bila ya kutumiwa, kuna mpango gani wa kutumia eneo hili? Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wizara ya Nishati na Madini ina mipango mingi ambayo miongoni mwake inajielekeza katika kusambaza huduma za umeme katika maeneo mengi na hasa ya vijijini. Masuala yaliyoulizwa ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Janet Kahama yanahusu nishati mbadala. Nishati mbadala ni mojawapo ya mipango inayotekelezwa kupitia Wizara ya Nishati na Madini.

Naomba kupitia Bunge lako Tukufu nimshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Taasisi husika watuandikie Wizara ya Nishati na Madini na sisi kupitia Taasisi zetu kama Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* pamoja na Shirika la Umeme *(TANESCO)* na kwa sababu pale Wizarani tuna Kitengo maalum ambacho kinahusika na masuala ya nishati mbadala tuone ni jinsi gani tunaweza kusaidia taasisi hizo. Tumekuwa tukifanya hivyo kwa taasisi nyingi na tuna mipango mingi ambayo pia inaendeleza usambazaji wa huduma ya nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Ofisi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Yeye anachokisema shule zetu tumejenga nyingi na karibuni maabara yatakuwepo, sasa nishati gani tunaweza kutumia kwamba tukitegemea umeme tu haiwezekani. Je, hamuwezi kueneza *biogas, solar energy* kwa manufaa hayo, si kwamba ana *specific area,* hapana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru hicho ndicho ambacho nilikuwa nakisema kwamba suala la *biogas* ni mojawapo programu ambazo tunazifanyia kazi Wizara ya Nishati na Madini. Kwa kusema hivi ninamaanisha kwamba zoezi hili lilikuwa likiendelea katika sehemu mbalimbali Tanzania, ndiyo maana nasema kwa mahitaji maalum kwa sababu ni programu ambayo ipo lakini maeneo ya mahitaji ni mengi sana yanawezekana yakawepo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ana *interest* nayo angependa tuyashughulikie kutokana na hii nishati ya *biogas* ili tuweze kuyahudumia. Nilikuwa nasema ni vyema tukawasiliana nae ili sisi tulifanyie kazi hilo jambo. *(Makofi)*

Na. 160

**Alama za Barabarani**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE (K.n.y. MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA)** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo alama mbalimbali za tahadhari barabarani zenye madhumuni ya kuepusha ajali:-

Je, ni alama zipi muhimu zinazopaswa kuonyeshwa wakati chombo cha moto, hasa gari linapoharibika wakati likisafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo chochote cha usafiri yakiwemo magari, pindi yanapoharibika, dereva lazima atumie taa za tahadhari za gari hilo ambao ni za *emergency, indicator* zote aziwashe na ziwe zinawaka kwa pamoja. Dereva akumbuke kuwa gari linatakiwa

kuwa nje ya barabara, kama haliwezekani kutoka nje ya barabara anapaswa aliweke karibu na ukingo wa kushoto wa barabara na iwe mbali na makutano ya barabara, daraja au kona kali na sehemu nyingine zozote za hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hizo za awali, dereva anapaswa kuweka kiashiria chekundu cha pembe tatu *(reflective triangle)* karibu na ukingo wa barabara si chini ya umbali wa mita 30 nyuma ya gari na kiashiria kingine cha pembe tatu katika umbali ule ule mbele ya gari hilo. Kufanya vile kutafanya madereva wa magari yanayokuja mbele na nyuma ya gari hilo kuweza kuchukua tahadhari katika kulipita gari lililoharibika, sio kuweka majani au miti au magogo na hii kwa kweli imekuwa ni tabia mbovu, tabia chafu ambapo unakuta watu barabarani wameweka magogo, mawe na kwa kweli inaleta hatari zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hatua zote hizo za tahadhari zikifuatwa na dereva au madereva wote wanaoharibikiwa na magari yao kutaepusha ajali zinazotokana na uharibifu wa magari barabarani. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili mafupi ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa uwekaji wa majani, matawi, magogo na hata mawe umekuwa kitu cha kawaida sasa kuashiria kuwa gari limeharibika vitu ambavyo mara nyingi haviondolewi barabarani hata baada ya hilo gari lililoharibika kuondoka na hivyo kuwa chanzo kikubwa cha ajali. Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha tabia hiyo hatarishi?

Je, wajibu kisheria wa kuweka viashiria vyekundu vya pembe tatu *(reflective triangles)* unawahusu vilevile waendesha bajaji na mikokoteni vyombo vyao vinapoharibika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwanza hakika hilo tatizo tunalo na tumekuwa tunalisemea na tumejaribu kadri tuwezavyo kuchukua hatua. Lakini ifahamike kwamba haya matukio yanayotokea wakati mwingine sehemu ambazo kwa kweli kwa sababu ya uhaba wa usafiri wa askari wetu matrafiki kuweza kufikia na kuweza kuwachukulia hatua pale pale linatupa taabu niweze kukubali. Lakini ni kitu ambacho hakikubaliki na kitu ambacho tunakisemea mara kwa mara na nichukue nafasi hii hapa nilipo kuwaambia kwamba wale watu ambao wamekuwa na tabia hiyo kwa kweli inaleta hatari zaidi kuliko wao wanavyofikiria na tutajitahidi wale ambao wanapatikana hatua zinachukuliwa na tutajitahidi kuona kwamba kwa kweli tunachukua hatua kali tusiendelee na matatizo kama hayo.

Kuhusu hili la pili la *reflective triangle* kusema kweli hili linawabana wote, lakini watu wa mikokoteni kwa kweli Mheshimiwa Mbunge itakuwa ni taabu. Lakini kwa kweli watu ambao wana bajaji, sheria imepitishwa juzi na utaratibu ambao umeanza sasa hivi na sina uhakika lakini ni suala ambalo nafikiri tutalitazama lakini ninavyodhani kwa kuwa huu ni utaratibu wa kuondokana na *accident* katika barabara basi nadhani na wao linaweza likawahofu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Ningependa kumjibu kaka yangu, mwalimu wangu, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika kipindi cha hivi karibuni kumeongezeka na matatizo ya ajali barabarani na pia haya yametokana na uzembe wa madereva barabarani pamoja na vitendo vya watu kuweka *triangle* na vitu kama hivyo ambavyo vimeashiria ajali ambazo zimekwishatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kukufahamisha na Bunge lako Tukufu kwamba Jeshi la Polisi limeongeza vitendea kazi ili kuimarisha Kitengo cha *Traffic* na hivi sasa tunavyoongea tumeongeza zaidi ya pikipiki 50 ambazo zitakuwa zinafanya *patrol* katika barabara kubwa hapa nchini ili kudhibiti uhalifu wa madereva ambao wanaendesha vibaya barabarani, ambao wanavunja sheria za barabarani. Ningependa kuwahakikishia Watanzania kwamba Jeshi la Polisi lipo imara na tutajitahidi kadri ya uwezo wetu, moja kuhakikisha kwamba sheria za barabarani zinafuatwa na ajali za barabarani zinapungua.

**MHE. HILDA C. NGOYE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa *Captain* John Chilligati alishatamka hapa Bungeni kwamba ilipofika mwaka 2004 suala la uwekaji wa magogo na majani kama alama za barabarani lingekomeshwa wakati ule mara moja. Lakini tatizo hili bado linaendelea mpaka hivi leo, je, Serikali inatoa tamko gani sasa la kuhakikisha kwamba inakomesha kabisa tabia?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena ningependa kutamka kwamba kuweka vigogo barabarani na miti ni marufuku na askari polisi ambao wanaona vitendo hivi wanapewa amri ya kuchukua hatua mara moja. Napenda kuwafahamisha Watanzania kwamba kitendo cha kukiuka Sheria za Barabarani kitachukuliwa hatua kali sana hivi sasa na hatuwezi kuruhusu Watanzania kuendelea na tabia hii.

Na. 161

**Wazigua Wanaosihi Chogo – Jimbo la Handeni**
**Kwa Hadhi ya Wakimbizi**

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

(a) Kwa nini Wazigua waliokimbia Somalia kuepukana na adha na mateso waliyokuwa wakiyapata huko na kuja kuishi kwao Handeni wamepewa hadhi ya Wakimbizi na wengine hawajapewa uraia tokea miaka ya 1990?

(b) Je, ni lini watakuwa huru kuishi katika vijiji vya asili Wilayani Handeni badala ya kuwekwa kambini pale Chogo – Handeni ambapo kila wanachotaka kufanya lazima wapate kibali ikiwemo kusafiri?

(c) Je, utaratibu huo wa Serikali si unaweza kuashiriwa kuwa ni kitendo cha kuwanyima Wazigua hao haki zao za msingi katika nchi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wasomali waliokimbia Somalia na kuja kuishi Handeni wamepewa hadhi ya Wakimbizi kwa sababu hawajawahi kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na. 7 ya mwaka 1995. Mpaka kufikia Desemba, 2009 jumla ya Wakimbizi 1,423 kutoka Somalia wamekwishapatiwa uraia wa Tanzania wa kuandikishwa na mchakato wa kuwapatia uraia waombaji wengine 500 unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu huu unachukua muda mrefu kwa kuwa unafanywa kwa makini na kuzingatia usalama na maslahi ya nchi. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wakimbizi hawa watakuwa huru kuishi katika vijiji vya Wilaya ya Handeni au mahali pengine popote Tanzania mara tu watakapokuwa raia wa Tanzania, kwani Katiba ya nchi yetu inaruhusu raia wa Tanzania kuishi mahali popote watakapo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni kati ya nchi ambazo zinaheshimu haki za binadamu kwani pamoja na Wakimbizi hawa (Somali Bantu) kutakiwa kukaa katika makazi ya Wakimbizi bado wanazo haki zao za msingi kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998 *(The National Employment Policy)* ya mwaka 2008, pamoja na Sheria nyingine za Kimataifa zinazohusu masuala ya Wakimbizi. *(Makofi)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Serikali inakubali kwamba imebadilisha swali langu nililouliza? Kwa sababu swali la msingi lilikuwa Wazigua waliotoka Somalia sio Wasomali waliotoka Somalia; je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kwenda kuona kambi ile na kwenda kuona pale na kuona kwamba wanaoishi pale ni Wazigua?

La pili, ni lini kambi ile sasa itaondoka hadhi ya kuwa kambi ili mimi kama Mbunge niweze kuingia pale bila kuomba kibali chochote ili nikafanye kazi za Chama changu cha CCM na Serikali katika kuleta maendeleo katika eneo lile? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haiwezi ikakosea tukawakataa watu ambao ni watu wetu. Uhakika wa historia ni kwamba hawa ni Wasomali wa asili ya Kizigua lakini hawawezi kuwa Wazigua. Kwa sababu kihistoria hawa walihamia Tanzania si kwa ridhaa yao; wakati wa historia ya kupeleka watumwa kutoka Tanganyika, na sehemu zingine za Afrika; hawa walichukuliwa karne ya 18 na walikuwa wanakwenda sehemu mbalimbali za dunia.

Lakini hawa wa asili ya Kizigua waliotoka Tanga walikwamia maeneo ya Somalia na hawa tunaowaita Wazigua hawa ni kizazi cha nne. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Sheria zetu huwezi ukasema hawa ni Watanzania nafikiri huo ndiyo msingi wa kuanzia. Ndiyo maana tunajibu kwa kusema kwamba walivyorejea baada ya mapigano ndani ya Somalia baada ya kutolewa Siad Barre na matatizo ambayo yalitokea katika nchi ya Somalia, Wasomalia wametapakaa ulimwengu mzima. Wale waliokuja Tanzania na hususani maeneo ya Handeni, tumewafanyia utaratibu na Sheria ya Uraia wa Tanzania ya mwaka 1995 kwa watu hawa imepindwa kidogo ili kuwasaidia. Yapo masharti ambayo yamelegezwa kwa kuzingatia historia yao na kuzingatia nini kilitokea.

Lakini naomba niliahakikishie Bunge lako Tukufu na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hawa kwa kweli tunasema kwamba ni Wasomali wa asili ya Kizigua na si vinginevyo na ndiyo maana wanavyokuja inakuwa ni rahisi zaidi. *(Makofi)*

La pili, hatuwezi tukakiuka taratibu ambazo zinahusu makambi haya ya Wakimbizi na ndiyo maana bado utaratibu ambao tunaufanya na Shirika linaloshughulikia Wakimbizi bado Sheria zake zinabaki pale pale na hatuwezi tukazipinda kwa upande wa kambi moja na kwa sababu hiyo ningemwomba Mheshimiwa Mbunge atuwie radhi kwa sababu hapa Sheria ni msumeno tunakwenda kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo.

Lakini huruma ipo na ndiyo maana Serikali inakwenda kwa mbio sana kujaribu na kwa kiasi tumeweza kupunguza na kulegeza masharti na kuwapa Utanzania hawa watu tunaowaita Wazigua lakini tunaosema ni Wasomali wenye asili ya Kizigua.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wageni wanaokuja Tanzania wanachukua muda mfupi tu miaka mitano au kumi wanapata uraia. Hawa ni Watanzania wa asili lakini kwa bahati mbaya wanakutana na mazingira hayo. Kwa nini imechukua muda mrefu wao kuhalalishiwa uraia wao wakati kwanza wana asili ya Tanzania lakini kuna wageni wanakuja hawana asili hata kidogo ya Watanzania na wanapata uraia haraka hawa kwa nini mmechukua muda mrefu kiasi hicho?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Sheria ya Tanzania haimruhusu mtu ambaye ni mgeni ambaye ameingia nchini kwa kipindi cha miaka minne au mitano kupata uraia; kama hao wapo ningeomba anisaidie niwafahamu ili tuwachukulie hatua stahili na kuwanyang'anya uraia ambao wameupata kimakosa. *(Makofi)*

Ningependa kusisitiza kwamba kwa wale wakimbizi ambao wako pale Chogo, Serikali imeshaamua kwamba watapata uraia na sasa hivi tupo katika harakati za ku-*computerise* ile *system* ambayo itatuwezesha kutoa. Kati ya sababu ambazo imefanya harakati hii ichelewe ni

kwamba hii *system* imekuwa ni *manual* kwa muda mrefu lakini kwa sasa hivi *system* imeshakuwa *computerised* na naamini kabisa kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu wale wote ambao wako pale Chogo ambao walikuwa na nia ya kupata uraia wa Tanzania watapata. *(Makofi)*

Na 162

**Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji Mto Momba**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Je, Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa kilimo cha Umwagiliaji Mto Momba ambao unakadiriwa kuwa na heka 8,000 ambazo zikiendelezwa zitasaidia kuendeleza kilimo kwa vijiji vya kata ya Kipeta?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006 wataalamu wa kilimo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga walishirikiana na wenzao kutoka katika ofisi ya umwagiliaji ya Kanda ya Mbeya kufanya uchunguzi wa awali wa mradi wa umwagiliaji wa Maleza utakaotumia maji ya mto Momba.

Matokeo ya uchunguzi huo wa awali yanaonyesha mambo yafuatayo:-

(a) Kuna haja ya kupima eneo linalofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliajiukizingatia kuwa kuna eneo lililoko ndani ya hifadhi ya Uwanda ili kuepuka migongano inayoweza kujitokeza baadaye kati ya wakulima na wahifadhi.

(b) Ipo ardhi nzuri na maji ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, takribani hekta 4,000 zinaweza kuendelezwa maana zingine ziko ndani ya hifadhi.

(c) Mwamko wa wananchi katika kilimo cha umwagiliaji ni mkubwa isipokuwa kuna vikwazo ambavyo vinakwamisha kuendeleza kilimo ikiwemo ukosefu wa daraja imara la kuunganisha kijiji cha Kimasamba na Kata ya Kipeta. Hata hivyo maendeleo mafupi ya ujenzi wa barabara ya Mlowo - Mbozi ni kichocheo kizuri cha maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa umo kati ya mikoa sita yenye mazingira mazuri ya uzalishaji wa mazao hasa ya chakula na hivyo kuchangia vizuri katika usalama wa chakula. Kwa kutambua hilo Wizara yangu inafanya mawasiliano na Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili kiweze kupewa kazi ya upimaji ardhi ya mradi. Nimeishauri pia Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kuhakikisha kwamba mradi wa umwagiliaji wa Malezi unaingizwa katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Mradi *(DADPs)* ili uweze kuombewa

fedha katika programu ya kuendeleza sekta ya kilimo wa kuendeleza Umwagiliaji *(National Irrigation Development Fund).*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kabisa kwamba Mkoa wa Rukwa hauna wataalam wa *Irrigation* na Waziri wa wakati huo Mheshimiwa Charles Keenja ndiye aliyeniandikia barua mimi kupokea mradi huu kwamba utakuwa wa Wizara. Sasa yapata miaka saba na tunavyozungumza na kusema kwamba mradi huu utaingizwa kwenye Wilaya ya Sumbawanga haujawa mradi kwa sababu mchanganuo haujakamilika. Je, utatekelezwaje?

La pili, wakati Serikali yetu imeamua kuweka mkakati mzito katika kilimo; tunazo habari kwamba kule Kapunga ukiondoa Misri maana ndiyo ya kwanza kuwa na kiwanda cha kisasa cha kukoboa mpunga na Kapunga ni ya pili katika Afrika, habari tulizonazo ni kwamba shamba lile sasa halilimwi kwa sababu mwekezaji amemua kulima shairi. Je, hii ni sawa na Serikali inachukua hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutekeleza mradi huu wa Maleza napenda nirudie tena kumhakikishia kwamba mimi mwenyewe binafsi nimefuatilia mradi huu na tayari nimeshawaagiza Maafisa ya Kanda na kinachofanyika sasa ni kufuata taratibu zile kwamba uingizwe katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya na hili nimewaagiza kwamba itekelezwe kusudi tutakapoingia katika kupanga mipango ya mwaka 2011 basi mradi huu uweze kutokea. Naomba niamini kwamba tumechukua hatua na jambo hili litatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili labda niseme kwamba ni kweli; tulipoanza kutaifisha mashamba na hasa yale ya Mbarali na Kapunga lengo kubwa lilikuwa ni kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula. Shamba la Mbarali kwa taarifa nilizonazo linafanya vizuri kabisa wanaendelea vizuri isipokuwa hili la Kapunga yapo matatizo ya mwekezaji kuwa na mahusiano mabaya na wakulima wadogo wanagombea maji kwenye *intake* na wakati mwingine alitaka kulima jatrofa badala ya mpunga.

Mimi niseme kwamba tulikubaliana walime mazao ya chakula na Serikali imekwisha kataza shairi si zao ambalo mwekezaji yule alime. Yeye labda analima kwa *interest* zake lakini sisi tumesema alime mazao ya chakula. Kwa maana hiyo hata hicho kinu kikubwa anachokisema Mheshimiwa Mzindakaya na mimi nakifahamu, kama mpunga hautalimwa maana kinu kile kinakuwa *redundant*. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba mwekezaji yule tutaangalia hatua za kuchukua asiendelee kubadili yale tuliyokubaliana wakati anakabidhiwa shamba hilo.

Na 163

**Mbegu Bora za Kilimo**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kilimo bora nchini ni pamoja na maandalizi ya mbegu bora kwa wakulima;

(a) Je, Serikali inazitambua taasisi zipi zinazostahili kuzalisha mbegu bora za mahindi kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini?

(b) Je, katika kutoa ruzuku ya mbegu bora,ni utaratibu upi unaofuatwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mbunge, napenda kutoa rambirambi kutokana na kifo cha aliyewahi kuwa Mbunge wa Bunda Mheshimiwa Kanali Makunenge miaka ya 1990 kilichotokea wiki iliyopita na mazishi kufanyika wiki iliyopita katika kijiji cha Bugoji, Wilaya ya Musoma Vijijini. Nawapa pole wanafamilia na vilevile naungana na wananchi wa Jimbo la Bunda katika kuomboleza msiba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya taarifa hizo za kusikitisha naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Uzalishaji wa mbegu bora hapa nchini unaongozwa na Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 na kanuni zake. Ili mtu binafsi, kampuni au taasisi yoyote ile iweze kuzalisha au kufanya biashara ya mbegu bora hapa nchini ni lazima isajiliwe na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Taratibu hizi zinafanyika ili kuhakikisha ubora wa mbegu zinazosambazwa kwa wakulima unazingatiwa.

Kwa misingi iliyoelezwa hapa juu, Serikali inazitambua taasisi zinazostahili kuzalisha mbegu za mahindi kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Taasisi hizo ni pamoja na Kituo cha Utafiti cha Uyole ambacho huzalisha mbegu mama *(pre-basic seeds)* na kwa wakala wa mbegu za kilimo ambao huzalisha mbegu za msingi *(basic seeds)* na zilizothibitishwa *(certified seeds),* makampuni binafsi ya mbegu kama vile *Highland Seed Growers* ambayo huzalisha mbegu zilizothibitishwa *(certified seeds)* na vikundi vya wakulima wadogo ambao huzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(quality declared seeds).*

(b) Serikali inatoa ruzuku ya mbegu kwa kutumia mfumo wa vocha *(National Agricultural Input Voucher Scheme)* ambapo mfumo huu unahakikisha kuwa mkulima mdogo mwenyewe uwezo mdogo wa kununua pembejeo za kilimo anawezesha kununua na kutumia pembejeo zenye ruzuku. Katika mfumo huo wakulima hao huchaguliwa kupitia Kamati ya Vocha ya Kijiji *(Village Voucher Committee)* na majina yao hupitishwa na Serikali ya kijiji na hatimaye majina hayo hupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji. Utaratibu huu wa vocha unawawezesha wakulima walengwa kupata pembejeo za ruzuku. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa hapo awali Kituo cha Utafiti cha Uyole walizalisha mbegu ya mahindi ya 615 pamoja na 6303 na kuwauzia wananchi walikuwa wanakizunguka kituo kile na hivyo kuleta hamasa kubwa ya kilimo. Ni kwa nini zoezi lile la Kituo cha Utafiti Uyole halijawa endelevu kwa kuwapatia mbegu wananchi wanaozunguka eneo lile?

Pili, msimu huu wa kilimo wa mwaka 2009/2010, tumeshuhudia mahangaiko makubwa sana kwa wakulima wakitafuta mbegu ya Uyole *hybrid 619* na 6073 matokeo yake zilionekana mbegu ambazo ni za kutoka nje ya nchi au nchi jirani. Ni lini Serikali itawapa uwezo Wakala wa Mbegu wa Taifa kulitumia kikamilifu shamba la magamba kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu inayohitajika?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kituo chetu cha Uyole kinafanya kazi nzuri sana ya kuzalisha kwa njia ya utafiti na kupata aina mbalimbali ya mbegu pamoja na zile ambazo Mheshimiwa Mpesya amezieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho tumesema hapa katika Bunge hili ni kwamba pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika vituo vya utafiti bado changamoto yetu ni kuhakikisha ya kwamba mbegu zinazalishwa katika vituo hivyo zinazalishwa kwa wingi ili ziweze kumfikia mkulima. Sasa kama zilitumika pale Uyole ilikuwa ni sehemu ya utafiti kuonyesha kwamba zinaweza kufanyika lakini hazijazalishwa vya kutosha.

Sasa kazi tunayoifanya sasa hivi ni kuisaidia *ACA* iweze kutumia shamba la Magamba ambalo tumewakabidhi na mashamba mengine yaliyoko nchini na kwa kushirikiana na mashamba ya Magereza na JKT na wakulima wadogo ili tuweze kuzalisha mbegu kwa wingi. Kazi hiyo itaendelea na itafanyika. *(Makofi)*

La pili, kwa sababu sasa hivi hatujitoshelezi kwa mbegu zinazozalishwa hapa nchini na kwa kuwa tumekwishasema hapa kwamba sehemu kubwa ya mbegu ambayo inatumika hapa nchini zinatoka nje ya nchi kwa kuagizwa basi, kwamba ilifika huko na wakatumia mbegu inayoagizwa kutoka nchi za nje ndiyo hali halisi ilivyo kwa sasa; lakini shabaha yetu ni kwamba mbegu inayozalishwa hapa nchini iwepo kwa wingi katika siku zinavyokuja. *(Makofi)*

Na. 164

**Mikopo ya Pembejeo kwa Wakulima Wadogo Wadogo**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa mikopo ya pembejeo za kilimo hutolewa kwa watu wenye uwezo mkubwa na hati za kuweka rehani. Je, Serikali imeweka utaratibu gani kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo ambao hawana hati yoyote na wanahitaji mikopo hiyo?

**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo hutoa mikopo kwa wakulima ngazi mbalimbali wakiwemo wakubwa na wadogo wenye uwezo wa kuwa na dhamana zenye hatimiliki ambazo zinajumuisha; Hati miliki zilizosajiliwa na Wizara ya Ardhi, Leseni za Makazi na baadhi ya Hatimiliki za Kimila zinazotambulika kisheria, na ni kweli kwamba wakulima wadogo wadogo walio wengi hawana uwezo wa kuwa na dhamana zenye hatimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hili Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo imeweka utaratibu wa kuwapatia wakulima hawa mikopo kutumia.

(a) Dhamana ya Halmashauri ya Wilaya; katika utaratibu huu Halmashauri za Wilaya hutoa dhamana kwa kusaini mikataba ya kuridhia kuhakikisha mkopo uliotolewa unarejeshwa kwa wakati. Dhamana ya aina hii imetumika kudhamini Mifuko ya Pembejeo ya Wilaya.

(b) Dhamana ya Vikundi, katika utaratibu wa *SACCOS* na vikundi vilivyosajiliwa kisheria vinatakiwa kuwa na akiba sawa na theluthi moja ya mkopo wanayoomba. Akiba hii huwekwa katika taasisi zilizoingia mkataba na mfuko ambazo ni Shirikisho la Vyama vya Akiba na Mkopo *(SCCULT, 1992)* na kampuni ya Dunduliza.

(c) Dhamana ya Vyama vya Ushirika vya Msingi, katika utaratibu huu benki zilizoingia mkataba na mfuko hutoa mikopo ya pembejeo kwa Vyama vya Msingi vyenye hati za usajili. Benki ambazo hutoa mikopo ya aina hii ni Benki ya Wananchi Mbinga. Benki ya Wakulima ya Ushirika Kagare na Benki ya Ushirika Kilimanjaro.

(d) Dhamana ya wanunuzi wa mazao ya utaratibu huu unatumika kwa wakulima ambao wameingia mkataba  ya ununuzi wa mazao *(contract farmers)*. Katika utaratibu huu wakulima waliongia mikataba ya manunuzi hukopeshwa pembejeo au zana za kilimo kwa kudhaminiwa na mnunuzi wa mazao yao. Wakulima walionufaika na utaratibu huu ni chama cha wakulima wa chai Kagera. Chama cha Wakulima Chai Mufindi na wakulima watatu wa alizeti wa Mkoa wa Singida.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hatimiliki ya kimila bado utaratibu huu wa kupima maeneo unakwenda taratibu kwa hiyo wananchi wengi hawajapimiwa maeneo na kwa vile baadhi ya Halmashauri haina utaratibu wa kukopa na kuwakopesha wakulima wadogo wadogo. Je, Serikali ina utaratibu gani kuhamasisha Halmashauri waanze utaratibu huo ili wakulima wadogo wakopeshwe kupitia Halmashauri hiyo?

Swali la pili, kwa vile kuna maeneo mengi ambayo hawahitaji mbolea wanahitaji mbegu lakini wanalazimishwa kuchukua mbolea na usipochukua mbolea hutapata mbegu. Je, kwa nini wakulima hao wanalazimishwa kuchukua mbolea huku ardhi yao bado haihitaji mbolea?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu suala la Halmashauri kuwawekea dhamana wana vikundi vinavyokopa ni jambo ambalo Halmashauri zingine zinafanya kwa sababu sera inaruhusu. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu kwa Mheshimiwa Laizer ni kwamba angeshauriana na Halmashauri ya Longido kama ni tatizo maalum la pale ili kuona kwamba na yenyewe inashiriki katika kuwawekea dhamana ikiwa imeamini kwamba vikundi vile vinaweza vikalipa.

Mheshimiwa NaibU Spika, lakini Halmashauri ni sehemu na vyombo ambavyo vinasimamia maendeleo na maendeleo ya kilimo sasa yako chini ya Halmashauri hizi. Kwa hiyo, ni wao ndiyo wanaoweza kusema tunawaamini hawa na tunawawekea dhamana sera inaruhusu. *(Makofi)*

Kuhusu kutoa mbolea au mbegu kwa watu ambao wanalazimishwa kwa kweli hakuna watu ambao wanalazimishwa kupewa mbegu hizi isipokuwa tuliweka utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kuna mahala ambapo wakulima wenyewe wanadhani ardhi yao inafaa na ina rutuba ya kutosha na hawahitaji kuingia katika utaratibu wa kupata pembejeo, basi tunaweza tukaarifiwa na hatuwezi tukalazimisha wakulima kupokea pembejeo basi tunaweza tukaarifiwaa na hatuwezi tukalazimisha wapokee pembejeo ambao wao wanadhani hawaihitaji. *(Makofi)*

Na. 165

**Mradi wa Kujenga *Refinery* Kata ya Somangila - Temeke**

**MHE. IDD M. AZZAN (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga *refinery* eneo la Amani Gomvu, Kata ya Somangila, Temeke na wananchi kuthaminiwa mali zao kwa madhumuni ya kujenga *refinery*; na kwa kuwa hakuna taarifa zozote za mradi huo mpaka sasa kwa wananchi ambao wamezuiliwa maeneo yao kwa muda mrefu.

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani za mradi huo?

(b) Kama mradi huo haupo tena; je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi waliofanyiwa uthamini na kuzuiliwa kufanya lolote katika maeneo hayo kwa muda mrefu?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ulikuwepo mpango wa kujenga Kiwanda cha Kusafisha Mafuta ya Bidhaa za Petroli *(Petrolium Oil Refinery)* katika eneo la Amani Gomvu, Kata ya Somangila, lakini Serikali imesitisha mradi huo ili kuepuka athari mbaya za

mazingira *(Substancial Negative Environmental Impact)*. Hivyo imeamuliwa Mradi huo utafutiwe eneo lingine.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi wa awali uliopangwa kutekelezwa katika eneo hilo hautatekelezwa, Serikali imefanya mabadiliko ya matumizi ya ardhi hiyo kutoka kujengwa Kiwanda cha Kusafishia Mafuta ya Bidhaa za Petroli, na sasa eneo hilo limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara *(Real Estate Development)*. Taratibu za kuhakiki mali za wananchi na viwango vya fidia zimekamilika na kwamba fidia italipwa na mwekezaji ndani ya miezi mitatu ijayo kuanzia Februari, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kuwa viwango vya fidia vitakavyolipwa vitazingatia Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 inayosisitiza kwamba fidia lazima iendane na bei ya soko na hakuna mwananchi atakayepunjwa au kuonewa. Serikali inaendelea kuwaomba wananchi wa Amani Gomvu kutokuvamia eneo hilo kwa kuwa liko kwenye mpango wa kuendelezwa kwa mujibu wa Sheria za Ardhi na Mipango Miji. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kigamboni yote ni eneo lililoko katika mpango wa kujengwa mji mpya, lakini mpaka hii leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa; je, Mheshimiwa Waziri anasemaje katika hilo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba eneo la Kigamboni, siyo Kigamboni yote, lakini sehemu ya eneo la Kigamboni limetengwa kujengwa Mji Mpya wa Kigamboni.

Hatua iliyofikiwa sasa hivi ni kwamba tumepata mtalaam mwelekezi ambaye anachora *master plan* kuwa huo Mji Mpya utafananaje. Mwezi ujao, atatuletea hiyo *master plan* ili na sisi tuiangalie kama inafanana na kile tunachokitaka ili hatimaye lile eneo la Kigamboni liendelezwe kama Mji Mpya wa kisasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunatumia muda wa matangazo kumalizia maswali yaliyobaki. Tuaenda Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Na. 166

**Mabalozi Kutoka Zanzibar**

**MHE. DR. ALI TARAB. ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni ya Muungano:-

(a) Je, Mabalozi wangapi wanaoiwakilisha nchi yetu katika Balozi za nchi za nje?

(b) Je, Mabalozi wangapi kati yao wanatoka Tanzania Zanzibar?

(c) Je, ni asilimia ngapi ya Wanadiplomasia wetu katika Balozi hizo wanatoka Tanzania Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Tanzania ina Mabalozi 32 wanaoiwakilisha Tanzania nchi za nje.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nchi za nje wanaotoka Zanzibar ni wanne. Mabalozi hao wapo katika Balozi zetu za Rome - Italia, Cairo – Misri, Beijing – China na Muscat - Oman. Pamoja na Mabalozi hao, pia wapo Mabalozi Wadogo *(Consuls General)* kwenye Balozi zetu ndogo zilizopo Dubai – *UAE* na Mombasa – Kenya. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Wanadiplomasia wanaoiwakilisha Tanzania katika Balozi zetu wanaotoka Zanzibar ni 13 sawa na 24.2% ambapo wanaume ni kumi na moja na wanawake ni wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inafanya kila juhudi kuongeza watumishi zaidi kutoka Zanzibar kwenda kufanya kazi katika Balozi zetu mbalimbali zinazoiwakilisha Tanzania nchi za nje, pamoja na Idara ya Mambo ya Nje, Zanzibar. Zoezi hili hata hivyo linategemea sifa zinazostahili endapo maofisa hao watakuwa nazo ili kujenga, kuimaarisha na kudumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mabalozi wanne kati ya Mabalozi 32 ni asilimia 12.5; je, haujafika wakati huu sasa hivi ambao kuna Wazanzibar wengi tu wenye sifa na elimu ya juu ili kuifanya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa uonekane kama una sura ya Kimuungano?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nakubali kwamba Zanzibar inao vijana waliosoma, wenye elimu ya kutosha na wenye sifa za kutosha na ndio maana nimesema Wizara yangu itaendelea kuhakikisha kwamba idadi ya Mabalozi kutoka Zanzibar inaongezeka kila wakati inapohitajika. Sisi tutajitahidi kuhakikisha kwamba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inayo sura ya Muungano kwa kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Na. 167

**Mkataba wa Kubadilishana Wahalifu na Nchi za Rwanda, Burundi na Congo**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Kwa kuwa hadi sasa nchi yetu haina Mkataba *(Protocol)* wa kubadilishana wahalifu na nchi za Rwanda, Burundina na *DRC*, hasa ikizingatiwa kuwa wahalifu wengi hasa majambazi wanaotumia silaha katika Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa hutokea kwa kiasi kikubwa katika maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali itaandaa lini Mkataba huo na kuuleta Bungeni ili uridhiwe?

(b) Je, hadi sasa ni wahalifu wangapi waliofanya uhalifu katika Mkoa wa Kigoma na hususan Kasulu na kukimbilia nchi jirani?

(c) Je, Serikali imefanya juhudi gani kuwarejesha nchini wale wachache waliobainika (kukamatwa) ili wachukuliwe hatua za kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a), (b) na ( c ) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tayari ina Mkataba na Rwanda *(Etradition Agreement)* ambao unaruhusu kubadilishana wahalifu. Kuhusiana na nchi mbili zilizobaki, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara husika ambayo ni ya Mambo ya Ndani ya Nchi, itafanya utaratibu ili Tanzania iweze kuwa na Mikataba rasmi ya aina hiyo na nchi hizo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kujua takwimu za wahalifu wanaokimbilia nchi jirani bila wahalifu hao kuwa wamekamatwa. Hadi sasa hakuna takwimu hizo kwa kuwa hakuna aliyekamatwa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kurejesha watuhumiwa toka nchi za Burundi, *DRC* na Rwanda kwa kuwa bado zina machafuko ya kisiasa. Hata hivyo, hadi sasa Tanzania imefanikiwa kurejesha watuhumiwa wawili ambao ni raia wa Burundi waliohusika na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi *(Albino).* Wahalifu hao walirejeshwa kwa njia ya kirafiki kupitia makubaliano ya Kipolisi yaliyofanyika hapo awali katika vikao vya *East Africa Regional Polici Chiefs Cooperation Organization (EARPCO)* na *Southern Africa Regional Police Chiefs Cooperation Organization (SARPCO).*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nina maswali madogo tu ya nyongeza.

Kwanza, nishukuru kwa kuwa na Mkataba wa Kubadilishana Wahalifu na nchi ya Rwanda. Lakini swali langu la kwanza la nyongeza ni kwamba kwa nchi za Burundi na Congo - *DRC,* Naibu Waziri anasema itafanya utaratibu ili Tanzania iweze kuwa na Mkataba wa namna hiyo. Sasa ningependa kujua itafanya utaratibu huo lini kwa sababu wahalifu kama unavyoona

nchi hizi ziko tete kisiasa na wahalifu wanaongezeka. Nataka kujua *time line* ya Mkataba kwa Congo – *DRC* na Burundi ?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, jibu la (b) kwa maoni yangu limenishangaza kidogo. Ni dhahiri takwimu hizi zipo katika Jeshi la Polisi. Mwaka jana Mji wa Kasulu ulitekwa wote mchana kweupe na majambazi nane yenye silaha na zipo takwimu za Kipolisi kwamba hawa watu bado wamekamatwa wako kwenye magereza yetu. Nataka kujua *exactly* ni wangapi walikamatwa? Na mwaka jana huo huo, Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ilivamiwa na majambazi mchana kweupe tena wakiwa na mabomu na silaha nzito, ni dhahiri kuna takwimu katika Jeshi la Polisi. Sasa kunijibu hapa kwamba hawana takwimu, alijajibiwa swali hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, naomba swali (b) likafanyiwe utafiti ili lijibiwe vizuri na lijibiwe upya kwa sababu halijajibiwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpe pole sana Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa sehemu ya Jimbo lake la Kasulu kuvamiwa. Lakini, nimhakikishie tu kwamba Tanzania kama ilivyo kawaida yake, inajaribu sana kulinda usalama wa raia wake na mali zao na Serikali itajitahidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutajitahidi sana utaratibu huu wa kuwa na Mikataba hii na Burundi na *DRC* uanze haraka kwa sababu kuwa na Mikataba ya aina hii kuna mchakato mrefu kidogo kwa sababu inabidi kwanza tuwe na mazungumzo na wenzetu wa Burundi na *DRC* kabla hatujawa na Mkataba kamili.

Kwa hiyo, tutajitahidi, na ninawahakikishia kwamba tutajitahidi kwamba mchakato huu uanze haraka kadri inavyowezekana nikishirikiana na wenzangu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Kuhusu swali (b), nakubali, namhakikishia kwamba tutafanya utafiti, tujue ni kiasi gani hasa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa sababu hapa ametaja mambo ya polisi, ili tujue idadi kamili ya hao watu ambao anafikiri wamekamatwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umeisha. Sasa tunaendelea na kutambulisha wageni tulionao. Nina orodha ndefu kidogo ya wageni, kuna wengine nitawataja kwa ujumla wao.

Wageni walioko Bungeni asubuhi hii, kwanza ni wageni 35 wa Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni makada wa CCM kutoka Kata ya Sollya, Wilaya ya Manyoni wakiongozwa na Bwana Mohamed Suleiman. Bwana Mohamed Suleiman yeye ni Afisa Tarafa ya Kilimatinde. Sasa wale wageni 35 mahali walipo

wasimame tuwaone. Ahsanteni sana. Huyu ni Katibu mwenezi wetu wa Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo nadhani mtamfagilia vizuri. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini. Mgeni huyu anaitwa Bwana Henry Nyiti, ambaye ni Mkurugenzi wa *Interstate Mining and Minerals*, kampuni inayotafuta, kuchimba na kufanya biashara ya madini. Bwana Henry uko wapi? Ahsante sana! Karibu. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa ambao ni Mheshimiwa Diwani. Huyu Diwani, anasema ni shupavu sana wa Kata ya Mawengi Ludewa na wakala maarufu wa pembejeo za kilimo, Wilaya ya Ludewa, ni Mheshimiwa Leogard Mpambalyoto. Yuko wapi Mheshimiwa Diwani huyu? Ahsante sana, nasikia ni shupavu kweli. *(Makofi)*

Tuna ndugu Francis Lwoga, yeye ni wakala maarufu wa pembejeo za kilimo hususan katika Kata ya Ludewa, lakini vilevile maeneo mengine ya Ludewa na nje ya Ludewa. Bwana Francis Luoga yuko wapi? Ahsante, tumekuona.

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale ambao ni Mkurugenzi wa *The East African Nguvu Kazi Juakali Partners* kutoka Same, Kilimanjaro, ndugu Eliot Mnzava. Halafu tuna Profesa Peter Kamuzora kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Yuko wapi Profesa? Okay!

Tuna wageni nane kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, wakiongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Ludovic Utouh. Ahsante sana tunafurahi kuwaoneni. Bwana Ludovic Utouh, mimi nimesoma naye mambo ya uhasibu pale *IDM Mzumbe*. Karibuni sana. Kwanza kabisa tunashukurru sana kwa kazi nzuri unayofanya Bwana Utouh pamoja na timu yako. Siyo tu umeijengea heshima nchi, lakini Bunge letu nadhani limewezeshwa kufanya kazi yake vizuri sana kutokana na kazi yako. Kama mzalendo wa nchi hii, tunaomba uendelee vilevile na usiyumbe hata kidogo. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, ambao ni mke wake na binti yake wote wako hapa. Mke wake, *Mrs. Tarab* yuko wapi? Ahaa, na binti yuko wapi? Aaah, watoto wake! Karibuni sana! Sasa, katika hao, watoto wake ni Asia, Ortenblad na Easter Verita Pina. Asia na Ester ni wanafunzi wa *Masters Degree (MSC)* katika fani ya *Nursing Midwife* kutoka *Uppsala University* – Sweden, wako nchini kwa *field work* ya wiki nane pale *Muhimbili National Hospital*. Wale waganga wetu wako wapi? Ooh hongera sana! Mkimaliza huko, mnakuja kufanya kazi huku huku! Halafu tuna wajukuu zake, Melissa na Tariq watoto wa Asia Ortenblad, wasimame. Wale *grandchildren* wasimame basi, naona wako *shy*, *okay*, wapo lakini. *(Kicheko/Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa James Lembeli ambalo ni Mwandishi wa Habari wa *Radio Free Africa* na Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Shija Felician. Ahsante sana. Halafu kuna Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Paskali Ntale, kuna Katibu wa CCM Kata ya Nyihogo, Kahama Mjini Ndugu

Lucy Peter, halafu kuna Katibu wa CCM Tawi la Nyihogo, Kahama Mjini, Ndugu Hawa Kasonso. Ahsanteni sana, karibu sana naona mnafanya kazi yenu hasa wakati huu. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Eliatta Switi, Mbunge wa Viti Maalum, ni wanafunzi kutoka *St. John's University.* Naomba wote wasimame hawa wageni wa Mheshimiwa Switi, na pale wote ni akina dada, tunawatakia heri, mmalize kabisa shule, tunawahitaji. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesya, hawa ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi, yupo Katibu Kata wa Majengo, Ndugu Zulfa Mwalalika. Naomba msimame wote. Ahsante. Katika hawa yupo Katibu wa Uchumi Kata ya Majengo, Katibu wa Tawi Mlelwa Kata ya Maanga, Katibu Tawi la Kagwina Kata ya Sinde na yupo Mwenyekiti Mtaa wa Soko Kuu Kata ya Sisimba, Anna Mwakabonga. Yuko wapi? Nimemtaja kwa sababu wajina wangu! Ahsante sana! *(Kicheko)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja ambao ni wahamasishaji wanaoongoza kikundi kizuri cha waimbaji na sanaa ya maonyesho ambao ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kibo, Kata ya Ubungo, Ndugu Jovin Kione, amefuatana na Ndugu David Mponji. Hawa wawili, mmoja ni Katibu na mwingine ni Mwenyekiti. Katibu huyu ni wa Umoja wa Vijana wa CCM Kata ya Ubungo. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Diana Chilolo ambao ni mume wake ndugu Ernest Chilolo na msaidizi wa Mbunge Mwanjaa Kaunda. Karibuni sana. Tunakushukuru sana Bwana Chilolo, tunafurahi kukuona na mke wako anafanya sana kazi hapa. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 30 kutoka *Dodoma Association Training Centre*, wako wapi hawa wanafunzi kutoka *Dodoma Association Traing Centr*e? Aaa, *okay,* ahsante sana tunafurahi kuwaoneni. *(Makofi)*

Halafu tuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela ambaye ni Profesa Jwani Mwaikusya wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, yupo wapi Profesa? Aaah, ahsante sana. Profesa Mwaikusya vilevile ni Wakili pekee Mtanzania kwenye Jopo la Mawakili wa Utetezi Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Rwanda. Kwa hiyo, yuko kwenye kazi ya Kimataifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine wanaleta vikaratasi kuhusu wageni wao. Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Zaynab Vullu, wana wageni wao ambao ni Madiwani na Watendaji wa Halmashauri ya Kisarawe wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Jema Sela. Ahsante sana! *(Makofi)*

Halafu, Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ana mgeni wake anaitwa Bwana Pius Matare Gweso, sijui huku wanaita Museveni, ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Tailo. Yuko wapi Museveni wa Tanzania? Karibu sana ! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri mpeleke majina kule kusudi yaweze kuandikwa, kwa sababu hapa inakuwa kazi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, naomba nitoe matangazo ya kazi. Kwanza, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, yeye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 11 Februari, 2010, saa 7.00 mchana wakutane katika chumba namna 231.

Halafu, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana wakutane kwa maandalizi ya shughuli za Kamati katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo pia wakutane saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa B. Mtajuana huko huko, saa 7.00 pia mchana. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tena saa 7.00 mchana wakutane katika ukumbi namba 227.

Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, Bwana John Joel, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Ofisi ya Bunge imeongeza posho kwa siku tatu, hivyo Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mkajaze fomu za posho kwenye Ofisi ya Mhasibu, *ground floor*. Nafikiri ni kwa sababu hili Bunge lilikuwa liishe tarehe 9, tumeongeza mpaka leo, ndiyo sababu hiyo. Kwa hiyo, wote mnahusika.

Halafu, tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, anasema hivi, leo jioni saa 1.45 usiku, kutakuwa na Uzinduzi wa Riwaya au kitabu cha Kiswahili Mwele Binti Tabaan, kilichoandikwa na Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa. Spika wa Bunge Mheshimiwa Samuel Sitta atakuwa Mgeni rasmi kwenye sherehe hiyo fupi ambayo itahudhuriwa na wadau wote wa vitabu wakiwemo waandishi wa vitabu, wachapishaji na wasomaji. Wabunge wote mnaalikwa kwenye sherehe hiyo fupi ya kihistoria itakayochukua dakika 15 tu. *(Makofi)*

Kama sijasahau, nadhani jana pia mlitangaziwa kuwa kuna sherehe, sijui wapi...sherehe iliyotangazwa jana, leo ipo? Ile sherehe ya kuipongeza timu yetu iliyokwenda kushinda *East Africa*. Kwa hiyo, ipo sijui saa ngapi, tangazo halijaonekana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na shughuli.

## KAULI ZA MAWAZIRI

## KAULI YA YA SERIKALI KUHUSU TAULO ZA KIKE BANDIA AINA YA *“ALWAYS”*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika,kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni Na. 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu taulo za kike bandia aina ya *"always"* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 19 Januari, 2010, Tume ya Ushindani pamoja na Shirika la Viwango Tanzania ilipokea malalamiko kutoka Kampuni ya *Mek One General Traders Ltd.* ya Dar es Salaam kuhusu kuwepo kwa taulo za kike bandia aina ya *Always* katika soko la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Alama za Bidhaa Sura Na. 85 mapitio ya Sheria ya mwaka 2002, Tume ya Ushindani ambayo ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, ina jukumu la kudhibiti bidhaa bandia katika soko la Tanzania. Aidha, bidhaa bandia ni bidhaa iliyotengenezwa kwa kuiga nembo au alama ya bidhaa ya mmiliki mwingine bila ya ruhusa yake kwa nia ya kudanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia malalamiko hayo, Tume kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* ambalo lina jukumu la kusimamia ubora wa bidhaa na ambalo vilevile ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Jeshi la Polisi nchini, ilifanya msako na kufanikiwa kukamata jumla ya katoni 12,466 za bidhaa hiyo katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Kiasi hiki cha bidhaa kilikamatwa kwa nyakati tofauti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 21 Januari 2010, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Kampuni ya *Mek One General Traders Ltd.* lilikamata katoni 2,882 katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam, mali ya mfanyabiashara Mazeh Meghji. Aidha, tarehe 23 Januari 2010, katoni 8,110 za bidhaa hiyo hiyo zilikamatwa mjini Arusha, mali ya mfanyabiashara Paulo Augustino Lema, ambaye ndiye aliyeingiza bidhaa hii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kusaka bidhaa hiyo liliendelea na mnamo tarehe 29 Januari, 2010 kwa ushirikiano na Jeshi la Polisi, Tume ya Ushindani ilikamata katoni 1,221 katika mitaa ya Msimbazi na Mafia jijini Dar es Salaam, mali ya mfanyabiashara Elibariki Mollel na katoni zingine 253 zilikamatwa siku hiyo hiyo eneo la Manzese, jijini Dar es Salaam, mali ya mfanyabiashara Gabriel Massawe. Mpaka sasa ni jumla ya katoni 12,466 zimekamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua stahiki zimechukuliwa dhidi ya wafanyabiashara husika ikiwa ni pamoja na kutozwa faini na kuteketeza bidhaa hiyo kwa gharama zao. Jumla ya shilingi milioni 16.5 zimelipwa kama faini kwa mujibu wa sheria. Kwa mujibu wa Sheria ya Alama za Bidhaa, mfanyabiashara anayekiri kosa hutozwa faini isiyozidi shilingi milioni tano na gharama za kuharibu zisizozidi shilingi milioni mbili. Kwa mujibu wa sheria hiyo Bwana Lema ambaye ndiye aliyeingiza bidhaa hii nchini ametozwa jumla ya shilingi milioni saba, Bwana Mazeh Meghji ametozwa shilingi milioni 3.5; Bwana Elibariki Mollel shilingi milioni tatu na Bwana Gabriel Massawe ametozwa shilingi milioni tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za uchunguzi wa Tume zinaonyesha kuwa kiasi cha katoni 15,000 za taulo za kike bandia aina ya *Always* zimeingizwa katika soko la Tanzania

kinyume cha sheria. Kiasi kilichokamatwa ni sawa na asilimia 83 ya bidhaa zote. Tume ya Ushindani, Shirika la Viwango Tanzania na Jeshi la Polisi wanaendelea na msako katika mikoa mingine ili kuhakikisha kuwa bidhaa hiyo inaondolewa sokoni haraka iwezekanavyo. Mfanyabiashara Paulo Agustino Lema ambaye ndiye ameingiza bidhaa hiyo nchini anasaidiana na taasisi hizo ili kuhakikisha kwamba bidhaa hiyo inaondolewa sokoni. Nalipongeza Jeshi la Polisi na taasisi hizi mbili za Serikali kwa jitihada walizofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wananchi wote kwa ujumla hasa kina mama wenzangu kwa usumbufu wowote uliojitokeza. Wizara na Taasisi zake inapenda kuwahakikishia watumiaji wa bidhaa hiyo na wananchi kwa ujumla kwamba waendelee kutumia bidhaa halisi za *Always* kwa kuwa kiasi kikubwa cha bidhaa bandia zilizoingizwa nchini zimekamatwa kabla ya kuwafikia watumiaji. Hata hivyo wananchi wanatakiwa kuwa makini na kuepuka kutumia taulo hizo ambazo wanaweza kuzitambua kwani zinaonyesha zimetengenezwa Aprili, 2009 na Desemba, 2009. Vilevile zina maandishi ya *DRI Plus,* ambazo hazionekani katika taulo halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kudhibiti bidhaa bandia, hata hivyo wananchi wanaombwa kuona umuhimu wa kushirikiana na Serikali na Taasisi zake kwa kutoa taarifa mapema, mara tu wanapobaini kuwepo kwa bidhaa bandia ili hatua stahiki zichukuliwe kudhibiti bidhaa hizo ambazo zinaweza kuhatarisha maisha ya watu na uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uzoefu umeonyesha kwamba kwa kiasi kikubwa bidhaa bandia vilevile ni hafifu. Kwa mantiki hiyo utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa kabla hazijaletwa nchini ni muhimu ili kupunguza tatizo hili. Serikali inataka kufanya hivyo mapema iwezekanavyo kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko inatoa onyo kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote wanaojishughulisha na biashara ya bidhaa bandia ikiwa ni pamoja na kufutiwa leseni zao. Ni vema wafanyabiashara wote watambue kuwa katika soko huru suala la kufuata taratibu za biashara ni la lazima na siyo la hiari. Serikali itaendelea kuteketeza bidhaa bandia kama ambavyo imekuwa ikifanya bila huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia fursa hii kuwakumbusha watengenezaji na wasambazaji wa bidhaa zinazoigwa watoe elimu ya kutosha kwa watumiaji wa bidhaa zao ili waweze kutambua bidhaa halisi na kusaidia kupiga vita bidhaa bandia. Aidha, tunawashauri wafanyabiashara kuomba kupewa nakala ya cheti cha uwakala wa bidhaa wakati wa ununuzi wa bidhaa ili kuondoa tatizo la kudanganywa na kupata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ni mategemeo yetu kwamba watumiaji wa taulo hizi wawe makini kutochukua vitu ambavyo vina thamani ya chini ama vinahatarisha maisha yao. Kwa hiyo, wawe waangalifu wakati wa kununua. Tunaendelea Katibu. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 *(The Election Expenses Bill, 2009)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA**: Kabla sijamuita mtoa hoja nilikuwa nina tanagazo dogo. Tukiwa katika Bunge la *SADC* Bunge la mwisho lililofanyika Zimbabwe, Mheshimiwa Engineer alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati inaitwa *Democracy Governance and Gender Equality* ni Kamati kubwa sana katika *SADC n*a alichaguliwa bila kupingwa kwa hiyo Bunge la *SADC* lina Kamati za Kudumu tano, katika hizo mbili zinaongozwa na Watanzania maana yake nyingine inaongozwa na Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, na mara zote hata akitaka kutoka Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa watamng'ang'ania tu na mimi Naibu Spika ni Makamu Mwenyekiti wa Bunge *SADC.* Kwa hiyo, kwa asilimia kubwa Bunge la Tanzania linaongoza *SADC. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye Muswada wa Sheria wa Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 *(The Election Expenses Bill 2009*). Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshugulikia mambo ya Bunge.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liupokee, liujadili na hatimaye kuupitisha Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 *(The Election Expenses Act, 2009).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maelezo ya muhtasari kuhusu Muswada huu, napenda kukushukuru kwa fursa uliyonipa ya kuuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Pili namshukuru sana Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Peniel Lyimo, Msajili wa Vyama vya Siasa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria na wataalam wake pamoja na wadau mbalimbali walioshiriki katika kutoa michango mizuri sana katika uboreshaji wa Muswada wa kutunga Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 *(The Election Expenses Act, 2009).* Pia napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na wajumbe wa Kamati yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua hii ningependa kutoa taarifa kwamba Muswada ambao wamegawiwa Wabunge, Muswada ambao umechapishwa upya badala ya kutoa majedwali ya marekebisho mbalimbali yaliyotolewa kwanza na wadau wa Muswada huu vyama vya siasa na Kamati ya Bunge na asubuhi hii pia itatolewa jedwali dogo kwa ajili ya marekebisho mbalimbali madogo madogo ya kitaaluma ambayo yameonekana pia katika Muswada ambao ulichapishwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 na hata kabla ya hapo na pia baada ya Jamhuri ya Tanganyika kuungana na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar tarehe 26 Aprili, 1964 nchi ilikuwa na chaguzi za aina mbalimbali.

Katika chaguzi zilizoshirikisha vyama vingi vya siasa mwaka 1995, 2000 na 2005 yamekuwepo malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali hasa vyama vya siasa na wagombea kuwa uwanja wa siasa hauko sawa kutokana na baadhi ya vyama vya siasa na wagombea kukosa fedha za kugharamia shughuli za uchaguzi, hivyo kushindwa kutumia haki yao ya Kikatiba iliyopo katika Ibara ya 21 na 21(1) ya mwaka 1977.

Pia vyama na wagombea wenye fedha nyingi kuzitumia katika kampeni bila kikomo na kufanya ushindani katika uchaguzi usiwe dhahiri na sawa na kumekuwa na hisia kuwa wale wenye fedha huchaguliwa kwa sababu ya fedha zao na siyo kwa sababu ya ama uwezo wao au sera za vyama vyao. Lakini kwa hakika pia siyo tabia nzuri hata kidogo kwa viongozi kama vile Madiwani, Wabunge hata Rais kutegemea zaidi fedha ili kupata nyadhifa hizo; japokuwa haiwezekani kukwepa matumizi ya fedha katika michakato ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza namna bora zaidi ya kusimamia matumizi ya fedha nyakati za uchaguzi, na ndiyo maana basi Muswada huu unapendekeza namna bora zaidi ya kusimamia matumizi ya fedha nyakati za uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia malalamiko hayo, mwaka 2006 Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kubaini tatizo hili aliagiza taasisi mbalimbali nchini zinazohusika na chaguzi kulifanyia kazi suala hili. Sababu za msingi za agizo la Mheshimiwa Rais zinaongezewa nguvu zaidi na maamuzi ya Mahakama Kuu ya Tanzania, katika Shauri la Madai Na.77 la mwaka 2005 lililohusu uhalali wa Sheria inayoruhusu kutoa takrima kwa misingi na utamaduni wa Kiafrika, na Mahakama kutoa uamuzi kuwa utaratibu wa takrima unatoa mwanya kwa wagombea kutoa rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo katika mazingira haya Serikali imeona iko haja ya kuimarisha demokrasia ya uchaguzi kwa kuhakikisha kwamba kunakuwepo kwa mazingira yaliyo sawa kwa wagombea wakati wa uchaguzi ili kuweza kupata viongozi wenye uwezo wa kuongoza na kuwaridhisha wananchi kwa ushawishi wa sera na siyo fedha. Katika kutimiza dhamira hii, Serikali imeamua kuleta Sheria mpya iitwayo *Election Expenses Bill* ili kuweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu mapato, matumizi ya gharama za kampeni na uchaguzi.

Madhumuni ya Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ni pamoja na kuweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu gharama za uchaguzi kwa vyama vya siasa na wagombea wake ili kuondoa upungufu uliopo sasa katika Sheria za Uchaguzi, Maadili ya Viongozi wa Umma na Vyama vya Siasa, kuweka utaratibu wa kisheria utakaofanya uwanja wa ushindani katika chaguzi kuwa sawa na halisi, kudhibiti vitendo vya rushwa na matumizi makubwa ya fedha katika kampeni na uchaguzi wa vyama vya siasa na wagombea, kuweka utaratibu wa kisheria na kuratibu zawadi, misaada na michango itakayotolewa na kupokelewa na vyama au wagombea wakati wa kampeni za uchaguzi. Aidha, sheria hii inalenga katika kuweka utaratibu na kudhibiti matumizi ya fedha wakati wa Kampeni za Uchaguzi na kuweka mfumo wa kisheria wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha na vilevile kuainisha adhabu kwa watakaokiuka

masharti yaliyomo katika Sheria inayopendekezwa na pia kuweka maadili ya uchaguzi yatakayokuwa na nguvu za kisheria tofauti na maadili ya sasa ambayo yalikuwa yanazingatiwa kwa hiari na vyama vya siasa na wagombea wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawasilisha Muswada huu leo mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya kupata mawazo mazuri ya wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, wananchi na asasi za kiraia, jambo ambalo limewezesha kuboreshwa kwa Muswada huu na ndiyo maana tukalazimisha uchapishwe upya. Ni matumaini yangu kwamba michango yenu ambayo mtaitoa leo baadaye wakati wa kujadili Muswada huu itasaidia kuuboresha zaidi Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu nane. Sehemu ya kwanza inaweka masharti kuhusu mambo ya utangulizi ambayo ni jina, tarehe ya kuanza kutumika, kutumika kwa sheria hii katika Tanzania Bara na Zanzíbar na tafsiri ya maneno na misamiati. Sehemu ya pili inaorodhesha kazi za Msajili wa Vyama vya Siasa ikiwemo mamlaka ya kusimamia na kukagua gharama za uchaguzi kwa vyama vya siasa na mwenendo wa wasimamizi wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu inapendekeza masharti kuhusu fedha zitakazotumika kwa ajili ya uchaguzi, maana ya gharama za uchaguzi, uchaguzi ndani ya vyama vya siasa, gharama ambazo vyama vya siasa vinapaswa kutumia wakati wa uchaguzi, masharti kwa vyama vya siasa na wagombea kutoa taarifa kuhusu gharama zitakazotumika wakati wa uchaguzi. *(Makofi)*

Aidha, sheria inaweka sharti la kutoa taarifa kuhusu michango au misaada inayotolewa na kupokelewa na vyama vya siasa, kuzuia fedha kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kampeni za uchaguzi na matumizi ya gharama kwa vyama na taasisi zisizo za kiserikali wakati wa kutoa elimu ya kampeni na chaguzi za kisiasa siku 90 kabla ya Uchaguzi Mkuu na siku 30 kabla ya uchaguzi mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne inaweka masharti kuhusu uwajibikaji wa Vyama vya Siasa, kwa kuvitaka vyama hivyo kutoa taarifa ya fedha zilizotumika wakati wa Kampeni za Uchaguzi, kutoa nyaraka au maelezo kwa matumizi ya fedha wakati wa Kampeni, kuwasilisha hesabu za matumizi na kuweka kumbukumbu sahihi za gharama za uchaguzi. Sheria inaelekeza kuwa Chama cha Siasa na Wagombea wake katika uchaguzi wanaweza kuzuiwa kushiriki katika uchaguzi endapo watakiuka masharti yaliyopo kwenye Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano inapendekeza masharti yanayokataza baadhi ya matumizi ya fedha kama gharama za kampeni na uchaguzi. Matumizi hayo ni yale yanayohusu gharama kwa vitendo vinavyozuiwa na Sheria na pia Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na pia Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1978. Sehemu hii inakataza vitendo vya wagombea kuwasafirisha wapiga kura kwenda vituo vya kupigia kura kwa nia ya kuwashawishi ili wawapigie kura. *(Makofi)*

Sehemu ya sita inapendekeza makosa ya ujumla pamoja na adhabu zinazoweza kutolewa kwa kukiuka masharti ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba inaweka masharti kuhusu haki ya wagombea wa Ofisi ya Rais na wagombea wenza kutumia vyombo vya habari na wajibu wa Serikali na vyombo vya habari hasa vile vya umma kuwawezesha kuitumia haki hiyo. Aidha, sehemu hii pia inaipa Serikali wajibu wa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kwamba vyama vya siasa, wagombea wao na wapiga kura wakati wa kampeni wanawafikiwa bila ubaguzi wala kupewa vitisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane na ya mwisho inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuoanisha masharti ya Sheria hiyo na Sheria hii mpya. Marekebisho ya msingi ni kuongeza kifungu cha 13A katika Sheria ya Vyama vya Siasa kwa lengo la kuweka utaratibu utakaowezesha Msajili wa Vyama vya Siasa kupata taarifa juu ya mgombea au chama cha siasa kinachojihusisha na vitendo vya ukiukaji wa masharti ya sheria hii au Sheria ya Uchaguzi wakati wa kampeni za uchaguzi na pia wakati wa kura za maoni na pia hata kabla ya hapo. Aidha, kifungu hicho kinaweka utaratibu utakaowezesha kuhifadhi utambulisho wa watoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi na kabla sijaomba kutoa hoja napenda kutoa taarifa kwamba Sheria hii pia sasa inasababisha mabadiliko makubwa katika Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 ambao Muswada wake utaletwa mara tu baada ya Waheshimiwa Wabunge kuupitia Muswada huu na iwapo wataukubali basi Muswada utakaofuata utakuwa umeweka maanani masharti ya Sheria ya Muswada huu, sasa baada ya maelezo hayo naomba kwamba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu na kuupitisha ili uweze kutumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hii sasa imetolewa na kuungwa mkono, sasa nitamuita Mwenyekiti au mwakilishi wake wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu. Naona mwakilishi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge Viti Maalum. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, idhini yako kabla sijatoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2009.

Naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru sana kwa heshima na taadhima wananchi wote wa Mkoa wa Iringa, kimsingi ambao kwa baraka zao asubuhi ya leo nimeweza kusimama hapa na kupata nafasi ya kutoa maoni haya ninasema asanteni sana ninawashukuruni sana Wanayalukolo wote wa Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 *(The Election Expenses, Bill, 2009).*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, tarehe 18

Januari, 2010, Kamati ilikutana katika ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam na kupata maelezo ya Serikali kuhusu Muswada huu. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Ofisi ya Bunge ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari kwa madhumuni ya kuwaalika wadau wafike kwenye kikao cha Kamati na kutoa maoni yao. Katika Kikao hicho, Mheshimiwa Waziri ilieleza kuwa nchi nyingi duniani zimekuwa na udhibiti na usimamizi wa matumizi ya fedha wakati wa uchaguzi, jambo ambalo Kamati imeafiki kuwa lina ukweli na mifano ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilielezwa kuwa Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa sheria inayoweka pamoja na mambo mengine utaratibu wa kisheria wa kusimamia na kuratibu matumizi ya gharama za kampeni kwa vyama vya siasa. Utaratibu huu unalenga kuweka mazingira yatakayowezesha kuwepo kwa uwazi zaidi katika matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kuelezwa madhumuni na sababu, Kamati pia ilielezwa mambo muhimu yanayolengwa katika mapendekezo ya Serikali kuhusu Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Mambo hayo ni ukomo wa michango, michango inayozuiliwa, ukomo wa matumizi, kutangazwa kwa mali/fedha za kampeni na uchaguzi *(public disclosure)* na mchango wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kupokea maelezo ya Serikali, ilipata fursa ya kuwasikiliza wadau waliofika mbele ya Kamati. Wadau hao walitoka vyama 12 vya siasa nchini, watu binafsi na asasi nane zisizokuwa za Kiserikali. Utaratibu wa Kamati uliotumika kuwasikiliza wadau uliwapa nafasi kuelezea maoni yao na baadhi yao kuyawasilisha kwa maandishi ili yafanyiwe kazi. Naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni na mapendekezo yao katika kusaidia Kamati kuboresha Muswada ulio mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa navishukuru vyama vya siasa nchini na asasi zisizo za Kiserikali kwa kutenga muda wa kuchambua Muswada huu na kutoa maoni ambayo kwa sehemu kubwa yamepokelewa na Serikali.

Aidha, nachukua fursa hii kuipongeza ofisi yako kwa utaratibu mzuri wa kuwaalika wadau kwa njia ya kuwaandikia barua na kupitia vyombo vya habari. Utaratibu huu unasaidia kwa kiasi kikubwa kuwashirikisha wananchi kwa karibu zaidi katika mchakato wa kutunga sheria kwa kushirikiana na chombo cha wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu Muswada huu umevuta hisia na usikivu wa watu mbalimbali kutokana na shabaha na madhumuni yake. Kabla ya kuendelea, nikiri kwamba suala la kudhibiti matumizi ya pesa katika mchakato wa kisiasa kwa misingi ya sheria mahususi ni jipya katika historia ya Tanzania. Kwa sababu hiyo, Kamati ililazimika kufanya uchambuzi wa kina zaidi na kwa umakini wa hali ya juu ili kuzingatia mambo yote muhimu

kisheria bila kuathiri misingi madhubuti ya demokrasia. Kamati ilifanya jumla ya vikao viwili mjini Dar es Salaam ambapo Serikali ilikubali maoni kadhaa ya Kamati kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na wadau tarehe 18 Januari, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 na 9 Februari, 2010 Kamati ilikutana tena mjini Dodoma ili kujiridhisha katika marekebisho yaliyofanywa na Serikali katika sehemu mbalimbali za Muswada huu. Katika vikao hivi Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 114 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 na kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wengine ili kupata maoni zaidi. Nichukue fursa hii tena kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika vikao hivi na kutoa mchango mkubwa kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao tulivyofanya mjini Dodoma, njia iliyotumika iliruhusu Waheshimiwa Wabunge kujadili ipasavyo kila Ibara kabla ya kuingia Ibara nyingine. Pale ilipotokea kutofautiana kwa hoja maridhiano yalifikiwa kwanza baina ya Waheshimiwa Wabunge na kisha baina ya Kamati na mtoa hoja. Majadiliano yalikuwa ya kina na wakati mwingine sheria mbalimbali na kesi zilizowahi kuamuliwa na mahakama zilirejewa. Kwa mfano, Ibara za 13 na 65 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka wa 1977, zinazohusu usawa mbele ya sheria na muda wa Ubunge ni miongoni mwa rejea zilizotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kimsingi Kamati inakubaliana na hoja ya Serikali katika mapendekezo ya jumla kuhusu Muswada huu. Kamati imezingatia sana umuhimu wa kuwa na sheria inayodhibiti matumizi ya fedha katika mchakato wa uchaguzi. Bila shaka Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kuwa uchaguzi ni moja ya mambo muhimu sana katika mchakato wa kisiasa. Mara baada ya kubadili mfumo wa siasa tuliokuwa nao, sote ni mashahidi kuwa ushindani wa kisiasa uliongezeka kulingana na mabadiliko haya ya kidemokrasia. Katika mfumo mpya wa kisiasa tuliouanza kuna hisia kuwa ushindani uliopo unahitaji utaratibu mahususi wa kudhibiti namna ya kushindana kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilizingatia kuwa iwapo kutakuwa na udhibiti wa matumizi ya fedha katika mchakato wa uchaguzi, kwanza, tutakuwa na mfumo madhubuti unaozuia uwezekano wa kupata watu wasio na sifa katika uongozi. Pili, mfumo wa demokrasia yetu utahifadhi haki na usawa katika kampeni kwa kuzuia matumizi ya fedha kupita kiasi na tatu, itasaidia kuondoa wasiwasi katika namna wanavyopatikana viongozi muhimu wa kuchaguliwa na wananchi jambo ambalo lina faida kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, pamoja na kukubaliana na mapendekezo ya Serikali, kwa ujumla Kamati ilikuwa na maoni na ushauri katika Ibara mbalimbali za Muswada kama ulivyowasilishwa mbele ya Kamati. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati ilipokelewa na Serikali iliiahidi Kamati kwamba itazingatia mapendekezo yaliyotolewa kwenye vikao vya Kamati. Mapendekezo hayo ni yale yaliyotolewa katika vikao vya Dar es Salaam na vile vilivyofanyika mjini Dodoma kama nilivyoeleza hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo nianze kwa kueleza maoni ya Kamati kuhusu jina refu la Muswada kwa kuwa sehemu hii inataja kwa kifupi madhumuni ya msingi ya sheria inayopendekezwa, kwa kuzingatia sababu za mapendekezo yanayotolewa na Serikali katika Muswada huu, Kamati ina maoni kuwa jina refu la sheria inayopendekezwa linaweza kuboreshwa kwa kuweka vitu kama nukta, koma, mara baada ya neno *funds* katika mstari wa tatu na kuondoa neno *and* lililopo baada ya neno *funds* ili kuweka kifungu cha maneno *to prevent.* Kwa ushauri huu jina refu la Muswada lisomeke kama ifuatavyo; *"An act to make provisions for the funding of the nomination process election campaign and election with a view to control the use of funds, to prevent illegal practice in the nomination process, election campaign and elections, to make provision for allocation management and accountability of funds and to provide for consequential and related matters."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu kuna mazoea ya kuweka maelezo ya madhumuni na sababu katika sehemu ya mwisho ya Muswada, maelezo hayo yametolewa kwa lugha zote mbili, yaani Kiingereza na Kiswahili hata hivyo Kamati imebaini kuwa maelezo yaliyotolewa kwa Kiingereza kuhusu sababu na madhumuni yanatofautiana kimantiki na maelezo yaliyotolewa kwa Kiswahili, inaonekana kuwa maelezo ya Kiswahili yanafanana vizuri na kueleweka vyema kuhusu nini hasa malengo ya Muswada kuliko yale maelezo ya Kiingereza. Kamati inashauri kuwa kwa siku zijazo mazoea hayo ya lugha mbili yazingatie umuhimu wa lugha hizo kutotofautiana kimantiki.

Kuhusu madaraka ya Msajili kwa Vyama vya Siasa, mapendekezo ya Serikali yanampa madaraka makubwa Msajili kama vile kuingia au kuamuru kuingia eneo lenye nyaraka na kukagua au kuchunguza kumbukumbu za chama cha siasa kwa kujibu wa Ibara ya Tano na kutaka taarifa zinazohusu gharama za uchaguzi au mgombea kama inavyoruhusu Ibara ya Sita, aidha Ibara ya Tisa sehemu ndogo ya pili na ya tatu inalazimisha Vyama vya Siasa kumpa Msajili maelezo kuhusu kiasi cha fedha kilichotumika na kinachokusudiwa kutumika kwa shughuli za Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine la Madaraka ya Msajili linaonekana katika Ibara ya 11(3) ambapo Vyama vya Siasa vinatakiwa kumpa taarifa juu ya kiasi cha fedha kilichokusanywa na kuchangishwa kwa ajili ya kampeni za uchaguzi. Aidha, Ibara ya 13(4) inazitaka asasi zisizokuwa za Kiserikali, taasisi za dini au asasi za kiraia kupeleka hesabu zinazohusika na gharama za uchaguzi iwapo watakuwa wamehusika katika uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii pia itavitaka vyama vya siasa kupeleka hesabu za matumizi wakati wa uchaguzi kama inavyopendekezwa katika Ibara ya 17(3) na Ibara ya 18(2) Ibara ya 19(2). Katika Ibara ya 19(3) Msajili anatakiwa kutoa mwongozo wa namna ya kuweka kumbukumbu ya matumizi ya fedha ya vyama au wagombea wakati wa uchaguzi. Mapendekezo ya Serikali katika Ibara za 20 na Ibara ya 24 kama yalivyokuwa katika Muswada tangu awali yanaongeza madaraka ya Msajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na marekebisho yaliyofanywa na Serikali katika Ibara ya Tano ya Muswada ulioletwa awali, Kamati inaendelea kushauri kuwa aina za nyaraka

zitakazotumika katika ukaguzi zibainishwe kwa umakini mkubwa ili kulinda baadhi ya nyaraka za vyama ambazo si vyema kukaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine wa marekebisho yaliyozingatia ushauri wa Kamati ni kama Ibara ya 10 ya Muswada kama ulivyokuwa tangu awali katika Ibara ya 10(1)(a) yanatajwa mambo ya kuzingatia wakati Waziri akieleza ukomo wa kiasi cha fedha kwa ajili ya gharama za uchaguzi, Kamati ilishauri kuwa sheria hii izingatie namna ya kuwafikia wapiga kura kwa urahisi, ushauri ambao pia ulipokelewa na Serikali. Pamoja na usikivu huo wa Serikali Kamati inashauri kuwa Sheria hii imtake Waziri kushirikiana na vyama vya siasa katika kupanga ukomo wa juu katika kiasi cha gharama za fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii niliyoitaja ni mifano michache tu ya miongoni na ushauri uliofanyiwa kazi na Serikali katika kuboresha Muswada huu, zipo Ibara zingine kadhaa zimeboreshwa baada ya kufanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa kwenye vikao vya Kamati, naishauri Serikali kwa uelewa na ushirikiano wa hali ya juu katika mchakato wa kuujadili na kuuchambua Muswada huu jambo ambalo limesaidia sana kuufikiasha Muswada huu katika hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili utekelezaji wa sheria hii ufanyike kwa ufanisi na kukidhi madhumuni yake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anatakiwa kuwa na kasi inayowawezesha wahusika kutekeleza moja ya masharti ya sheria hii, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali iwezeshwe zaidi katika majukumu yaliyoelezwa katika sheria hii Kifungu cha 19(4). *(Makofi)*

Aidha, ni muhimu kwa Serikali kuzingatia kuwa Sheria hii pekee haitoshi kudhibiti matumizi ya fedha kama inavyokusudiwa. Pamoja na mambo mengine mfumo mzima wa uchaguzi na suala la maadili ya umma vinapaswa kufanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hayo ndiyo maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria za Gharama za Uchaguzi, natumaini kuwa yale ambayo Kamati haikuyagusia Waheshimiwa Wabunge mtaongezea pindi mtakapopata nafasi ya kuchangia na kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, naomba tena nikushukuru wewe binafasi kwa kunipa nafasi hii, aidha, nimshukuru Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, na watalaamu wa Serikali kwa ushirikiano na ufafanuzi wa kina walioutoa kwa Kamati. Ushirikiano huo ulisaidia Kamati kukamilisha hoja hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Katiba, Sheria na Utawala kwa michango yao ya kina iliyowezesha kuboresha Muswada huu, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo; Mheshimiwa George Lubeleje, Mweketiki wa Kamati, Mheshimiwa Ramadhani Maneno Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Stephan Galinoma, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Aboubakary Bakary, Mhehsimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Yussuf Makamba, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Salim Yussuf

Mohamed, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Makatibu wa Kamati hii Ndugu Athumani Hussein na Elihaika Mtui, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mawasilisho mazuri, sasa nitamwomba Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

Kwanza niipongeze Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuwa *very objective*, naamini Waziri atazingatia maoni yao lakini vilevile niseme kwamba hotuba yangu iliandaliwa wakati bado mabadiliko ambayo yameletwa leo asubuhi hatujayapata, kwa hiyo, kama kuna vitu ambavyo vitakuwa vimerekebishwa kwenye Muswada na kama vipo katika hotuba yangu naomba pia visizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi *(The Election Expenses Act 2009).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatambua umuhimu wa uwepo wa sheria ya kudhibiti matumizi ya fedha wakati wa kampeni. Hii inatokana na ukweli kwamba upinzani nchini umekuwa mhanga mkuu wa fedha chafu na safi (zisizo na ukomo) ambazo zimekuwa zikitumika wakati wa uchaguzi na ni Kambi ya Upinzani ambayo kwa miaka nenda rudi imekuwa ikidai uwepo wa sheria ya kudhubiti matumizi ya fedha katika kipindi cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tulishuhudia jinsi ambavyo fedha za *EPA (BOT)* zaidi ya shilingi bilioni 40 zilizochukuliwa na kampuni hewa ya *Kagoda* na fedha nyingine nyingi za wafanyabiashara mbalimbali, walio na wasio halali ndani na nje ya nchi zilivyofanikisha kwa kiasi kikubwa kukipa ushindi Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wa Urais, Ubunge na Udiwani. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(a).

**NAIBU SPIKA:** Naomba uisome.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, inasema kwamba bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge, Kifungu (a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani sasa hivi ametoa taarifa hapa ambayo mimi imenistua, anaposema kwamba sisi sote tulishuhudia jinsi fedha za *EPA* na pesa zingine ambazo ziliipatia ushindi Chama cha Mapinduzi katika nafasi ya Urais, Ubunge na Udiwani, haya maneno kayatoa wapi na naomba aweze kulithibitishia Bunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nia yetu ni kutunga Muswada utakaoweza kudhibiti tabia chafu, sasa hayo mengine umetoka kwenye pointi za maana ukaingia kwenye vitu ambavyo hatuna ushahidi navyo. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kufuta kwa sababu kiutaratibu wa Bunge kama mtu unatoa kauli unawajibu wa kuithibitisha kama ni kweli au siyo, sasa Mheshimiwa Chegeni, hawezi kunilazimisha nifute kauli kwa sababu tunazungumzia suala la Gharama za Uchaguzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Usizungumze na Chegeni zungumza na mimi.

**MHE. HALIMA J. MDEE-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI SERA, URATIBU NA BUNGE:** Sawa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Tuzungumze mambo ambayo tutafanya Muswada huu uwe na maana na mantiki kwa Watanzania wote, kwa hiyo, mkiingiza chumvi, mkaingiza na mafuta kwa lengo la kisiasa mnawapeleka wananchi kutokuelewa mantiki ya Muswada huu, sasa mimi ningependa sehemu hiyo uiache ili kusudi utoe mantiki ya Muswada, watu wote wasikilize, huu Muswada siyo wa Chama cha Upinzani wala siyo wa CCM ni wa Bunge la Tanzania, naomba tuwe *objective* katika vitu vikubwa kama hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa naomba maoni kwa sababu tunawaambia Watanzania!

**MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maoni ya Kambi ya Upinzani na nitathibitisha nikitakiwa kufanya hivyo, naomba niendelee na hotuba yangu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na maneno haya hayapo.

**MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ubishi kwamba tutakapokuwa na sheria nzuri ya kudhibiti matumizi ya fedha chafu katika chaguzi zetu, itawezesha kila mwanachama ndani ya Chama cha Siasa kuwa na fursa sawa za kugombea.

Halikadhalika itafanikisha kwa kiasi kikubwa kwa watu kutokuchaguliwa kwa kigezo cha fedha walizoweza kukusanya, bali kwa uwezo wao wa kufanya kazi na uadilifu kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi katika Muswada wenyewe, tunaambiwa kwamba, madhumuni ya na malengo ya sheria hii ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia na kuratibu mapato na matumizi ya gharama za kampeni kwa vyama vya siasa na wagombea. Halikadhalika kuweka utaratibu utakaowezesha Serikali kuchangia Vyama vya Siasa na vile vile kuweka utaratibu wa kisheria utaakaowezesha Serikali kuchangia gharama za Kampeni na uchaguzi na uchaguzi kwa vyama vya siasa na vilevile kuweka utaratibu wa kisheria wa kuratibu zawadi, misaada na michango itakayotolewa na wagombea wakati wa kampeni za uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni husika pia yanabainisha kwamba sheria inalenga katika kuweka utaratibu wa kudhibiti matumizi ya fedha wakati wa kampeni za uchaguzi. Hali kadhalika uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma na vilevile kuainisha adhabu kwa watakaokiuka masharti yaliyomo katika sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa vilevile kwamba sheria hii ina madhumuni ya kuweka mazingira yatakayowezesha kuwepo kwa uwazi zaidi katika matumizi ya fedha zitakazotengwa kwa ajili ya kampeni za uchaguzi na kwamba sheria husika ina malengo ya kusaidia kudhibiti matumizi mabaya ya fedha na vitendo vya rushwa kwenye gharama za kampeni za uchaguzi kwa kuwepo kwa uratibibu wa fedha zitakazotumika katika kampeni za uchaguzi ndani ya vyama vya siasa na katika uteuzi wa wagombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sasa tuangalie kama muktadha mzima ulioelezwa kwenye malengo ya Muswada, ndicho hasa kilichokuwemo ndani ya Muswada ambao Bunge lako Tukufu likiuridhia na Rais kuuridhia, itatumika katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika miezi nane kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muktadha wa Muswada wa kuzuia fedha chafu; licha ya kwamba tunaambiwa madhumuni ya Muswada ni kuzuia fedha chafu/haramu na fedha za nje, hakuna kipengele chochote ndani ya Muswada kinachoharamisha masuala yafuatayo:-

Kwanza, matumizi ya fedha za dhani zilizopatikana kiharamia, wizi wa fedha za umma, pili, fedha chafu zinazotokana na dawa za kulevya na tatu, fedha zinazotokana na makampuni ya kigeni au mashirika ya Kimataifa yaliyo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu pekee kinachozuia matumizi ya fedha katika Muswada huu ni Kifungu namba 12(1), (2) na (3). Vifungu husika vinavizuia vyama vya siasa, mashirika ya kijamii, taasisi, mashirika yasiyo ya Kiserikali, taasisi za kidini na kadhalika kutokuingiza fedha nchini, kwa malengo ya kutumia wakati wa uteuzi (ndani ya vyama) na wakati wa kampeni za uchaguzi. Tafsiri ya fedha kwa mujibu wa vipengele husika imejumuisha fedha, magari, ndege, bendera, usafiri, *t-shirt*, bendera, machapisho mbalimbali, matangazo ya kwenye redio na *television*, chakula na vinywaji kwa wapigakura au kitu kingine chochote kinachotarajiwa kutumika katika kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kwamba Muswada husika umewanyima fursa Watanzania wanachama wa Vyama vya Siasa kutokuchangia vyama vyao katika Uchaguzi Mkuu, na licha ya kwamba Muswada huu una malengo ya kuzuia fedha za nje ili kuzuia ushawishi wa wageni katika uchaguzi wa nchi yetu kama ambavyo Serikali inavyotuaminisha Watanzania, Muswada huu unazitambua na kuzihalalisha fedha za nje, chafu au safi ambazo zitaaingizwa ndani ya nchi siku 90 kabla ya Uchaguzi Mkuu au siku 30 kabla ya uchaguzi mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi la kujihoji, kama kweli dhamira ni kuzuia fedha kutoka nje ili kuepuka ushawishi wa mataifa ya nje ama wachangiaji mmoja mmoja kutoka nje, iweje leo kuwe na mipaka ya muda utakaozihalalisha fedha? Uharamia ni uharamia, haijalishi kama umefanyika usiku au mchana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa pia, madhumuni ya Muswada ni kuweka utaratibu utakaowezesha Serikali kuchangia gharama za kampeni na uchaguzi kwa vyama vya siasa. Kinyume chake, kipengele 8(1) cha Muswada kinatamka wazi kwamba ni jukumu la vyama vya siasa kujigharamia uchaguzi. Hakuna kipengele hata kimoja kinachoonyesha kwamba Serikali hata kwa uchache kitachangia gharama za kampeni na uchaguzi kwa vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosemekana sasa ni kwamba eti Serikali ilikuwa na dhamira ya kuvisaidia vyama vya siasa kugharamia gharama za mawakala na kwamba baada ya vituo vya kupiga kura kuongezeka kutoka 35,000 mpaka 50,000 imegundua kwamba zitahitajika shilingi bilioni 20, kwa gharama ya 20,000/= kwa kila wakala wa chama cha siasa ambazo ni nyingi sana! Hii inatokana na tamko ambalo Waziri mwenye dhamana alilitoa wakati wa semina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa akili ya kawaida shilingi bilioni 20 si fedha nyingi hasa inapohusu zoezi muhimu kama la Uchaguzi Mkuu ambalo linaamua mustakabali wa nchi yetu. Kama tunaweza kutumia zaidi ya shilingi bilioni 300 kwa safari za ndani na nje ya nchi ndani ya miaka miwili, au shilingi bilioni 33 kwa viburudisho maofisini ndani ya mwaka mmoja tu wa Bajeti, iweje leo ishindikane kupatikana shilingi bilioni 20 kwa zoezi linalofanyika mara moja katika kipindi cha miaka mitano? Ingewezekana kabisa Serikali kupunguza gharama kwa kuwalipa mawakala 10,000/= kila mmoja ambayo ingepunguza nusu ya gharama ya awali na kufikia shilingi bilioni 10 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoonekana hapa, ni dhamira ya makusudi ya Serikali, kwa kujua umasikini/ukata wa vyama vya siasa nchini, ukitoa Chama Tawala kinachopata ruzuku ya zaidi ya shilingi bilioni moja kwa mwezi, kuhakikishe kwamba kunakuwa hakuna mawakala wa vyama katika vituo vya uchaguzi, kama ambavyo imekuwa ikijitokeza kwa miaka nenda rudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una mkanganyiko wa vifungu mbalimbali ambavyo visipotolewa ufafanuzi vyaweza kuleta utata baadae wakati wa tafsiri ya sheria. Vifungu hivyo ni; 8(4), 11(2), 11(4) na 15 (1). Kifungu cha 8(1) cha Muswada huu kinatamka bayana kwamba ni wajibu, jukumu la chama cha siasa kugharamia uchaguzi kwa kutumia

rasilimali zake na Kifungu cha 8(4) kinamruhusu mgombea kupokea au kukubali msaada kwa ajili ya kugharamia uchaguzi kutoka kwa mtu au taasisi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15(1) kinatamka kwamba fedha zote zinazotolewa na taasisi au kikundi cha watu au na mtu yeyote kwa ajili ya mchakato wa uteuzi au gharama za uchaguzi wa chama cha siasa kama zawadi, mkopo au msaada lazima upelekwe au uhaidiwe kupelekwa kwenye chama cha siasa kinachohusika na si vinginevyo, na chama cha siasa kinatakiwa kutoa taarifa za michango husika wakati ikitoa taarifa. Kifungu cha 11(2) kinatamka kwamba kila chama cha siasa kinatakiwa kuhakikisha kwamba michango yote chama inayokipata inawekwa kwenye akaunti maalum iliyofinguliwa na chama kwa madhumuni ya kugharamia uchaguzi na gharama zote zinatakiwa zilipwe kutoka katika hiyo akaunti husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kipengele cha 15(1) kinatamka kwamba fedha zote na michango yote kwa malengo ya gharama za uchaguzi zinatakiwa kupelekwa kwenye vyama na kwa kuwa msingi wa Sheria unasema kwamba ni jukumu la chama cha siasa kusimamia na kugharamia uchaguzi wake, kisheria haijulikani nafasi ya fedha anazozipata mgombea zinaingizwa katika fungu gani katika zoezi zima la gharama za uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 10 cha Muswada husika kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana kupanga kiasi cha fedha kitakachotumika katika gharama za uchaguzi kwa kuzingatia ukubwa wa majimbo, aina ya wagombea, idadi ya watu na miundombinu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona ingekuwa jambo la busara kwa maamuzi hayo kufikiwa baada ya kushauriana na kuafikiana baina ya Vyama vya Siasa na Msajili. Waziri mwenye dhamana asije akatumia rungu lake la kupokea ushauri tu toka katika vyama husika na kisha kuamua kwa matakwa yake, kama ilivyojidhihirisha katika kikao cha Morogoro ambacho licha ya wadau kutoa maoni mbalimbali juu ya utaratibu wa kuendesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ushauri wao uliwekwa kapuni na uchaguzi kuendeshwa pasipo kuzingatia maoni husika. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza manung’uniko kutoka kwa wadau hao muhimu katika siasa za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine chenye utata, ni kifungu cha 24(2) kinachompa mamlaka msajili wa vyama vya siasa kumkosesha sifa za kugombea *(disqualify)* mgombea kwa kigezo kwamba ametenda matendo yanayokatazwa na sheria *(prohibited practice).*

Mheshimiwa Naibu Spika, si sahihi kwa msajili wa vyama vya siasa kufanya kazi ambayo ni ya Tume ya Uchaguzi kisheria. Vifungu 40(3) na 44(3) vya Sheria ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali ya Mtaa vinaipa mamlaka Tume ya Uchaguzi kumzuia mgombea kugombea, baada ya pingamizi kuwekwa na mgombea mwenzake na Tume kujiridhisha kwamba mgombea husika amekiuka sheria na taratibu za uchaguzi, hivyo kukosa sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kwamba kumpa mamlaka haya ni kuingilia kazi za Tume ya Uchaguzi, Kambi ya Upinzani inahoji uwezo wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kirasilimali watu na kinyenzo inaweza kuhimili pilikapilika za uchaguzi wa Rais, Ubunge na Udiwani na idadi ya malalamiko yanayotarajiwa kuwepo kuwepo kwa sheria hii. Kambi ya Upinzani inashauri suala la kuamua kama mgombea ana sifa ama laa libaki kwa Tume ya Uchaguzi na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 22 kinazuia mtu au wakala wake kabla, wakati au baada ya mchakato wa uteuzi kutoa fedha, chakula, kinywaji, kiburudisho au kitu chochote kinachofanana akiwa na malengo ya kumshawishi mtu huyo kumpigia kura au kutokupiga kura wakati wa uteuzi. Kipengele husika pia kinatamka bayana kwamba ni kosa kwa mtu yeyote kukubali kupokea chakula, fedha au kiburudisho ili asipige kura au kwa malengo ya kumpigia kura mtu fulani. Kifungu hiki ni zalio la maamuzi ya Mahakama Kuu ambayo iliharamisha takrima! *(Makofi)*

Kipengele husika kilizua mjadala mzito sana, hali iliyopelekea kuongezwa kwa kifungu ambacho kitatambua timu ya mgombea ambayo itajumuisha vikundi vya ngoma, kama kundi ambalo linaruhusiwa kisheria kugharamiwa na mgombea husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa tahadhari kwamba kuruhusiwa huku kwa vikundi vya ngoma, isije ikawa tiketi ya kuirudisha takrima kwa mlango wa nyuma kwa wagombea kuwa na vikundi vya ngoma kila kijiji, mtaa na kitongoji kisingizio kikiwa utamaduni wa Kiafrika wa kukirimiana kwa kutoa chakula, pombe na pesa kwa malengo ya kupigiwa kura au kuzuia watu wasipige kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria hii, ikiwemo TAKUKURU kutekeleza wajibu wake kwa umakini, ili kuondoa fikra ambazo zimetawala kwenye vichwa vya watu kwamba vyombo husika vinafanya kazi kwa matakwa ya Serikali iliyopo madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kipengele cha 28 kinazungumzia amani na utulivu ambao ni jambo muhimu sana wakati wa Uchaguzi Mkuu. Kwa mujibu wa kifungu husika, itakuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na ulinzi na usalama wakati wa kipindi cha uteuzi, kwenye vyama vya siasa halikadhalika wakati wa kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, toleo la kwanza la Muswada liliweka zuio kwa vyama vya siasa au mgombea kutumia walinzi binafsi wakati wa kipindi cha uteuzi au wakati wa kampeni. Cha kushangaza toleo la mwisho la Muswada limekitoa kifungu husika. Kambi ya Upinzani inahoji juu ya utoaji wa kifungu tajwa licha ya kwamba yaweza kuonekana vikundi hivi haviruhusiwi kushiriki katika uteuzi na katika shughuli za kampeni kutokana na sheria kutoa mamlaka kwa Jeshi la Polisi kulinda amani, kutolewa kwa kifungu hicho chaweza pia kuashiria kwamba sheria hii kwa upande wa nyuma inatambua matumizi ya vikosi vya ulinzi vya vyama vya siasa maarufu kama *Green guard* (CCM), *Blue guard*(*CUF*) na *Red brigade* (CHADEMA). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo sivyo iweje kifungu husika kinachokataza matumizi ya vikundi hivyo kimetolewa wakati kilikuwa hakina madhara yoyote kilivyokuwepo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mawazo yenu, tunao wachangiaji wengi na hii Miswada ni miwili, kwa hiyo, inabidi yote iishe leo kwa sababu kesho tutakuwa na Muswada mmoja na ni siku ya kufunga Mkutano. Mchangiaji wangu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Fred Mpendazoe na tunaweza kumfikia Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula nadhani tutamfikia pia.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia Muswada huu muhimu na labda niseme kuanzia mwanzo kwamba sisi hasa katika Kambi ya Upinzani tumepiga kelele siku zote kutaka fedha zinazotumika katika uchaguzi zijulikane ni kiasi gani na zimefanya kazi gani na kupiga vita fedha zote haramu zisiingie kwenye uchaguzi kwa sababu ndizo kadi za wapiga kura kununuliwa, wapiga kura kupewa fedha na kununuliwa, chumvi, sabuni na kadhalika, kugawiwa kwa wapiga kura, kwa hiyo, kimsingi hakuna ambaye atakataa Muswada unaotaka kupinga hayo labda na yeye mwenyewe awe katika sura ya kutaka kutoa vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo kama lengo ni la Muswada uliowasilishwa una nia ya kudhibiti vyama vingine zaidi ya chama chenye nguvu kinachotawala basi tutaupinga Muswada huu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuupingi kwa madhumuni ya kuzuia fedha haramu wala fedha zinazotokana na ufisadi, tunapinga Muswada unaofanya kudumaza demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba nianze kuingia moja kwa moja kwenye maeneo mbalimbali.

Kifungu cha 4 kinazungumzia mamlaka makubwa ya Msajili wa Vyama. Kwa bahati mbaya pamoja na maoni yote yaliyotolewa na wadau ambayo bahati mbaya Serikali haikuyazingatia sana pamoja na marekebisho madogo madogo yaliyofanyika, Msajili wa Vyama kwa mujibu wa sheria namba 5 ndiyo mlezi wa vyama, ndiyo mwandikishaji na Msajili wa Vyama, ndiye anayevishauri vyama. Unapomgeuza kuwa polisi na wakati huo huo kuwa hakimu anayeweza kuweka pingamizi kwa mgombea katikati ya uchaguzi na wakati huo huo atamtoa yule mgombea hata kama ni kwa kushauriana na Katibu Mkuu na Chama chake baadaye, lakini mamlaka hayo anayo yeye, akapewa mamlaka ya kuingia mpaka kwenye mafaili ya vyama kwenda kupekua umeondoa yale mamlaka yanayotolewa au yale mahusiano yaliyojengwa na sheria namba 5 inakwenda kinyume kabisa na *best practices* za kurundika mamlaka mikononi mwa mtu mmoja.

Msajili katika sheria hii mahali popote hakupewa chombo chochote cha kushauriana naye katika majukumu anayoyafanya, ni Msajili na ana mamlaka yote, ni kitu ambacho duniani

hakijatokea. Tume ya Uchaguzi katika taratibu na sheria zilizopo imefanyakazi nzuri kwa sababu Tume ikifika mahali kuna *objection* inapelekwa au kuna pingamizi inawekwa Tume inajiita, inakaa kama Tume inajadili, inasikiliza pingamizi. Msajili hakupewa kifungu chochote.

Mimi katika hili naomba niseme toka mwanzo, pamoja na marekebisho ninaukataa tena Muswada huu kwa sababu unakwenda kinyume cha *best practices* na nia njema tuliyotaka ya kudhibiti haitapatikana kwa njia ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tena kwa haraka kwa sababu muda utakuwa mdogo katika kifungu cha 10, *a political party or a candidate expense funds* sasa sheria inajichanganya. Huku nyuma wanasema kwamba fedha zote zitatumika na vyama vya siasa lakini kifungu cha 10(2) kinaweka *where in exceptional circumstances a political party or a candidate*, kwa hiyo kumbe na *candidate* ameruhusiwa, lakini huko kwingine imemnyima. Naomba Waziri aangalie huu mkanganyiko kwa sababu ukisema kwenye kifungu kingine kule nyuma kwamba ni *political party* peke yake *then* kuna tatizo ambalo huko mbele kutakuwa na migongano ambayo siyo ya lazima. Sheria inayotungwa na ni lazima iepuke migongano ni lazima iepuke watu kupelekana mahakamani, ni lazima ihakikishe kwamba uchaguzi hata kama *process* itaenda sawa, baadaye tusiende kukutana tena mahakamani.

Niseme tena kwa kifupi kuhusu *restriction of foreign funding to election*. Kwa bahati mbaya sheria inatoa matatizo ambayo ni kweli labda yangeweza kutokea. Nilitegemea kwamba *restrictions* zinazowekwa katika Kifungu cha 12 *restriction* hizi zingetaka taratibu zenye kuleta uwazi, zenye kuleta udhibiti, zenye kufanya usimamizi uwe makini, lakini si kuzuia. Vyama vingine ni dhihiri sisi tunachapa bendera zetu China, kama katikati ya uchaguzi mahitaji ya bendera yamekuwa mengi tunazuiwa kuleta kwa njia halali kwa fedha zetu za Chama, hii ni kinyume na taratibu za demokrasia. Mtanzania yuko huru kwa fedha zake kama amezipata na amezitangaza aruhusiwe hata ni dakika ya mwisho kuagiza kitu chochote kutoka popote, akilete nchini kwa sababu hapo unathibitisha kwamba siyo fedha haramu kwa sababu uwezo unao na sheria unayo hakuna sababu ya siku 90.

Vyama vyetu vidogo na kwa hili naomba niseme hata kwa Wabunge wa CCM wasifikiri watapona, ukichangiwa hata na wale wapenzi wako kuna mahali unaambiwa ukichangiwa lazima uwe ume-*declare* wakati wa *nomination*. Sasa wakati wa *nomination* uko katikati ya uchaguzi rafiki amejitokeza na rafiki wewe humpangii, anayekupangia anayekupenda anakupenda mimi nataka leo nikuwekee mafuta huwezi kumwambia siku zaidi ya 90 kabla unipe hii taarifa kama wewe utanichangia halafu baadaye mimi nisiweze kuulizwa.

Mimi nafikiri hapa tunakwenda kinyume kabisa. Tutengeneze taratibu zinazotaka ukichangiwa na rafiki yako wakati wowote taarifa ipelekwe kwa yule yeyote atakayepelekwa japo mimi sitaki ziende kwa msajili. Taarifa ziende kwa chombo kile kinachotakiwa kufanya tathimini kwa sababu hutajua ni lini rafiki yako atatokea, ni lini utahitaji mafuta na umeambiwa kabisa ukitumia zaidi ya fedha ulizotangaza ni kosa la jinai. Lakini zaidi ya pale tukisema kwamba fedha ziweze kuchangwa au michango ipokelewe na chama peke yake tuna utamaduni Tanzania mimi Katibu Mkuu wa CHADEMA na naomba nieleze hapa uzoefu. Watanzania wengi hata sasa wanaogopa kuchanga fedha kwa Vyama vya Upinzani kwa sababu kuna dhana ambayo inatumika kwamba watashughulikiwa. Hili limetokea. Sisi tuna *experience* na mkihitaji

tutatoa ushahidi kamili kwamba watu ni waoga, Watanzania utamaduni wetu hatujafika mahali tukaamini kwamba tunaweza kuchangia vyama vingine isipokuwa CCM. CCM ina uwezo wa kuwaita wafanyabiashara ikatumia rungu lake la ukubwa, rungu lake la ukubwa, rungu lake la kuwa Chama Tawala ikaweza kupata michango wakati wowote. Lakini vyama vingine haviwezi kuita watu haraka. Sasa hapo tunachoua ni demokrasia hatujengi demokrasia, unalenga kujenga demokrasia sahihi. Kama unajenga demokrasia tutoe nafasi. Hii kama nilivyosema siyo kwa watu wa Upinzani tu hata kwa Mbunge kama kuna sababu yoyote wamechukiana na katibu Mkuu ukaenda kuchangia na rafiki yako umezidi ya ile uliyotangaza utachukuliwa hatua ni *(criminal offense)* ni kosa la jinai. Nadhani hapa hatujengi demokrasia ambayo tungeipenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema fedha ziende kwa *nomination* kifungu cha 14 ndiyo nilichosema kinapinga kwa sababu si kinasema; *"All expenses to be incurred during the nomination process within the political party shall be borne out by a political party concern."* Huko mbele tunasema Msajili atatengeneza *uniform regulation* sina tatizo na *regulation* ambazo atatengeneza, ninachoogopa tu hapa ni kwamba *regulation* kama tulivyoona kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa tusije tukatengenezewa *regulation* kwa sababu haziji Bungeni tukatengenezewa *regulation* ndiyo ambazo zinakuwa kali zaidi kuliko sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano ukichukua kanuni ambazo Morogoro tulikubaliana wadau zilisema kwamba "Mgombea yeyote wa Chama cha Siasa atadhaminiwa na kiongozi wa Chama" mwongozo uliotengenezwa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ilikuwa inasimamiwa ule uchaguzi TAMISEMI ikaenda mbele zaidi katika mwongozo ikasema maafisa wa ngazi ya chini kabisa ya Chama hicho ni kinyume kabisa na Katiba yetu ya CHADEMA. Kwa matokeo haya tukaondolewa kabisa Wilaya 30 hata kabla hatujaanza uchaguzi. Hii ni hatari katika demokrasia. Kama tunaanza kudhibitiana kwa sheria basi nadhani kwa kweli ni lazima tufike mahali kwamba sasa tuko pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake kuna mgogoro mkubwa Wilaya 30 tuliondolewa na Katibu Mkuu wa CCM akatokea hadharani kwamba tuna viti 24,000 tumevishinda bila upinzani yaani bila kupingwa. Lakini mmetuondoa kwa kutumia kipengele cha mwongozo ambao wala siyo kanuni, hatukuulizwa, hatukushauriwa Katiba zetu zimekiukwa na Serikali, Serikali inayopaswa kutusaidia ili Katiba za Vyama ziende sambamba zimewekwe pembeni kwa njia ya kitu kinachoitwa mwongozo. Ni hali ya hatari kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda unakimbia na nimalize, kipengele cha Waziri ambaye ndiye anayesimamia anakwenda kutuwekea ni kiwango gani cha fedha, hebu fikiria Waziri huyo naye anakwenda kugombea uchaguzi, hebu fikiria Waziri huyo naye katika jimbo lake ana mpinzani, ndiyo anakwenda kuwekea kipingamizi cha  fedha atakazotumia. Akitumia vibaya tunafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatunga sheria ambazo haziendi katika taratibu za dunia za *transparency*. Taratibu za kawaida zinataka yule ambaye ni *interested party* awekwe pembeni na yeye asishughulike katika kuamua. Ikiwa anakuchukia, anakuambia wewe hela bwana ni hii na huna *appeal*, hakuna rufaa yoyote unayokata popote ni sheria ya ajabu kwamba unaweka mamlaka katika chombo lakini hutoi nafasi yoyote ya kukata rufaa popote akikuamulia ndiyo

mwisho, hatma yako inaamuliwa na mtu mmoja, labda kwa sababu anakuchukia una macho makubwa. Mimi naona hii ni sheria ya ajabu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi siungi mkono hoja hii, naomba Serikali iyaangalie haya mambo kama kweli inapenda kuleta demokrasia na kama kweli nia ni ile na kama Kambi ya Upinzani tumeeleza wazi kwamba kama tulikuwa na nia ya kudhibiti ni kwa nini basi fedha haramu hazikuandikwa kwenye kifungu chochote kwamba fedha hizi ni haramu, kifungu fulani kikatae hakuna popote. Kwa nini fedha zinazotokana na dawa za kulevya hakuna kifungu chochote. Hii ni dhahiri kabisa kwamba Muswada haukulenga hicho tu. Tumezungumza pale mfano wa *EPA* na mimi nairudia tena kwamba ni kweli kwamba kama tunavyosema fedha haramu tumelilia kila siku ni pamoja na fedha zetu haramu zilivyotumika kwenye *EPA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu akisema kwamba si kweli sisi tuko tayari tunaweza kwenda kudhibitisha. Tunapinga katika Muswada huu kwamba isitokee fedha zikaenda kuchukuliwa mahali bila kufuata utaratibu zikatumika kwa kunufaisha chama fulani. Ndicho tunachosema naumba nisiunge mkono hoja, naomba maelezo ya kina Serikali ikiwa tayari kurekebisha haya mimi Muswada huu nitauunga mkono kwa sababu naupenda.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa nchi yetu. Cha kwanza kabisa naomba niseme kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu nauunga mkono Muswada huu. Ni vyema tuanze hatua ya kwanza kama kuna marekebisho tutakavyokuwa tunautekeleza tunaweza kuona ni sehemu gani zinatakiwa kuimarishwa, kusahihishwa lakini kuna haja ya kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa yanayoikabili nchi yetu ni pamoja na hili tatizo kubwa la rushwa na hasa rushwa wakati wa uchaguzi. Naomba kuunga mkono kabisa maoni ya Kamati ukurasa wa sita ambayo imeeleza vizuri sana kwamba Muswada huu utakuwa ni moja ya hatua ya kuimarisha demokrasia katika nchi yetu. Tunafahamu ni kutokana na hilo ndio maana nasema niunge mkono hoja hii kwa sababu tunaanza hatua ya kuimarisha demokrasia yetu ambayo ilianza kuonekana kuzoroteshwa na matumizi makubwa ya fedha wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu sana, fedha nyingi zilitumika katika uchaguzi wa mwaka 2005. Kinachonipa faraja sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoapishwa hotuba yake ya kwanza Bungeni tarehe 30 Desemba, akizungumza na Bunge alizungumzia suala hili. Alikuwa ndipo amemaliza kuapishwa, alikuwa ameliona hili likitokea katika uchaguzi na alikuwa wa kwanza kulisema na kutoa tahadhari kwamba kuna haja ya kulishughulikia.

Leo tupo hapa tukiwawakilisha wananchi tuweze kuwa na sheria itakayoweza kutusaidia kuondoa tatizo hili ambalo linaikabili nchi yetu. Kwa hiyo, kwa hilo ndio maana naomba niunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Lakini ninayo maoni ambayo ningependa kuyasisitiza katika kuunga mkono Muswada huu kama ilivyoelezwa ukurasa wa 10 mpaka wa 12 katika maoni ya Kamati katika kudhibiti

matumizi ya fedha wakati wa uchaguzi, nimefarajika sana kuona kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa anaelekeza nguvu zake kuhakikisha kwamba vyama vya siasa ndivyo vinavyochukua hatua ya kudhibiti na ndio la msingi kabisa na mimi napenda nisisitize.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wengi tumeshasikia na huwa tunasema sehemu nyingi chama legelege huzaa Serikali legelege, chama kikiyumba, Serikali inayumba, chama kinachokula rushwa hakiweza kuzaa Serikali isiyokula rushwa. Kwa hiyo, kudhibiti rushwa wakati wa uchaguzi msisitizo mkubwa kama ilivyoonyeshwa katika maoni ya Kamati, nakubaliana na naomba kusisitiza uanzie kwenye vyama vya siasa. Kwa sababu vyama vya siasa au chama kinachoshinda ndicho kinachounda Serikali. Kama chenyewe kitashindwa kudhibiti rushwa katika chama chake Serikali yake itadhibiti vipi rushwa hata kama kutakuwa na sheria nzuri namna gani? *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuanzie kama tuko kwa dhati tunataka kuondoa rushwa tuanzie katika vyama vyetu vya siasa. Sheria hii iweke kanuni na iwe kali zaidi chama kinachoonekana kimeshindwa kudhibiti rushwa wakati wa kura za maoni na wakati wowote ule kisiruhusiwe kuendelea na uchaguzi. Hakuna maana ya chama kile kuunda Serikali kama chenyewe huku kimeshindwa, na tatizo hili tumeliona la rushwa kwenye uchaguzi kwa sababu tunapata viongozi ambao hawakuchaguliwa na watu ni wale walionunua uongozi, wametoa fedha wakapata uongozi, hawakushawishi wananchi kwa sifa zao wametumia fedha zao.

Sasa kwa nini sheria hii isiwe na mkazo zaidi na kuweka kanuni ya kukikataa chama, na chama kisiendelee kuwa chama cha siasa iwe ni moja ya masharti ya kwamba chama kinachoshindwa kudhibiti rushwa katika chama chake, wanachama wake, hata kufutwa kwenye chama cha siasa kifutwe. Kwa sababu rushwa inaozesha Taifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naunga mkono kama walivyosema katika ukurasa wa 10 mpaka 12 kama kwa dhati tunataka kuondoa rushwa tuanzie kwenye vyama vya siasa. Kanuni sasa iwekwe ya kusema chama hiki kimeshindwa na Msajili kweli apewe nguvu ya kukiondoa na kukifuta. Tukubaliane hivyo Watanzania katika sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja nisema hii kufafanua. Mbunge ameshinda kwenye chama kile kwa kutoa rushwa, anateuliwa kuwa Waziri, akiteua bodi yoyote katika Wizara hiyo, ataweka wale ambao atakula nao rushwa. Katika taasisi za umma wataendelea kukusanyana ili waendelee kula rushwa. Ndiyo maana nasema chama kianzie huko, kiwadhibiti na kuwaondoa na chama kikionekana hakifanyi hivyo hakifai kuwa chama cha siasa kitakachotusaidia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini vile vile kuangalia mifumo yetu. Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Uchaguzi na TAKUKURU ili viweze kusaidiana kuondoa rushwa wakati wa mchakato wote vinatakiwa viwe huru kweli kweli, kama haviko huru sheria hii haitafanyakazi. Namna gani tuviweke huru tujifunze katika nchi ambazo zimefanya hivyo na zipo. Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Uchaguzi iwe huru na iwe huru kweli kweli na nguvu inazopewa kweli watatenda haki na usawa kwa vyama vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la rushwa limeingia katika jamii. Rushwa hutolewa na rushwa hupokelewa tena kwa siri. Kwa sasa wananchi wanaomba rushwa kwa hiari yao na kwa shauku kubwa. Kwa hiyo, watoaji wa rushwa wanapata nafasi rahisi sana kwa sababu yanakuwepo makubaliano. Kwa mazingira hayo huwezi ukapata ushahidi mahali ambapo watu wanataka wapewe rushwa kutokana na umaskini uliokithiri na mtoaji rushwa naye anataka anunue uongozi anapokea naye ana shauku ya kupokea rushwa, utapataje ushahidi pale? Ni tatizo kubwa tunatakiwa tuelimishe sana jamii na kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wakichukia rushwa, wote tukichukia rushwa, rushwa itaondoka. Lakini kama hatutaichukia rushwa hata tuwe na sheria nzuri namna gani kama inavyoonekana mwanzo wetu huu kuipitisha sheria hii hakuna kitu kitakachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba niwaase Watanzania tunapokwenda katika uchaguzi na tunapopitisha sheria hii, kuna sifa kuu mbili ambazo zinafaa kwa kiongozi. Tukizitumia hizo Watanzania tutasaidia sana kuondoa rushwa. Mtu anayetakiwa kuwa kiongozi awe na sifa hizi mbili, ya kwanza awe na uwezo wa kuongoza, mchapakazi kweli kweli, sifa hiyo ni ya kwanza ya mtu kuwa kiongozi.

Lakini sifa ya pili ambayo itatusaidia kuondoa rushwa, mtu yeyote anayetaka kuwa kiongozi Rais, Mbunge au Diwani anatakiwa awe na sifa ya pili ambayo ni muhimu awe hataki kuwa kiongozi. Kama mtu hutaki kuwa kiongozi utatumiaje fedha nyingi kununua uongozi? Utatumiaje fedha nyingi sana kuingia Ikulu ambapo kuna matatizo mengi na mazito? Utatumiaje fedha nyingi kupata Ubunge wakati Ubunge ni matatizo makubwa, utatakaje kuwa Diwani wakati Udiwani ni mzigo mkubwa kuwatumikia wananchi? Kama uongozi ni utumishi mahali popote katika historia yeye aliyeonekana kwenye jamii anafaa kuwa kiongozi cha kwanza alikuwa hataki kuwa kiongozi. Alishawishiwa sana kwamba kubali kuwa kiongozi hakutoka yeye ashawishi watu na hata kuwanunua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sifa hii ya pili kama Watanzania tutaizingatia wakati tunakwenda kuchagua viongozi wale wanaotaka sana uongozi na wananunua uongozi na wanatumia fedha nyingi kwa sasa hawafai kuwa viongozi na tusiwachague. Tuwatafute wale kabisa kwa dhati hawataki, kama mtu anataka kuwa Rais kwa gharama kubwa sana atumie utajiri wake anazunguka kule na kule kununua watu huyo hafai tujue hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge yeyote ambaye anataka kuwa Mbunge na anatumia fedha nyingi sana, utajiri wake awe Mbunge huyo hafai kuwa Mbunge. Hiyo ndiyo sifa kubwa ambayo itatusaidia sisi Watanzania kuwaacha wale watu na baadaye hawatatumia hizo fedha ambazo wanazo na wametajirika wakati mwingine kwa kuwadhulumu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipenda niseme hayo nikizidisha zaidi ninaweza nikawachosha. Nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja kwamba sijajiandaa vizuri baada ya kuipata ripoti hii nitazungumza japo kidogo. *(Makofi)*

Kwanza niseme kwamba Muswada huu ulichelewa kwa sababu ulikuwa uanze pale ambapo vyama vingi vilipoanzishwa, ndio umetufikisha hapa. Lakini kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia sasa hivi ni vyema tukaanza pamoja na Mheshimiwa Dr. Slaa atakuwa na wasiwasi lakini ni vyema tuanze baadaye tutafanya haya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mzuri, uzuri wake ni jinsi ya kuweza kubana matumizi mabaya ya fedha za wananchi. Japokuwa mtu ataona kwamba ni fedha hizo amezipata kwa njia ambazo si halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu kwamba eneo moja ambalo halijaguswa sana ile *nomination process*, kipindi ambacho sasa hivi tunaelekea cha wagombea kutafuta nafasi ya kuwa *nominated*, hapa ndipo fedha zinapotumika pia haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba sana kama haijatokea humu basi kuwe na kanuni zinazowabana hasa watu kwamba ni kipindi gani mtu anatakiwa aanze kufanya ile *process* ya *nomination* badala ya kutumia fedha nyingi ambazo kwa kweli matokeo yake ni haya watu kuwa na ugomvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tayari kuna watu wameshaanza kujitokeza na tulipo hapa sasa watu wako kule. Lakini kuna wengine wameanza kujitokeza miaka miwili iliyopita kwa kurubuni watu kwa kutumia fedha za umma na wengine ni wafanyakazi wa Serikali lakini wako *interested* kuwa Wabunge, Madiwani na kadhalika. Sasa kwa kweli kanuni kama haitakuwepo ya kuwadhibiti lakini pia muda wa *nomination* uanze lini, iwepo kanuni au iwekwe kwenye sheria kwamba *nomination process* inaanza mwezi fulani kwa vyama vyote tuwe *even* siyo chama hiki kina wakati wake na chama hiki kina wakati wake na chama hiki kina wakati, lazima utengwe muda maalum kabisa labda mwezi wa saba kuwe na wateuzi ambao watakuwa ni *candidate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiingia kwenye Muswada ukianzia na kifungu cha 2(b) ambacho kinahusu *candidates* hawa upande wa Zanzibar kwa kweli kimeelezea ni Wabunge pamoja na wale ofisi ya Makamu wa Rais. Naomba sana katika marekebisho ya baadaye sehemu hii i-*cover* hata kwa wenzetu wa wawakilishi kwa sababu wote tumesajiliwa na mwanajili mmoja wote tuko kwenye chama kimoja. Sasa kama lengo ni kuzuia hii rushwa au matumizi mabaya ya fedha za umma ukiwa tutaacha upande mmoja huoni kwamba hii sheria inatumika sivyo. Kwanza Zanzibar hatuna TAKUKURU sasa kudhibiti utadhibiti vipi? Ni tatizo hilo.

Kwa hiyo, ndiyo tuone upande wa Zanzibar wenzetu utakuwa na hali ngumu hii itakavyokuwa kwa sababu wenzetu wana *room* ya kuweza kupitisha fedha zao lakini sisi hatuna *room*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na hiyo iangaliwe baadaye na wenzetu tuwaone kule tuangalie jinsi gani kuna nia njema tu bila shaka, hakuna nchi inayopenda rushwa kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kifungu namba 9(1) *disclosure of fund,* katika kifungu hiki mgombea anatakiwa aelezee ni kiasi gani cha fedha atatumia. Nataka kujua kwamba ku-

*disclose fund* ambayo utakayotumia wakati wa *nomination process* kila mtu ambaye anataka kugombea a-*disclose* hizo *amount* atakazotumia au tayari wewe umeshateuliwa, nilitaka tu nifahamu kwamba labda katika *process* ya *nomination* watu wote wale wanaotaka kugombea labda wanatakiwa waelezee ni kiasi gani wanatumia au tayari mtu ameshajulikana kwamba yeye ni *candidate* ndiyo anatakiwa a-*disclose* hiyo *amount.* Nilitaka ufafanuzi kidogo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niangalie kifungu cha 10(2). Hapa ningependekeza kwamba huyu mgombea asiwajibike kabisa katika kutoa taarifa kwa *register* kwa sababu kuna chama chake ambacho ni *responsible* vinginevyo kutakuwa na matatizo wakati mwingine *candidate* ameshapata fedha, ameshatumia zaidi lakini sasa amekaa kinywa. Lakini ikaja ikagunduliwa kwamba huyo *candidate* alitumia fedha ambazo ni *excess*. Sasa tatizo hapa ni kwamba anaweza akaenguliwa lakini chama chake kama kitakuwa *responsible* kitambana zaidi ili aweze kukielezea chama chake vizuri kwamba kuna kiasi fulani ambacho tumekipata kama *excess*.

Kwa hiyo, ningeomba chama ndiyo kihusike badala ya *candidate*. Ukimuhusisha *candidate* hapo kutakuwa na *contradiction*. Lakini ukiangalia kifungu cha tatu, kama *candidate* atatumia hela ambayo ni *excess* au chama ina maana tayari imeingia kwenye makosa, sasa kuna haja gani kwenye kifungu cha pili hapo kuwepo? Kwa sababu hapo tayari hilo ni kosa halafu unataka ripoti ya nini na umesha-*commit* kosa. Basi ningeangalia uhusiano hapa wa Kifungu cha pili na cha tatu kwa sababu tayari umeshahukumiwa hata unapeleka ripoti wewe tayari una kosa, *what is next*?

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo umesha *commit* ni kosa na ripoti umepeleka sasa utafanyaje? Hakijaelezwa kitatokea nini. Ningependekeza *either* kifungu cha pili kikatwe kibakie cha tatu. Kifungu cha 18(1), hapa pia inaelezea kuhusu namna gani *candidate* anaweza kupata pesa na kutoa *information/report* kama nilivyosema mwanzo nilitaka kujua tu kwamba ingekuwa kwenye sheria iingizwe kwamba *nomination* inaanza kipindi fulani, yaani ieleze kwenye sheria kwamba miezi fulani iwe ni miezi ya *nomination* na Uchaguzi Mkuu utakuwa mwezi fulani, yaani iingie kwenye sheria kama itawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama kifungu cha 18(5) hapo kuna *penalty* ambayo inatolewa kwa mgombea anayeshindwa kutoa taarifa ya matumizi ya pesa za ziada, ambayo nilisema *candidate* aondoshwe na badala yake iwe chama husika, hapa inaonyesha kwamba vyama hasa vichanga vitakuwa vinashindwa ku-*compete* kwa sababu wanajua kabisa kwamba atagombea lakini chama kitashindwa, sasa akishashindwa pale ripoti yake mwingine atashindwa kuipeleka, lakini hapa sheria inamwambia ni lazima apeleke ripoti.

Sasa kwa kweli inakuwa kama ni uonevu, yaani vyama vichanga vitashindwa kuweka wagombea wengi zaidi kwa lengo kwamba na wao waonekane kwamba wame-*contest* kwa hofu hiyo hapo kwamba keshashindwa, anashindwa kupeleka taarifa, kwa sababu kupeleka taarifa inaweza ikawa ni gharama kwa hiyo matokeo yatafutwa kwa *candidate* yule na ndiyo maana nikasema *candidate* asihusike, tukiachie *political party* kuliko hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha sita kinasema hicho chama chenyewe kimepewa *extension* ya muda, lakini huyo *candidate* hajapewa muda kwamba ameshindwa kupeleka apewe

muda zaidi ili aweze na yeye kujitetea au kuboresha hiyo ripoti yake. Sasa hapo unakuta kwamba kimemlenga *candidate* peke yake, kitu ambacho kitamuumiza kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema nilikuwa sijajiandaa vizuri kwa sababu ripoti yenyewe nimeipata sasa hivi, naomba tu niseme niunge hoja kwa sababu mwanzo ni mgumu, lakini baadaye kadri tunavyokwenda sheria hii itakuwa ni nzuri na lengo ni kuondoa rushwa na matumizi mabaya ya fedha katika nchi yetu. Tena nataka kusema naunga mkono hoja Muswada huu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa hii nafasi na mimi nichangie katika Muswada huu uliopo mbele yetu. Nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuweza kuwasilisha Muswada huu, lakini vilevile niishukuru Kamati kwa maoni mazuri ambayo imetuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja na ninaunga mkono hoja za Kamati na za Serikali. Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu ambaye kimsingi sheria hii inakuja kukamilisha lile wazo alilotupatia kipindi ambacho tuliingia katika kipindi hiki chetu cha uchaguzi ambacho kimsingi alilenga kuona kwamba uchaguzi ulenge kumpata mtu yule ambaye ana uwezo, ambaye anakubalika, ambaye ana uwezo wa kufanya ile kazi ambayo ameiomba. Nafasi ya Ubunge, nafasi ya Udiwani, nafasi ya Urais, yule ambaye anajua umuhimu wa nafasi ile na anaweza kutumikia nafasi ile, mtu ambaye ni mwaminifu, mtu ambaye ni muadilifu, mtu ambaye anatulia hata kukaa kusikiliza maoni ya wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema Rais ambaye ni sehemu ya Bunge hili, ametuwezesha kufikia kitu ambacho ni hatua nzuri na kimsingi Muswada huu unalenga kupambana na matumizi mabaya ya pesa ambayo yanakusudia kuitwa kwa jina moja rushwa. Tulikuwa tumefikia katika wakati mgumu sana ambapo inapofika kipindi cha uchaguzi kama hivi, si wakati unaokuwa na amani katika nchi yetu, ni wakati ambapo wale ambao ni walanguzi wa muda huu, wanautumia sasa kutafute njia ya kujineemesha, wanaona sasa ni wakati wa neema, kwa sababu kazi zao ni kuchuuza tangu asubuhi mpaka jioni, mpaka usiku kwenda kuanza kusaka nani anagombea kusudi kwake iwe mtaji, lakini akishampata yule basi anaanza kulinganisha nani anayefikiria kwamba atakuja kuwa na dau kubwa zaidi ili yeye ajifanye kwamba ni kiongozi wa msafara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo hayo sasa ndiyo yanaendelea kufanyika katika nchi hii ya Tanzania na si mambo kwa kweli ambayo yanaweza yakapata kiongozi bora au yakaleta kiongozi safi, isipokuwa tu tunaweza tukajaza nafasi, tukawa na Madiwani wengi, tukawa na Wabunge wengi, tukawa na Rais, lakini wote wakawa ni hovyo tu kwa sababu wamepatikana katika utaratibu usiofaa. Kwa kweli nadhani ni wakati mzuri ambao utaratibu huu unaolenga kudhibiti na kusimamia taratibu za mapato na matumizi ya pesa katika kipindi cha uchaguzi kwa mgombea na kwa chama ni wakati mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imetakiwa kwamba kila mgombea na kila chama kitakachoshiriki katika uchaguzi kitoe taarifa ya matumizi lakini pia kieleze vyanzo vyake, ni jambo jema sana. Kuna watu wengine hawana mpango wa kugombea lakini lengo lao ni kuvuruga utaratibu wa uchaguzi, lengo lao ni kuwawezesha wale ambao hawana uwezo, lakini

wanaweza tu wakawa watumwa wao sasa wanalenga kuandaa na kuwapa nafasi ili wakagombee, wawasukume kwa njia ya pesa ili wakipata nafasi hizo wakawe watumishi wao sio watumishi wa wananchi, lakini zaidi tumefika kipindi ambacho sasa watu wanaoandaliwa kwa *style* hiyo si pekee kwamba sio watumishi wa wananchi na kwamba ni watumishi wa wale tu wanaowatuma hata pia hawa ni watumwa wa nafsi zao na hata hawawezi kwenda kufikisha malengo ya wananchi kuwachagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapokuwa tumepata viongozi wa namna hiyo hatuwezi tukajisifu kwamba tuna viongozi bora, kwa hiyo, Muswada huu kwa kweli utakapopita na kuwa sheria hakika utadhibiti matumizi mabaya ya fedha, utadhibiti vitendo vya rushwa kwenye kampeni, lakini mimi naamini utaweza kutujengea msingi wa kuwapata viongozi wa kuaminika na kupata viongozi wenye nguvu na uwezo wa kutetea hoja za nchi na kusamia maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiria kwamba sasa uboreshwe vipi au mambo gani yatakayosaidia ili kuona kwamba Muswada huu unakwenda kusaidia sana. Walengwa ni Taifa zima, lakini kwa makundi makundi. Mimi nilikuwa naliangalia kundi la kwanza kwamba ni wananchi. Wananchi walikuwa wamefikishwa katika kipindi ambacho wanaomba na wanajadili, wana-*bargain*, kuna kuwa na *bargaining* ya kiasi gani ambacho wapewe, jambo hili ni hatari sana. Mimi nilianza kuingia katika siasa za kugombea mwaka 1995, ndiyo mara yangu ya kwanza niliingia katika kutafuta nafasi kama na mimi naweza kukubaliwa, lakini nilipofika kwa mara ya kwanza nikiomba nafasi, ilikuwa ni mwiko kabisa kwa mtu kuitaji pesa na hata yule anayekwenda kuomba kujaribu kupenyeza pesa hata kidogo, ilikuwa ni mwiko kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwaka 1995, mimi kwa historia yangu nilichokishuhudia, nilishuhudia wananchi wakiwaadhibu wagombea waliokwenda na pesa wakiwa wanasema umekuja kutununua? Kama umekuja kutununua hatukupi kura zetu, lakini sasa mwaka 2005 na 2010, kinyume chake sasa wananchi wamefika mahali pa kusema kwamba una nini, unataka kugombea una nini? Sasa hiyo hali kwa kweli ni hali inayoleta mchanganyiko kwa hiyo, lengo la kundi la kwanza mimi kwangu nasema wananchi kwanza, wapate elimu kiasi cha kutosha na waambiwe kabisa huko waliko watoke kwa sababu tunapokaa hapa kila tunachokijadili hapa, lengo na makusudi ni kuboresha maisha ya Taifa letu, lengo na makusudi ni kuona kabisa tunaweka mambo yetu vizuri ili mwananchi afaidike na nchi kama nchi ifaidike na ipate sifa kwamba tunafanya vitu vizuri katika nchi kama nchi, lakini na kwenye Mataifa mengine yajue Tanzania inafanya kitu kizuri na viongozi wake ni makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe mwananchi anapojiingiza katika kudai rushwa, na yeye kushiriki katika kusema umekuja na nini, anachokwenda kufanya sasa ni kwamba anahalalisha yeye kupoteza hospitali yake, anahalalisha yeye kupoteza shule nzuri, anahalalisha yeye kuchelewesha maisha bora, anahalalisha kupoteza barabara, mambo ambayo yeye ndiyo anatakiwa ayapate kwa kulinganisha ni nani huyu aliyempa nafasi. Sasa vitu hivi nasema kundi la kwanza ndiyo kuhakikisha kwamba yule mwananchi anaelewa kwamba unatakiwa ufanye uchaguzi kwa lengo la kupata kiongozi bora si bora kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kundi la pili katika hili ni kuhakikisha kwamba wale walio katika nafasi wanalindwa. Kweli mwisho wa uchaguzi ni mwanzo wa uchaguzi kimawazo, lakini kivitendo ni lazima aliye kwenye nafasi alindwe, sheria imlinde Diwani aliyepo, Mbunge aliyepo, imlinde Rais aliyepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mimi nashangaa uchaguzi unaambiwa ni katika miaka mitano, nafasi uliyoipata ni miaka mitano lakini kuna wengine sasa wameshafikia wakati uchaguzi ukimalizika tu *spirit* ile ile, Mbunge akienda Jimboni na wenyewe wanakuwa na wakwao Diwani, sasa haiwezekani nchi au jimbo au kata ikawa na viongozi wawili wanaofanya kazi sambamba lakini wakiwa ni wapinzani, hii haiwezekani. Lazima iwepo sheria ya kwamba yule mtu aliyepewa nafasi ya miaka mitano na wapigakura wenyewe amalize miaka yake mitano bila kuwa ameingiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa kundi la tatu liwe ni kwa wale wanaowania nafasi na wenyewe walindwe, walindweje sasa? Wapewe muda maalum wa kutangaza nia zao, si mtu analipuka tu wakati wowote anatangaza nia, kutangaza nia yake sasa anaitangazia kwenye mkutano wa hadhara wa jimbo, yeye ni nani? Ana kadamnasi huyu? Kwa sababu kundi limepewa aliyepewa ridhaa, kama hujapewa ridhaa nenda kwenye chombo, nenda kwenye gazeti. Siku mmekutana labda kwenye mkutano wa chama chako au mkutano mkuu tangaza, maliza, lakini ukishamaliza umemaliza, sasa kwa sababu ilikuwa ni ndani ya vyama, sasa imekuja ndani ya sheria, sheria itamke kwa sababu hawa ni viongozi wa nchi. Huyu anayetaka kuwania hii nafasi lini atangaze nia yake na kwa *style* gani. Haimaanishi kuzunguka kila mahali na kusema nia, hakuna nia hiyo kwenda kugawa pesa na hiyo inatupunguzia *credibility* ya kupata viongozi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaanza kubabaika hata kabla wakati haujafika. Kwa hali hiyo mimi ninasema kwamba tukisimamia hayo ni kwa uchache, lakini naamini kabisa yatakwenda vizuri. Sasa na hili nalo nilikuwa naomba liende sambamba na kuyaangalia madaraka ya msajili, katika hili naungana mkono na msemaji wa kwanza, alizungumzia sana juu ya msajili wa vyama, hata mimi nakuwa na mashaka kwamba kama mtu mmoja anapewa madaraka yote yeye peke yake, tusimuangalie huyu msajili aliyeko leo tu, tuangalie yeyote atakayeonekana ana sifa, kateuliwa anaweza akaingia na misingi yake, akaamua tu kukivuruga chama na kuwavuruga wagombea, kile chama kitalizwa vibaya sana. Madaraka yaliyo makubwa sana juu ya mapingamizi na ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi, mimi ningependekeza yakabaki kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana hata kuachia mwenendo bora wa uchaguzi, mimi ninashtushwa na kitendo cha kukuta katikati ya uchaguzi huyu mtu anaonekana hafai, halafu anaambiwa wewe nenda nje halafu mwingine aje, haya mambo yatatuyumbisha sana na labda yanaweza pia yasisaidie, lakini napendekeza kabisa kwamba yale masuala ya msingi, madaraka makubwa sana yanayohusu hasa mapingamizi juu ya mwenendo mbaya wa wagombea na vyama vyao yangesimamiwa na Tume ya Uchaguzi halafu yakaweza kuwa katika utaratibu ambao ni utaratibu mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi nilikuwa nafikiria kwamba nitachangia jioni kwa hiyo, kwa kunitamka sasa hivi, hayo machache ndiyo yalikuwa yako karibu sana. Naomba niseme kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE.SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie huu Muswada ni Muswada muhimu sana katika mustakabali wa Taifa hili, ni Muswada amabo utapelekea kuwa na viongozi waadilifu ambao hawakupatikana kutokana na hila, ghiriba, rushwa na vitu kama hivyo. Jambo hili ni jambo jema na tunapaswa kabisa kuliunga mkono, pamoja na kwamba bado tunadhani yako maeneo yanapaswa yaangaliwe ili kuufanya Muswada huu uweze kutekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri jambo hili limekuwa ni kero kubwa katika Taifa letu na Mheshimiwa Rais wakati analizindua Bunge hili alilitamka jambo hili, lakini inashangaza imechukua muda mrefu kuuandaa Muswada huu na mpaka kuufikisha katika dakika za majeruhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kufanya hivyo wamewanyima fursa Watanzania kuweza kutoa mchango wao wa maoni ili kuweza kuuboresha Muswada huu. Umekuwa ni Muswada wa kulipuliwa na kwa sisi ambao sasa hivi ndiyo tunaopata, hatukupata bahati ya kushiriki katika vikao vya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inatupa matatizo makubwa. *(Makofi)*

Lakini ili Muswada huu uweze kutekelezeka na ili kuweza kukuza demokrasia katika nchi yetu na kuwa na utawala bora, sheria zinazohusiana na masuala ya utawala na demokrasia ni lazima yaangaliwe sambamba na sheria hii. Ni lazima tuzipitie sheria za uchaguzi kama hiyo pia iliyoletwa leo, lakini pia ni lazima tuangalie sheria juu ya Tume ya Uchaguzi, sheria juu ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Maadili na Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vyombo vyote kwa namna moja au nyingine vinahusishana sana na masuala ya uongozi, utawala na demokrasia. Na tatizo kubwa lililoko sana ambalo linakera ni rushwa na ili kuweza kudhibiti rushwa, hatuwezi kuidhibiti rushwa kwa kutengeneza sheria tu peke yake bila kuwa na mikakati ya kujijengea uwezo wa kuisimamia sheria. Tuna sheria zipo tayari, lakini ni kwa kiasi gani sheria hizo zimekuwa *effective*, mimi sijui. Taarifa nyingi za rushwa zinatolewa, muda wa kuchunguza taarifa hizo ni mrefu, kesi zinazofikishwa mahakamani ni chache, kwa hiyo inakuwa tu kama vile kiini macho kwa Watanzania na ugonjwa huu unaendelea kuwepo. Ni lazima tufike mahali sasa tuangalie kwamba tumeimarisha vyombo vyetu vya kuisimamaia hii sheria ili hii sheria iweze kuwa na maana na makusudio ya sheria hii yaweze kuwa yametekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kwamba nimeupitia haraka haraka Muswada huu, sijapata mahala popote kuona eneo linalogusa mgombea binafsi. Suala la mgombea binafsi ni haki ya msingi ya Kikatiba, haki ya kuchagua na kuchaguliwa na sasa hivi Mahakama Kuu ya Rufaa inapitia chini ya jopo la Majaji kadhaa juu ya kadhia hii ya mgombea binafsi. Hofu yangu niliyokuwa nayo kama shauri hili litamalizika kabla ya uchaguzi huu wa mwaka huu wa 2010 nafasi ya mgombea binafsi katika Muswada huu iko wapi? Au ni kwamba Serikali imejiridhisha

kwamba wao kwa sababu ni warufani katika hili, rufaa yao itashinda kwa hiyo, ndiyo maana hawakutaka kuweka kipengele chochote kinachohusu mgombea binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili mimi nimeona kwamba ni pungufu katika Muswada huu na vinginevyo kama hukumu itatoka kabla ya uchaguzi na watu hawa wakapewa haki ya kushiriki katika uchaguzi wa mwaka huu sijui kama sheria hii itatumika au itasimamishwa kwa sababu haijampa haki, haijampa nafasi huyu mgombea binafsi. Lakini lingine ambalo nadhani kwamba ni vyema nalo tukaliangalia ni pale anapopatikana mgombea aliyepita bila kupingwa. Zipo njia nyingi zinazotumika za kumpata mgombea bila kupingwa ama mgombea anakubalika katika eneo lile au chama kile hakuna upinzani katika eneo lile au kwa hila, kwa ghiliba na kwa njia zingine zozote akajikuta mtu amebakia peke yake bila kupingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama tunataka kupanua demokrasia na kujenga misingi ya demokrasia yenye usawa, mgombea huyu kumtangaza amepita bila kupingwa nadhani ni kinyume na misingi ya demokrasia na utawala bora. Inapotokea ikwa hivyo, nilikuwa napendekeza kwamba mgombea yeyote atakayepata nafasi ya kuwa mgombea pekee, basi apigiwe kura za ndiyo au hapana na asitangazwe kuwa mshindi mpaka awe amepata zaidi ya asilimia hamsini ya kura zilizopigwa katika eneo lake, kama ni jimbo, kama ni kata na kadhalika, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewapa haki wananchi wale ambao mhusika anakuwa ni kiongozi wao. Mtu wa namna hiyo amechaguliwa na watu, tofauti na sasa wagombea hao wanaopita bila kupingwa wanachaguliwa na meza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili katika nchi yetu si jipya, si kwamba tunaleta dhana mpya au jambo jipya kabisa ambalo halijapata kutokea katika nchi hii, nakumbuka nimepata kushiriki chaguzi nyingi kutokana na umri wangu, wakati fulani wakati wa mfumo wa chama kimoja tulikuwa tukiwachagua wagombea kwa alama, ama jembe ama nyumba, ama yai, ama kuku na kadhalika, lakini tulipofikia kwa mgombea wa Urais tulikuwa tunapiga kura za ndiyo na hapana. Alikuwa ni mmoja lakini ni lazima apigiwe kura na alikuwa hawezi kutangazwa kuwa Rais wa nchi hii mpaka apate zaidi ya asilimia hamsini ya kura zilizopigwa. Kwa hiyo, nadhani jambo hili ni jema la afya kwa ajili ya kujenga demokrasia ya kweli katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nililokuwa nataka kuzungumza ni ya jumla tu kwamba sheria hii kwa sababu ya umuhimu wake na kwa sababu ya msukumo uliopo kutoka kwa wananchi, kutoka kwa viongozi kwamba ni lazima sheria hii iwe imepita na ianze kutumika katika uchaguzi unaokuja ni jambo zuri na ni jambo jema, mimi nalipongeza binafsi. Lakini kwamba limebeba mambo mengi kwa wakati mmoja, limebeba vitu vingi kwa wakati mmoja bila kuwepo na maandalizi ya kutosha haikutazama nini mahitaji ya wakati huu na mahitaji ya muda wa kati na muda mrefu. Tumetengeneza sheria ambayo imebeba vitu vyote ndani ya kapu moja na matokeo yake ni kwamba itakuwa ni ngumu kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ya msingi ambayo nitamuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha anipe ufafanuzi na maelezo. Moja kwa mfumo wetu ambao tumekuwa tukiutumia siku zote, Wakurugenzi wa Maendeleo ya Miji au Wilaya na Majiji, wamekuwa ndiyo wawakilishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi tunapofika katika nyakati za uchaguzi. Tume imeshindwa kujipanua, imeshindwa kusimama kama taasisi, hakuna mpango wowote wa kuifanya Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi kuwa ni taasisi ambayo inasimamia

masuala ya uchaguzi katika nchi yetu kama ilivyo katika nchi zingine zikiwemo nchi za Kiafrika kama vile Ghana.

Mheshimiwa Naibu spika, kwa hiyo, Tume imeendelea kuwatumia mawakala ambao ni watumishi wa Serikali, Wakurugenzi na Watendaji wa Kata na Vijiji na kadhalika ambao wote hawa ni waajiriwa wa TAMISEMI na wanawajibika kwa muajiri wao na wala hawawajibiki kwa namna yoyote na Tume. Kwa hiyo, jambo hili nilikuwa nataka nipate maelezo pamoja na kwamba najua Wakurugenzi ndiyo wanaowakilisha Tume, sasa Msajili anateremshwa mpaka kwenye jimbo la uchaguzi, nani atamwakilisha msajili katika maeneo hayo? Kwa sababu hamjamjengea uwezo Ofisi ya Msajili, hamjawajengea uwezo Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ni nani atamwakilisha?

Kwa hiyo, ni Mkurugenzi huyo huyo ndiyo atakuwa Msajili, anamwakilisha Msajili katika jimbo, Mkurugenzi huyo huyo ndiyo atakuwa anaiwakilisha Tume katika jimbo. Nitapenda nipate maelezo ni nani atawawakilisha ofisi hizi au taasisi hizi ambazo ni nyeti na muhimu katika mchakato mzima wa uchaguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi pia nashukuru kwa michango yenu, ninao wachangiaji wengi sitaki kuwataja majina maana wataniambia ulinitaja, lakini tunajaribu kuona kwamba tunapata wachangiaji wengi kadri inavyowezekana, halafu wakati huo huo tu *manage time*. Kwa hiyo, mimi wale wote walioomba wawahi, kuna watu walioomba hapa, wawahi, nikiwataja hapa watasema na mimi ulinitaja, muwahi. Kama baada ya makubaliano yetu tunaweza kukuta wote mmeshafikiwa muwahi, kwa hiyo, tukikutaja sasa, sio lazima tukurudie kama haupo, kwa hiyo, walioomba muwahi. Kama nilivyosema tuna Miswada miwili na hiyo yote lazima iishe leo, kwa hiyo, tutawasiliana. Waliomba wote wawahi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimesema asubuhi, leo tuna Miswada hii miwili ambayo lazima iishe leo. Lakini nikizingatia mazungumzo ya leo asubuhi niliona kulikuwa na mazungumzo ya jumla zaidi kuliko kuingia kifungu kwa kifungu ama kujadili Muswada.

Kwa hiyo, nitakuwa na wasemaji watatu. Tutamwita mtoa hoja halafu tuingie kwenye Kamati ya Bunge Zima ambapo kule tutakwenda kujadili kifungu kwa kifungu. Yule ambaye ana maoni kwenye kifungu hicho tunazungumza. Kwa sasa nitatoa nafasi kwa watu Waheshimiwa Wabunge watatu. Tutaingia Muswada wa pili, waliobaki hawa wataendelea. Kwa sababu

nimeona ile namna ya kuzungumza ni jumla. Kwa hiyo, tunaweza kujadili kifungu kwa kifungu tukiingia kwenye Kamati ya Bunge Zima.

Kwa hiyo sasa nitamwita Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella kama yupo na Mheshimiwa Jackson Makwetta, tuanze na hao. Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu ambao ni wa maana sana katika kukuza demokrasia katika Taifa letu. Lakini kama ilivyo kawaida naomba nichukue nusu dakika kuzungumza maneno mawili, matatu juu ya jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, karibuni hapa watu ambao tunalima pamba tumefurahishwa sana na Serikali kutupa pembejeo na kwamba tunaweza kununua mbegu kwa nusu bei na pia dawa kwa nusu bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nataka kusemea hapa naiomba Serikali sasa kuna watu ambao ni wajanja wanatumia nafasi hii kujilimbikizia fedha. Sisi watu tunaolima pamba tunaanza kulima mwezi wa Oktoba, Novemba, Desemba na ndiyo tunaponunua mbegu. Wakati ule hapakuwa na vocha, vocha zimekuja baada ya sisi kulima, baada ya sisi kununua mbegu. Sasa watu wanalazimishwa kwa kutumia vyombo vya Serikali, kwa kutumia watendaji wa Kata, kuweka sahihi kwa vocha ambazo hawakupokea na kwa hili likiachwa kuendelea ndiyo kusema watu watakuwa wanajichotea mapesa kibao na bila kuwasaidia wakulima. *(Makofi)*

Jambo hili naiomba Serikali mara moja ilichukulie hatua ili kuwapata hawa wajanja wajanja ambao wanataka kutumia nia nzuri ya Serikali ya kuwasaidia wakulima na wasihusishe mbegu mkataba mmoja na mambo ya dawa ni mkataba mwingine. Kama dawa ndiyo sasa zina vocha zipewe bila *condition,* bila masharti kwamba wasaini kwanza kwa ajili ya mbegu. Hilo nimemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada, kwanza nataka kusema wazi kabisa, sidhani hapa kunaweza kuwa na chama chochote cha siasa ambacho kinaamini kabisa katika kupata wawakilishi kwa njia ya kura kikapinga dhana ya kuwa na Muswada wa kudhibiti matumizi mabaya ya fedha katika uchaguzi. Hicho chama hakipo. Kwa hiyo, sisi *UDP* pamoja na wenzangu wote ambao wananisikiliza tunaunga mkono sana wazo la kudhibiti matumizi ya fedha ndani ya uchaguzi na jambo hili kusema kweli limeenda mbali mno. Watu wamefika mahali hata wanajitangaza kwamba mimi nachangia milioni 50 kwenda kumwangusha Cheyo na inaandikwa na kila mmoja anaona na haoni kuwa kwamba kufanya hivyo ni kuvunja sheria. Kama wafanyabiashara watajiweka kwamba wao watatumia fedha yao kutuchagulia nani awe Rais wa nchi hii, nani awe Mbunge wa nchi hii, nani awe Diwani, iwe Halmashauri ya namna gani, tujue kwamba tunajenga sehemu ambayo italeta machafuko katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyonge hawatakubali kwamba wao wachaguliwe Diwani ambaye tajiri anataka. Wananchi hawatakubali kwamba wachaguliwe Mbunge ambao wao wanamtaka, lakini matajiri hawamtaki kwa hiyo, wao matajiri wanamtaka ndiyo aende kuwa Mbunge. Wala nchi haitakubali kwamba tuletewe Rais ambaye amechaguliwa na matajiri wa

nchi hii. Najua wananchi wetu ni wadhaifu sana kwa hela. Najua wananchi wetu hawana fedha, watu hata wewe Naibu Spika, hiki kitu ambacho hakihusiki na chama. Nina hakika hata kwako sasa hivi kuna watu wanamwaga fedha kama njugu ili wewe uondoke kuwa Naibu Spika wetu, na wewe tunakupenda, unafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa msingi huo tutafute njia za kuhakikisha kwamba fedha haitawali, lakini ukweli ni kwamba fedha sasa ndiyo adui mkubwa wa demokrasia. Tusipoidhibiti hii fedha na ukiona watu wenyewe kwanza, wangeona kwamba ni afadhali wawe na mfumo huu mzuri wa vyama vingi kwa mfano, ndiyo unawasaidia hata kufanya biashara. Zamani tulipokuwa na chama kimoja kulikuwa na duka moja, tulipokuwa na chama kimoja kulikuwa vitu vya kuagiza kwa mstari. Leo kuna uhuru huu, uhuru huu unaletwa na ushindani wa kisiasa. Sasa wao wanataka kuumaliza huu ushindani wa kisiasa kwa kujipendekeza kwa chama kimoja tu. Hali hii nawaonya waache, kama unataka kusaidia vyama wasaidie vyama vyote. Lakini kwa utaratibu uliowekwa na sheria. Kwa hiyo, nilitaka kusemea hiyo dhana kwanza inakubalika, tufanye kila njia kudhibiti fedha ambayo sasa hivi ndiyo adui mkubwa wa demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujikita kwenye utekelezaji wa sheria yenyewe. Kwanza tuanze, ukiangalia na ukisoma sheria yote hii unaona kuna sehemu mbili za kudhibiti fedha. Sehemu ya kwanza ni kudhibiti fedha wakati wa mchakato wa kupata mgombea *(nomination process).* Sasa hii kwanza ina matatizo. Ukiangalia hata kwenye *article* ya tatu ambayo inazungumzia juu ya maelezo ya *nomination process* ni ya namna gani. Hii *nomination process* haina tarehe, angalau wangesema *nomination process* ni wakati kadhaa kabla ya *nomination day.* Kwa mfano, tunasema siku 90 kabla ya siku ya kuteua mgombea, ingejulikana kwamba wakati huu hiyo *nomination process* ndiyo kipindi ambacho tunashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakiko bayana ndani ya sheria na ya pili, hili jambo kabla ya uteuzi pia lina vipengele vingine ambavyo kwa mfano kipengele cha 14, *sub-article* ya pili zinamwambia Msajili ataweka utaratibu wa namna ya kuchaguana, kupata *candidate* unaofanana kwa vyama vyote.

Kwanza Katiba ya vyama hivi havifanani, mabaraza mbalimbali ya vyama vyetu yamepewa majukumu mbalimbali. Kwa mfano katika *UDP* tunasema tunapata, wewe unakuwa mgombea utakapothibitishwa na Mkutano Mkuu wa Wilaya wa Chama, ndiyo utaratibu wetu. Najua ndugu zangu katika Chama cha Mapinduzi wenyewe wana utaratibu ulio mrefu zaidi, sijui uende nyumba kwa nyumba, kata kwa kata, kitanda kwa kitanda. Huo ndiyo utaratibu wa kwenu. *(Makofi)*

Sasa unaposema huyu Msajili atengeneze *uniform* ndiyo kusema turudi tena kwenye vyama vyetu, twende kuhakikisha kwamba hata ile Katiba ya vyama vyetu na yenyewe tumeirekebisha kufuatana na sheria hii. Wakati wa kufanya mambo kama hayo kwa vyama 18 uko wapi? *(Makofi)*

Jambo la pili, ukiangalia katika *article 24, sub-article (1)* hili jambo limesema kwamba lazima kila chama kiweze ikiwa imemaliza utaratibu wake wa kupata wagombea siku 30 kabla ya tarehe ya uteuzi. Hebu tuangalie siku 30 maana yake nini. Siku 30 kama kwa mfano na ndiyo inavyoonekana itakuwa, kwamba siku ya uteuzi ni tarehe 16 Agosti. Kwa hiyo, kama siku 30

kabla ya siku hiyo, lazima tuwe tumepata wagombea tarehe 16 Julai. Kwanza ukileta jambo kama hilo Bunge hili mwezi wa Julai, mwezi wa Juni halitakuwa na watu, kwa sababu kila mmoja atakuwa jimboni kule nyumbani kuhakikisha kwamba amekuwa mgombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika kama wengine watakaokuwa wameshakataliwa tayari kule Bunge lako hili tunapojadili mambo ya Bajeti mimi na wewe kitakuwa ni kichekesho sana, maana yake mtu anajadili akijua kwamba yeye hatakuja tena kuwa Mbunge. Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba hilo nalo pia ni lazima liangaliwe. *(Makofi)*

Mimi nafikiri tungeweza kusema tu kwamba *with in 30 days* badala ya *before* tuseme katika muda wa siku 30 kabla ya siku ya uteuzi. Hiyo mimi naona inawezekana. Lakini haiishii hapo tu, kuna jambo lingine, pia katika mambo haya ya ku-*dis qualification* tumetoa, kusema kweli madaraka makubwa sana kwa Msajili pamoja na kwamba mimi namwamini Msajili. Lakini madaraka makubwa mno kwa Msajili na siyo hivyo tu. Sasa tumeunganisha *dis-qualification* na *process* nzima ya uchaguzi ambapo mimi ningefikiri *dis-qualification* ingekaa tu peke yake. Mtu anaweza kuondolewa wakati wowote tu, maana yake mimi sioni itawezekanaje kwa Msajili aangalie makabrasha ya *aspirants* wa Chama cha Mapinduzi nchi nzima. Aangalie vyama 18 aangalie madiwani, wagombea wote, halafu aseme kwamba huyu ni sawa huyu hapana, huyu nini. Itawezekanaje, *the job is just impossible. (Makofi)*

Kwa hiyo, tutafika mahali, aidha, kazi hiyo haitanywa kwa ufanisi kama tunajua hilo, kwa nini tunatunga sheria ambayo tunajua kwamba haitatupa matokeo ambayo yatakuwa mazuri. Wewe mhalifu aangaliwe tu, popote pale kama akipita *nomination day* awe *dis-qualified* baada ya *nomination day.* Hii ndiyo ingeweza kuleta ufanisi wa hii sheria na hatutakuwa tumembana Msajili kwa jambo lolote. Kwanza ukiangalia sheria yenyewe vile vyote vinavyopelekwa kule ni *confidential* yaani vyote ni siri. Sasa huyu Msajili atakayepekua majina ya watu wote wale halafu yeye *in his own motion* ndiyo aseme kwamba huyu nampinga. Hapa unajua na siasa bwana, leo tunaweza kuwa tuna Msajili mzuri, kesho tuna Msajili anayefanana na chama ambacho anakitaka yeye. Utaona watu wa chama fulani wanaondolewa kwa sababu ya *motion* kama hizi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, imekuwa haitusaidii, lakini la mwisho kwa sababu kengele imekwenda, natumaini wengine watajazia, ni mambo ya *reporting.* Ukisema kwamba eti *accounts* zote ziende pale zimekuwa *audited* na *CAG*. Nimempigia simu *CAG,* kwanza nimesikitika, pamoja na kujadili hii na wadau wengi, *CAG* hajaulizwa. Sasa mimi ambaye nafanya mambo ya *Public Accounts Committee* hii ni kazi ambayo haiwezekani kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali. Jambo ambalo lingeweza kuwezekana tungesema *the year following elections* basi *accounts* zote za matumizi ya uchaguzi ziwemo, kwa vile hatakuwa amezikagua zote. Lakini sasa tunachotaka kufanya eti afanye *special audit.* Nimeuliza hili swali mtu mmoja akasema aah, kama ni gharama basi ndiyo gharama ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rahisi kusema hivyo, lakini kama tunaweza nchi hii haina pesa. Kama tunaweza tukahakikisha kwamba pesa zingine tunazitunza kwa sababu ya shughuli zingine, tufanye hivyo. Mimi nafikiri kwamba hii *clause* pia napenda iangaliwe, afadhali tuzungumze *the year following elections* ndiyo *expenses* zote na *reports* zote ziweze zikakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Sikubaliani na mtu kusema tu kwamba

tutamwongezea Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali nyenzo, wewe utamwongezea fedha kutoka wapi?

Sasa hivi yeye mwenyewe bado analia anahitaji fedha nyingi hapati, leo unasema unaongeza tena ma-*accounts* kibao unasema utampa hela, hela unampa kutoka wapi? Kwa hiyo, hii ni kama vile tena tunatengeneza sheria ambayo haitekelezeki. *(Makofi)*

Mwisho naomba Waheshimiwa Wabunge muangalie vifungu hivi. La sivyo sheria hii itatufanya tufike mahali ambapo kila mmoja anakwenda Mahakamani bada ya uchaguzi huu. Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tutaenda kujitetea huko huko. Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella, atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Makwetta.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda niseme hiki kitu tunachokifanya hapa ni mapinduzi makubwa katika historia ya nchi hii na kwa Afrika nzima. Ni nchi chache zenye ujasiri kama Tanzania ambayo tunaweza tukaona athari za vitendo vyetu na kujisahihisha haraka. Nataka nianze kwa kusema kwamba nadhani tulitoa mwanya wa kila mtu kuangalia *process* ya Muswada huu, vyombo vya habari na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba kwa sababu nchi huwa inasikiliza vyombo vya habari sana, mimi nataka niseme Muswada huu kati ya Miswada yote ndiyo ambao umezungumzwa wazi wazi kwa upande wa Chama Tawala na Upinzani wote tumefanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isiwepo mtu akafikiria kwamba Waheshimiwa Wabunge hawataki Muswada huu, kazi tuliyoifanya hapa ilikuwa ni ya kuboresha Muswada ambao ni muhimu sana katika demokrasia ya nchi yetu. Kwa hiyo, yote tuliyozungumza na yote tuliyoyafanya ilikuwa wote tunaboresha Muswada na tunaendelea kuuboresha. Kwa hiyo, kusiwepo na hisia kwamba Wabunge walitaka kuukataa, huwezi kutu-*judge* ya kwamba tulitaka kuukataa kabla hata hatujauzungumza na huwezi kusema chakula kimeungua kabla hakijatoka jikoni. Kwa hiyo, tulikuwa tunapika tu Watanzania wote waelewe tulikuwa katika mapishi. Sasa ndiyo tunapakua. Ndiyo muonje kazi tuliyoifanya kwa siku zote hizi. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo nataka niliseme ni kwamba huu Muswada ni wa muhimu. Hakuna mtu anayekataa kwamba hakuna rushwa ndani ya chaguzi, wote, wote, wote tumeona watu wanatoa rushwa. Kama hujatoa umeona watu wanapokea rushwa, ambayo ni mwiko mkubwa kabisa na hasa sisi wana CCM inasemwa kabisa katika Kanuni zetu ya kwamba rushwa kwangu ni mwiko. Kwa hiyo, sasa hivi lazima tubanane kama tulikiuka hayo maadili turudi kwenye maadili na tusilionee aibu ya kurudi kwenye maadili na hata ukiangalia katika Sheria ya Rushwa katika nchi hii imekatazwa, tuseme Muswada huu unaongeza tu kukazia yale ambayo tulishayakubali hapa.

Kwa hiyo, tusionekane ya kwamba tunafanya vitu vya ajabu, tulishakubali katika Muswada wa Rushwa na sasa hivi tumeendelea kuufanunua zaidi, matumizi hayo hasa yanayoelekea katika sehemu ya rushwa na nitashangaa kama kuna chama hapa kitaonyesha kidole kwa mwingine. Hilo nitalishangaa sana kwa sababu kuna watu wanapenda sana kujikosha kosha oooh ni CCM, si kweli. Mimi nasema wote tukubaliane hapa tukitoka hapa, hakuna mtu kuhonga na ambao wameshahonga honga huko majina yakatwe, wasiingie kwenye msafara huu wa kupigiwa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chama kitakachopitisha watu ambao wameshajivuruga vuruga kule kugawagawa vijisenti, kichukuliwe hatua. Chama chochote kile kichukuliwe hatua kwa sababu wamekuwa wakiona. Watu wanapita wanagawa pesa, wananywesha watu pombe, watu wanafanya vituko vya kila aina. Sasa mara huyo ndiyo aje aletwe kwenye Bunge baada ya kupitisha Muswada huu. Hiyo lazima wote tukubaliane si Chama cha Mapinduzi wala chama kingine chochote katika vyama vile 18 tunaruhusiwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kusema, uchaguzi bila rushwa inawezekana? Ndiyo! Baadhi yetu tuliomo humu tulioingia zamani hili jambo ni jipya, jipya sana. Sisi tulikuwa tunaingia kwenye chaguzi kwanza majina saa nyingine yanatangazwa siku chache kabla ya uchaguzi. Unakwenda kujieleza. Mimi uchaguzi wangu wa kwanza niligombea Bunge la Afrika Mashariki nikiwa ndiyo natoka tu Chuo Kikuu na nilipita. Kwa sababu walichokiangalia ni sifa zangu, uwezo wangu, wakanichagua kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, sikuanzia hata Bunge la Tanzania. Lakini nilikuwa napita naomba. Unakuta watu wamesimama, jamani na mimi mnifikirie, mimi ndiyo naitwa Mama Mongella. Unaeleza, unamaliza unaenda kikundi kingine pale pale *Karimjee Hall.* Wakifika wanapiga kura kwa utashi wao, wanaweza kukunyima, wanaweza wakakupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siku hizi badala ya kuomba hivi, tunaomba hivi. Kwa hiyo sasa, kwanza ile inatuumiza. Wale ambao hatuna biashara, hatuna pesa, hizo pesa unapata wapi. Mimi naunga mkono hoja hii kwa sababu itaniondolea shida. Nitakuwa naomba tu hivi jamani, jamani, mmeniona mwenzenu, nimezungumza huko Bungeni, Serikali imesikia, mmeletewa umeme, mmeletewa feri mpya, mmeletewa hivi, ndiyo Chama cha Mapinduzi na Serikali yake ilivyo, mnichague tulete vingine. Hiyo ndiyo itakuwa hoja. Lakini mkienda unafunika kiganja, kwenye kiganja cha mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo sasa kwa sisi ambao kwa kweli zaidi ya kuwa tunaamini tu sera safi na usafi wa siasa ili tulinde amani ya nchi hii kwa sababu katika nchi nyingine mauaji haya mnayoyaona kila siku mnasema Bara la Afrika inatokana na hongo, wakisha honga anaingia Rais siyo safi, anaingia Mbunge siyo safi, anaingia Diwani siyo safi. Tusichezee mchezo wa kutumia vibaya pesa hata kama ni zako binafsi katika kuchagua viongozi na wananchi wana matatizo mengi, wanahitaji viongozi makini, *committed,* wenye uwezo, wenye uzoefu, wenye kujitolea, ndicho wanachohitaji na sisi humu tunahitaji katika kuiendesha nchi kwa sababu tunapokuja kwa pamoja unakuwa Mbunge wa eneo lako lakini unachangia katika maendeleo ya Taifa zima na nikitoa hoja ambayo inasaidia, itasaidia nchi nzima, haitasaidia upande wangu tu ama eneo langu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niseme hivi katika kutumia vibaya pesa, tumeanza udalali wa siasa. Watu wanabidi, siasa haiendi hivyo. Huwezi kuita sijui nani Majembe, anaitwa nani yule *Majembe Auction Mart* ama *Yono Auction Mart* ukasimama pale yeye ananadisha, Mama Mongella sasa naenda kwa shilingi ngapi. Hatuwezi kujenga Taifa hilo kwa namna hiyo, kazi iliyo mbele yetu ni kubwa zaidi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo nataka niseme kipengele kimoja, je, tumeweka uwezo wa kusimamia sheria hii? Mimi nina wasiwasi, kwa hiyo, tukishaipitisha hii Sheria mara moja taasisi husika na Serikali ziende zikafanye kazi ya kuhakikisha kila mahali kuna watu wanaotosheleza kusimamia Sheria hii wakati wa uchaguzi. Sheria hii ni hatari kama tutaitumia bila kuwa na wasimamizi makini. Anaweza akakugeuzia ikakukata, ina makali pande zote mbili. Mtu anaweza kusema huyu alihonga au hakuwa na risiti. Risiti mimi nakwenda kwenye Visiwa risiti ya mtumbwi naipata wapi? Atawaambia mama ingia, hana risiti anajiendeshea biashara yake kwa kukusanya tu. Sasa mimi niache kwenda kwenye Kisiwa cha Irugwa kwa sababu tu hana risiti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna mazingira magumu. Lakini ukiwa unapanda mabasi ya *public* na vitu vingine ni rahisi kupata risiti zote. Kwa hiyo, umakini, usimamizi wa kutafuta watu watakaosimamia, mimi nafikiria Ofisi ya *DED* labda katika Wilaya nyingine, katika Wilaya zilizo nyingi wako *under staffed, unless* wafunge shughuli zote za Wilaya na tunawategemea wale ndiyo watakaokuwa wanaendesha Wilaya zetu wakati sisi tuko katika mchakato wa uchaguzi. Lakini kwa kuongezea hili watafika mahali kazi nyingine zote zitasimama na kazi itakuwa moja tu ya kukimbizana na wale wanaogombea.

Kwa hiyo, hiyo *capacity* ya kutekeleza sheria hii mimi ndiyo nataka kwa kweli tukishamaliza kuipitisha tu haraka Serikali kati ya sasa na hapo tutakapofika kwenye kura za maoni wawe wameweka watu makini wa kusimamia Sheria hii. Kitu kizuri kinaweza kugeuka kikawa kibaya kwa sababu tu hakikutekelezwa vizuri. Wengi wasioipenda sheria hii wanangoja hii sheria i-*fail*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuzuia ku-*fail* ni kuhakikisha ya kwamba tumeweka watu makini wa kusimamia sheria hii na pia wananchi wetu, hii ni mpya. Tafsiri iwepo haraka ya Kiswahili. Twende tukaieleze vizuri ili kila mwananchi ajue ya kwamba ukipokea hongo, utaingia kwenye hatia kwa Sheria hii ya sasa. Isije ikawa watu wetu kila siku wanaburuzwa kupelekwa Mahakamani kumbe hakujua ya kwamba na wengi sasa hivi ukienda huko ambako watu wanatamba sisi tuko hapa tunafanya kazi, wataburuzwa Mahakamani. Wengi tunaweza hata kuburuzwa kwamba wewe umepokea hongo kumbe hakujua sheria inasemaje. *(Makofi)*

Kwa hiyo, semina za hawa wananchi wa kawaida na sasa hivi kwa sababu tumemaliza uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tuwatumie Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa na Vitongoji kuhakikisha kwamba wanapata sheria hii kwa Kiswahili na maelezo ya ziada ili hiyo kazi tupewe ama mwezi mmoja ama miezi miwili ielezwe kinaga ubaga watu wetu waelewe. Watu wetu wakielewa ndiyo watakuwa walinzi wa sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema tunaunga na mimi nikiwemo, naunga hoja mkono na vyama vyote tunavyozungumza na kwa sababu kuna uhuru kuna wanaosema, lakini wataunga baadaye. Najua Mheshimiwa Dr. Slaa akipata maelezo ya kutosha anaunga tu mkono siyo mtu mbaya. Kwa hiyo, naunga hoja mkono na yeye anifuate baadaye katika kuunga mkono. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pili, ningependa kupewa nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mkristo na katika Msahafu wa Kikristo kuna hadithi kwamba Wayahudi walimkamata mama mmoja katika kosa la uzinzi. Kwa hiyo, wakampelekea Yesu wakisema, wakitaka kujua kama anafuata Sheria za Musa. Kwa hiyo, alisema huyu mama amefumaniwa akifanya kosa hili na kwa Sheria za Musa inatakiwa apigwe mawe mpaka afe. Wewe unasemaje? Yesu akawauliza nani kati yenu hajafanya kosa hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akainama, wataalamu wa Msahafu wanasema kwamba alipoinama alikuwa anaandika dhambi ya kila mmoja kwenye karatasi akasema wewe tarehe hii ulifanya hivi na wewe tarehe hii ulifanya hivi, kwa hiyo, alipoinuka wote kwa kuwa kila mmoja alijiona dhambi zake zinaandikwa kila mmoja alitoweka na mwisho Yesu akajikuta amebaki na yule mwanamke mzinzi peke yake. Sasa kama lingekuwa ni darasa mimi ningeuliza ni nani kati yetu hapa ameingia hapa hakutoa hongo? Na asimame au anyooshe mkono, kama ingekuwa ni darasa. *(Makofi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wengi walinyoosha mikono)*

**NAIBU SPIKA:** Kanuni haziruhusu. *(Kicheko)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru hairuhusiwi lakini *message sent* kwamba kwa misingi hii tunazungumzia ajenda ambayo inatusuta wenyewe kama alivyosema Mheshimiwa Mongella pale. Kwa hiyo, sisi hapa tunatunga sheria ya kuzuia biashara ya kununua uongozi katika nchi hii na nashukuru kwamba mlionyoosha mikono kama ni kweli mmekuja hapa bila kununua uongozi wenu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano alipokuwa anafungua Bunge hili, alianza na maneno kwamba ni vizuri tutunge sheria itakayozuia tabia hii. Kimsingi ni lazima tujiulize, hivi mtu bora yeye mwenyewe anasimama kwa kiburi kwamba anafaa kuwa kiongozi na watu wamchague kwamba anafaa bila kuambiwa na wenzake kwamba anafaa? Inahitaji ushupavu wa aina yake. Chema chajiuza, kibaya chajitembeza. Watu bora wanapata taabu sana kugombea uongozi kwa sababu hawaelewi kama ni kweli wanafaa, lakini anayeona anafaa na wengine wote hawafai, nadhani ana kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili nadhani pamoja na kwamba wengi mmenyoosha mikono lakini nadhani kama ni treni, ilikuwa nje ya reli. Kazi yetu kubwa ni kurudisha treni kwenye reli na ndio Muswada huu. Ni nani mtu mwenye akili timamu, mpenzi

wa demokrasia na haki anaweza kupinga Muswada huu? Hakuna. Tunachozungumzia hapa kama alivyosema Mheshimiwa Mongella pale, ni namna ya kutekeleza lengo na madhumuni ya Muswada huu. Sheria hii peke yake haitoshi, ni lazima iambatane na utashi wa kisiasa. Upeleke kwa *tender,* kwa *PCCB,* polisi, wapi, bila ya sisi wenyewe hapa au bila ya wanaogombea kuwa na *political will* na nia ya kuzuia uchafu huu ni kazi bure. Ni kazi ngumu sana kwa kusimamia, maana rushwa ni siri ya watu wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa napendekeza kwamba kwanza, kazi ya kuuelimisha umma wa nchi hii ianze sasa na kwa haraka. Serikali igharamie, itenge fedha ianze kusema ubaya wa rushwa na vitendo vinavyofanana na rushwa ili wakatae kusudi tutekeleze nia hii. Maana hapa katikati sasa ilikuwa kama ni utaratibu kwamba ni sharti, ni wakati wa mavuno, kwa hiyo, rushwa ni sehemu ya uchaguzi. Bila kuandaa umma, bila kuandaa hawa watu, wananchi wanaochagua, ni kazi bure, inakuwa ni kazi ngumu sana. Nilidhani hili lingekuwa ni jambo la haraka amblo tunaweza tukalifanya bila matatizo yoyote na hii ni kazi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili nimesema tujisahihishe, tufungue ukurasa mpya katika uchaguzi. Kama alivyosema Mheshimiwa dada yangu pale kwamba hata sisi wenyewe hapa tutakuwa tumepata unafuu. Maana kama ni lazima uende na mfuko, hizo hela ziko wapi? Wanasema sijui ni makampuni, fedha za nje na za ndani, kwanza hata kuomba omba ni aibu sana, unahitaji *special courage* kuomba omba. Kuomba fedha ili ukapate uchaguzi!

Sasa hii itatupunguzia kazi lakini tuanze kwanza na elimu kwa umma. Kichafu hakiwezi kusafisha uchafu. Huwezi kuchukua mfagio wenye kinyesi cha kuku ukawa unasafishia nyumba, utakuwa unaeneza uchafu tu na ndio maana wakati mwili ukishakuwa mchafu, *you are not decent; decency is power in politics. When you are clean, you can afford to say anything* mbele ya watu; lakini kama ni mchafu si unaogopa kwamba wanakujua? Kwa hiyo, unabaki kubabaisha babaisha tu, maana wananchi wanatujua. Nani mwizi nani mchafu, wanatujua; wanatujua sana ila sisi tunadhani kwamba hawatujui. *We can hide but we can’t escape.* Watu wanatujua! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa tunapigiwa kura kwamba nani mchafu kupita mwingine yeyote yule, wangesema wewe mchafu, wewe mchafu, wewe mwizi, wewe namna gani. Mimi nashukuru Waziri Mkuu pale, umetangaza umaskini wako, ninasema kwa nia nzuri tu, kwamba una nyumba sijui ya pango Mpanda au wapi na shilingi ngapi. Tunapotangaza hizi hela tayari zimepungua, sasa inawezekana leo haziko tena. Kwa hiyo, hii ni kazi ngumu sana lakini nayo ni *courage,* ukishakuwa msafi wa vitendo, kauli na tabia yako unakuwa *clean.*

Mheshimiwa Naibu spika, nguvu ya Hayati Julius Nyerere ilikuwa ni kwa sababu ya usafi. Aliweza kusema lolote popote pale kwa sababu alikuwa msafi, alikuwa *decent. When you are dirty,* huwezi ukathubutu kusema baadhi ya mambo mbele ya watu kwa sababu watasema aah, si wewe tunakujua, ila tu hapa unajificha tu. Si wewe mwenyewe. Na ndio maana baadhi ya mambo haya yanakuwa magumu, hii sheria ni mwanzo wa safari ndefu. Tutapitisha sheria hapa lakini sasa ni lazima tuendelee kwenye maeneo mengine na natumaini kwamba mwanzo huu hautarudi nyuma tena. Kama ni treni, tuanze kuirudisha pole pole lakini tufungue ukurasa mpya kila mmoja na wananchi wataelewa tukianza hasa kwanza kuwaelimisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Fidel Castro wa Cuba, aliwahi kusema kwamba katika....

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, yupo bado!

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani ni mgonjwa aliwahi kusema kwamba katika nchi za kibepari madaktari hutibu pesa, wakati katika nchi za kijamaa madaktari wanatibu ugonjwa. Ningeweza kusema hapa kwamba katika nchi za kimaskini na za kibepari vilevile watu huchagua fedha na sio viongozi. Hivi katika nchi kama Amerika, unadhani Rais atatoka mtu maskini? Ni hela na katika nchi hii kama tusipoangalia itafikia wakati nchi hii sasa, Bunge litakuwa ni la matajiri, shughuli zitakuwa ni za matajiri na hao ndio watakaoelekeza nchi iende wapi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa nasoma kwenye gazeti wakasema kwamba wasomi sasa washike hatamu katika chama, chama chetu ni cha umma sio cha wasomi tu. Kwa hiyo, hata hilo tuwe waangalifu kwamba hii umma zaidi ya milioni tatu washikwe na watu watatu! Kama ni hivyo ni lazima tuanze upya, tumeweka masharti kwamba ajue kusoma na kuandika, basi tubaki hapo. Kitakachoamuliwa ni umma wenyewe, anafaa hafai, lakini kwanza amesema wawe wasomi! *I think this is a departure* kutoka kwenye *principle.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo mimi nilidhani tuseme kwamba hili suala la utashi wa kisiasa liwe namba moja. La pili, elimu kwa umma iwe namba mbili na tatu, sisi wenyewe hapa tuamue na tukiamua sisi hapa ni wengi, tutaonesha njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, mimi nilikuwa napendekeza kwamba kwa Muswada kama huu ambao unagusa vyama vyote, wakaone ni vizuri hata viongozi wa vyama vyenyewe wawe wanakaa pamoja. Kwa hiyo, tuanze kujenga utamaduni wa demokrasia ya kweli, maana ni kazi bure kuunda vyama vingi vya siasa kwa lengo la kuboresha demokrasia wakati nchi imejaa rushwa. Ni kazi bure hata ungekuwa na vyama 100, kama hatuondoi rushwa, hakutakuwa na haki, hakutakuwa na demokrasia, tutakuwa tunaendesha nchi ambayo ni hivi hivi, matarajio ya wachache, wenye fedha ndio wanaamua hapa na kuhonga honga kila mtu hapa na baadaye tunakuwa kama vivuli tu vya hao. Kwa kuwa kunakuja Muswada tena wa kutengenisha uongozi wa kisiasa na biashara na mali, mimi nadhani vilevile huu mwanzo huu ni mzuri, ni mwanzo mzuri. Ndassa uamue, unataka kuongoza watu au vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, Plato alikuwa ni Muitalia alisema binadamu ana sifa kubwa tatu; tamaa, akili, alikuwa Mgiriki, alikuwa na sifa tatu, tamaa, ushupavu na akili ya kuongoza na hii kwa mtu wa kawaida imegawanywa sawa sawa katika ubongo wake lakini mwenye akili atawale maana hana hulka wala tamaa ya kukusanya mali. Huyu mwenye ushupavu awe askari, huyu mwenye tamaa afanye biashara. Ukichanganya na kugeuza ukamuweka huyu anayependa mali awe mtawala, kazi yake itakuwa ni kukusanya tu kwa sababu ndio hulka yake; huyu shupavu atakuwa kazi yake ni kupiga watu mabomu tu na huyu mwenye akili hana hulka ya kukusanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati Afrika ya Mashariki iliwahi kuwa na watu wanaofanana na hivyo. Iddi Amin, tunamfahamu alikuwa Uganda, na kazi yake shupavu na Kenya ilikuwa na yule hayati... mlijua wenyewe. Aliwahi kumchagua Waziri mmoja akakuta hana gari, akasema *what have you done to yourself since I appointed you as a Minister?* Kwa hiyo, akasema kuanzia kesho kachukue gari, umefanya nini tangu nikuteuwe kuwa Waziri maana huna mali? Na Tanzania kulikuwa na nani? Basi tujifunze kutoka hapo, nguvu ya Nyerere ilikuwa ni *decency,* ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Naona mwalimu wangu kasema leo kali kabisa, haijapata kutokea. Maana huyu ni Mwalimu wangu mimi.  Sasa kwa sababu huu Muswada ni wa Vyama vyote, *CHADEMA* wamesema, *UDP* wamesema, *CCM* wamesema, *CUF* sasa nawaomba waseme; Mheshimiwa Mnyaa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. *ENG.* MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi angalau kwa kunipa nafasi nikatoa mchango wangu mchache na kwa kujua muda unavyotupa taabu, nitajaribu kuchangia machache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri na kumpongeza Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Muswada huu pamoja na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa namna walivyoweza kufanya marekebisho makubwa sana na nikiri kwamba Muswada huu lile toleo la mwanzo na hivi sasa kuna mabadiliko makubwa sana na kwa 80% Muswada huu ni mzuri sana. Kweli kulikuwa na mambo ambayo yanahatarisha lakini kwa busara za Waziri Marmo na Kamati husika ya Mheshimiwa Lubeleje, na wakajali wadau walioleta mapendekezo yao ambayo 90% yamekuwa *incorporated* humu mimi upande mmoja napongeza. Na suala la kuunga mkono au kutounga mkono, itabakia hii 20% na Waziri atakavyofanya marekebisho atakapotujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hayo kuna ushahidi ambao huu Muswada ulikuwa una matatizo sana. Kwa mfano katika toleo la zamani Ibara ya 4(2), ambacho kilimfanya Msajili aweze kuingilia kazi za Tume ya Uchaguzi, kimefutwa, hicho ni kitu kizito sana. Ibara ya 11(4), ambayo mwanzoni katika toleo la zamani ilimzuia mgombea kutokupokea mchango wowote kutoka hata kwa wananchi wa Jimbo lake kumsaidia katika gharama za uchaguzi, nayo pia imeondolewa na imewekwa sasa inaruhusiwa Mgombea aweze kuchangiwa kama alivyochangiwa Barrack Obama. Basi mgombea katika Jimbo lake au Rais katika Jamhuri nzima anaweza kuchangiwa na wananchi. Na isitoshe imeboreshwa zaidi katika hiki kipengele ambacho ninakifurahia sana katika Ibara ya 11(5), kwamba sasa kwa wale watakaokuwa na nia ya kumchangia Mgombea katika gharama hizi za uchaguzi, asipate vitisho vya aina yoyote, asipewe hujuma ya aina yoyote, asifanyiwe *disturbance* ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapo zamani tunajua; kwa mfano sisi katika vyama vingine ilikuwa mtu akikisaidia chama cha *CUF,* basi anawekewa vikwazo kazini. Sasa kutokana na sheria hii kipengele cha 11(5), ina maana mimi kama *organisation* yoyote hapa ndani au mtu anataka kunisaidia, jamaa yangu, leo anaweza kunisaidia katika pesa za kugharamia uchaguzi na kama atatishwa na mtu yeyote basi huyo mtu ana kosa la jinai na huku kifungu chake cha adhabu kimewekwa. Kwa maana hiyo, sasa Muswada huu wa vipengele hivyo vimepata uboresho mkubwa. Vile vile katika Ibara ya 23(6) ya *conveyance,* kusafirisha kwamba sisi kwa mfano kule

Visiwani, kuna watu wametengana kwa bahari, sasa hivi wanaweza wakaja wakashughulika kutoka Kisiwa kingine kwenda Kisiwa kingine; imetajwa katika Muswada huu. Kwa hivyo, hayo ni maendeleo makubwa na ni lazima tuipongeze Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala na Waziri mhusika kwa kufanya marekebisho hayo ambayo yalikuwa yanahatarisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nililokuwa nataka kulizungumzia na pengine hili ni zito kidogo kwa maoni yangu, katika Ibara ya 28(1), inayoruhusu matumizi ya vyombo vya habari vya Serikali. Muswada huu kwa wale wagombea Urais, wameruhusiwa kutumia vyombo vya habari vya Serikali, *Televisio*, Redio, kwa matumizi yaliyo sawa; kupewa *air time* iliyo sawa na havitakiwi vyombo hivi kuhujumu au ku-*destort information* ya mgombea yeyote yule wa Urais wa chama kingine chochote, kwa hiyo, haya ni maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba Mheshimiwa Waziri, aiunganishe Ibara hii ya 28(1) na Ibara ya 10 ya Muswada huu ambayo inasema *Limit of election expenses*, ambapo Ibara hii ya 10 Mheshimiwa Waziri, amepewa uwezo kulingana na ukubwa wa Jimbo, kulingana na idadi ya watu katika Jimbo, kulingana na uchaguzi wa Diwani, uchaguzi wa Mbunge, amepewa uwezo wa ku-*limit election expenses*. Sasa hapa ukichukua Ibara ya 28(1) na hii Ibara ya 10, kuna jambo limejitokeza hapa zito sana kwamba hapa vimezungumziwa vyombo vya habari vya Serikali, lakini Muswada huu haujazungumzia vyombo vya habari vya binafsi hata kidogo na ikiwa kuna *limit* ya *expenses* leo vitaunganishwa vipi vyombo vya habari vya binafsi ambapo kuna wagombea aidha, katika nafasi za Ubunge au katika nafasi za Udiwani au katika nafasi za Rais, wanamiliki vyombo vya habari; kwa maana ya Redio, *Television* au hata magazeti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *coverage* ya watu hawa itakuwa ni kubwa zaidi kwa sababu kile chombo ni chake. Hiki chombo ni chake, kama gazeti ni lake, kama redio ni yake, kama *television* ni yake, sasa Mheshimiwa Waziri hapa uta-*limit* vipi hizi *expenses* wakati mmoja ni mnyonge na tunataka kuweka ile *level* ya *play ground* kuwa sawasawa au angalau isipishane sana, ndio maana kubwa sana ya Muswada huu.

Sasa hapa ni vyema tuelezwe vyombo vya habari vya binafsi, vyama vingine vina *television*, vyama vingine vina redio, vyama vingine havina chochote, ni wanyonge mno. Sasa leo utafanya vipi katika Muswada huu kuviweka vyombo hivi ili navyo vionekane? Kwa sababu ikiwa mmoja saa zote yuko kwenye *television* anatangaziwa, mwingine hayuko, tayari hiyo hakuna *limitation of expenses* hapo. Sasa Mheshimiwa Waziri utufafanulie kipengele hiki utakifanya namna gani ili ipatikane haki sawa kwa wote. Isiwe mmoja yuko anatangazwa zaidi, mmoja hapati kutangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Ibara ya 30 ifafanuliwe kwa sababu Ofisa wa Tume kwa kitendo atakachokifanya awe hana kosa ikiwa amekifanya kwa *good faith*. Hii *good faith*, tafsiri yake ni pana, lakini *good faith* inaweza kuwa ni *bad faith* kwa mwingine. Nitoe mfano, ikiwa leo vyama vinataka kwenda kufanya kampeni kwenye kijiji fulani na vyama vitatu au vinne vikajitokeza kwa siku moja na kuna mnada, kwa hivyo kila chama kinataka kipate *coverage* siku ile kwenda kufanya kampeni katika kijiji kile; Afisa huyu kwa *good faith* iliyotamkwa hapa akavizuwia vyama viwili na pengine vilitangulia maombi, akakipa chama

kilicholeta ombi mwisho ili visigongane kule, amefanya kwa *good faith.* Lakini *good faith* hii kwangu mimi niliyepeleka ombi mwanzo kwenda kufanya kampeni kijiji kile na nikakataliwa akapewa mwingine, tayari ni *bad faith* kwangu. Sasa kipengele hiki kifafanuliwe, *good faith* hii kwa watu wengine ni *bad faith. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 28(3) ya toleo la zamani la Muswada huu kilitolewa kipengele ambacho kwa kweli ni kizuri ambacho sasa hivi kiko katika Ibara ya 29 na tukiangalia Jeshi la Polisi wakati wa kampeni, idadi ya Jeshi letu la Polisi hawawezi kufanya kazi zote zile, kwa hivyo, ilikuwa ni sahihi kutolewa kipengele kile walinzi binafsi wakaruhusiwa, kwa sababu kuna matukio sote tuna uzoefu. Hivi leo mimi nataka kurejesha fomu Tume ya Uchaguzi, na mnajua kuna matukio ambayo wengine wameshatekwa nyara; lakini leo na haiwezekani pengine Jeshi la Polisi lisiwe na nafasi ya kuweza kuja kunipa *coverage* mimi kurejesha fomu, watawapa *coverage* watu wangapi, wagombea wangapi katika nchi nzima? Kuanzia Madiwani, Wabunge, nani, ni *impossible.* Kwa hivyo, kile kipengele kilipoondolewa ikawa ni walinzi wa vyama sasa hivi wanaruhusiwa, mimi ninatoa hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache na kwa kujali wakati na hali halisi namalizia hapo. Lakini Ibara ya 10 ya Muswada huu ya uwezo wa Waziri mhusika, naomba ifafanuliwe na madaraka haya yasije yakatumiwa vibaya na hasa ukilinganisha na vyombo vya habari, uwiano uwepo. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH**: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mhesimiwa Philip Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge na watendaji wote waliosaidia katika kuandaa kwa hatua zote Muswada huu muhimu wa Gharama za Uchaguzi wa mwaka 2009.

Sheria hii ni nzuri sana hasa katika kuzingatia maadili ya matumizi ya fedha halali katika hatua za kuwapata viongozi wa kisiasa, sheria itadhibiti matumizi ya fedha chafu ambazo kwa njia moja ama nyingine fedha chafu zinaweza kuweka kiongozi ama viongozi wasio na sifa na hata wale wenye rekodi zisizofaa katika jamii kama vile wizi, ubadhirifu na fedha za umma, tapeli na kadhalika.

Mheshimiwa Niabu Spika, katika miaka ya hivi karibuni hasa ile ya 1990 sifa kubwa katika uongozi wa kisiasa imekuwa ni kwa yule mwenye nacho(fedha) ushindani ndani ya chaguzi umetilia uzito zaidi juu ya uwezo wa kifedha na sio sifa katika uongozi, jambo hili ni hatari sana kuendelea kuliacha hivi hivi kwani mara kadhaa tumejionea viongozi wa kisiasa wale wenye kutumia kipato cha fedha walizonazo kutotekeleza majukumu ya kisiasa kupitia uwakilishi wa wananchi nafasi wanapoipata mara nyingi hurejea katika shughuli zao walizozoea na kuwaacha wananchi bila uwakilishi. Sheria hii itadhibiti rushwa ya uchaguzi na hivyo kutoa uwanja sawa katika ushindani wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 10(1) kinazungumzia viwango vinavyotakiwa kutumika katika gharama za uchaguzi kifungu hiki kinampa uwezo Waziri kutangaza viwango vya fedha

zitakazotumika kulingana na ukubwa wa jimbo, aina ya wagombea, idadi ya watu na miundombinu na mawasiliano yaliyopo.

Pamoja na uamuzi mzuri wa sheria ningeshauri katika kipengele hiki sheria ingezingatia juu ya hali ya kipato cha wananchi wa jimbo husika mfano mzuri matumizi ya jimbo la Ilala linatofautiana na jimbo la Iramba Magharibi kwa hali ya kipato hivyo kigezo cha ukubwa, idadi ya watu muindombinu na kadhalika peke yake havitoshelezi kwani yawezekana kabisa matumizi ya gharama ya uchaguzi yakawa juu kwa eneo la watu wenye kipato kidogo (maskini).

Kadhalika sheria ingeona umuhimu wa kufanya udhibiti na kuangalia mwenendo mzima wa vyama hasa kupitia mapendekezo ya wagombea (kura ya maoni) kama kutakuwepo na vitendo vya dhahiri vinavyohusisha rushwa basi mgombea aliyehusishwa na rushwa aondolewe katika orodha ya kuwa mgombea anayekiwakilisha chama lakini pia hatua  za kisheria dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufunguliwa mashtaka ya jinai, mahakamani ya kutoa rushwa.

Wagombea lazima wachunguzwe kwa umakini, vyanzo vyao vya mapato na lazima awe ametangaza mali alizonazo na namna alikozipata ili kuepuka wagombea wezi na wafujaji wa mali za umma. Ili kuepusha migongano ya kufunika kesi nyingi mara baada ya uchaguzi kumalizika kwa kisingizio cha makosa yatakayohusishwa na sheria hii ambayo yanaweza kuwa ya   kutunga basi Sheria ya Uchaguzi *(Electoral Laws)* ifanyiwe marekebisho katika eneo la *security costs* iwe ni ile ya kiwango kilichotumika kilichoidhinishwa na Waziri kwa mgombea aliyeshinda, ile *security costs* ya shilingi 5,000,000/= ni ndogo na haiendani na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu spika, naunga mkono sheria hii.

**MHE.  DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa mwaka 2009. Nawapongeza Waziri Mheshimiwa Philip Marmo, pamoja na wote walioshirki kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Muswada huu utaondoa mianya ya rushwa kama ilivyokuwa inaonekana, matajiri wengi waliopata nafasi kubwa ya kushinda chaguzi nyingi sasa hata mgombea ambaye siyo tajiri ataweza kuchaguliwa na wapiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu utaleta tija endapo kutakuwa na usimamizi wa karibu tena ulio wazi, naomba sheria hii iangalie vipengele vya kuwabana viongozi wa vyama kwani wanaweza wakaanza kujinufaisha wenyewe badala ya kusaidia mgombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni vyema fedha hizi atakazoeleza mgombea ni bora zikaendelea kuwa chini yake na siyo kuziwasilisha kwa kiongozi wa kampeni zake. Hii itasaidia mgombea kutokuibiwa fedha zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono sana Muswada huu ili uweze kudhibiti mianya ya rushwa ili tupate wagombea ambao watashinda kihalali na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kutamka kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia nikiwa na matumaini kuwa Sheria hii Serikali itaziba kabisa nafasi ya fedha kutumika vibaya na kuwepo usiri wa fedha za mgombea.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa tulilonalo siyo wananchi bali ni mfumo ambao ulianza polepole na sasa umezoeleka hasa pale tulipoacha dhana ya kufanya vyama vya siasa kutokuwa ni vyama vya wafanyakazi na wakulima. Walipoingia wafanyabiashara, suala la uzalendo kama kigezo cha kuongoza nchi au jamii kikaanza kutoweka. Fedha zikaanza kutumika kama kigezo cha kuwa kiongozi, kiasi cha kuwaacha baadhi ya wananchi ambao ni maskini lakini mahiri kwa kuongozi kuachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada umekuja wakati muafaka ingawa temechelewa, lakini ni vizuri kuwa umeanza kwani tulifika wakati uongozi ulibidi ununuliwe, mwenye fedha alikuwa ndiye mwenye nafasi kubwa ya kuwa kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo langu ni kuwa baada ya Sheria hii kupita kutakuwa na hali ya kutoridhika kwa watu waliotaka uongozi kwa njia ya fedha. Serikali lazima iwe makini katika matukio yatakayoripotiwa na watu hao kwani watatumia njia nyingine za kuwarubuni washindi halali. Kutakuwa na fitna, kuwindana hata kuwarubuni wateuliwa wa haki hasa wakati wa kura za maoni .

Mheshimiwa Naibu Spika, naupongeza Muswada kwa kuweka udhibiti mkubwa ndani ya vyama vya siasa kuliko ilivyokuwa awali kwa kumpa msajili wa vyama *role* kubwa kwa kudhibiti wagombea. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. GIDEON A. CHEYO**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumpongeza mtoa hoja kwa kuwasilisha Muswada huu baada ya mchakato mrefu na mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja wakati muafaka ambapo Taifa letu liko katika jitihada za kupiga vita vitendo vyote vya udanganyifu na rushwa katika chaguzi mbalimbali zinazofanyika ndani ya vyama vya siasa na Serikali. Pamoja na kuunga mkono Muswada huu, hoja ipo kuzingatia ushauri ufuatao:-

Kwanza kwa kuwa masharti ya kutoa taarifa za mapato na matumizi kwa wagombea na vyama vya siasa wakati wa mchakato wa kura za maoni na kampeni za uchagizi ni utamaduni mpya kwa kuwa na kipindi maalum cha kutoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya Muswada huu. Bila elimu ya kutosha kwa wananchi huenda tukawa na pingamizi nyingi na kuathiri ratiba ya uchaguzi. Kazi hii ya kuelimisha umma ifanywe na Serikali pamoja na vyama vya siasa.

Pili, Muswada unaweka masharti ambayo yanapaswa kusimamiwa na msajili wa vyama vya siasa, Tume ya Taifa ya uchaguzi na kadhalika. Ni muhimu vyombo hivi vikawezeshwa kwa hali na mali ili viweze kusimamia na kutekeleza majukumu yao hadi ngazi zote za uchaguzi. Kwa hiyo, viwe na watumishi wa kutosha na Bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kama Taifa tuwe na mipango ya muda mrefu ya kuiwezesha Serikali kubeba gharama muhimu za uchaguzi. Vyama vya siasa na wagombea wabakie kugharimia ushindani baina ya vyama kwa chaguzi za Serikali za Mitaa na uchaguzi wa Serikali Kuu, ugharimiwe na Serikali kwa ujumla.

Nne, kwa maoni yangu suluhisho la kudumu kuondokana na vitendo vya udanganyifu na rushwa, ni kwa kila mmoja wetu kuamua na kukataa kushiriki katika vitendo hivyo viovu. Uadilifu na uaminifu kwa misingi ya dini zetu na utamaduni asilia vipewe kipaumbele katika kuelimisha na kukumbushana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo mfupi, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. SAID A. ARFI**: Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni wa lazima sana katika kujenga Taifa ambalo lina viongozi waadilifu wanaochaguliwa bila ghiliba, hila, rushwa na kadhalika, hatimaye chaguzi zetu hazitakuwa minada ya kura na mwenye fedha ndiye mshindi.

Hofu yangu Muswada huu unataka kutatua matatizo yote kwa wakati mmoja bila ya kuangalia mazingira ya nchi yetu, utekelezaji wa Muswada huu utakua ni mgumu. Tuangalie yapi ya lazima sasa, muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangu ya kwanza, rushwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu, lakini bila kujenga uwezo ni kujidanganya, ni lazima kwanza kuwepo nan mkakati wa kujenga uwezo wa taasisi zetu na sheria mbalimbali ili kuwezesha sheria hii iwe na manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema ni lazima pia kupitia sheria mbalimbali ili kurahisisha utekelezaji wa sheria kwa kuangalia Sheria za Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi, Msajili wa Vyama, Tume ya Maadili, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa namna moja vyombo hivi vinajihusisha na demokrasia, uongozi na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa ni kuboresha na kujenga demokrasia ya kweli chini ya msingi inayotoa haki na usawa. Lakini pia haki ya misingi ya Kikatiba ya mtu kuchagua au kuchaguliwa lakini Muswada huu haukuzingatia haki hii ya Kikatiba, Muswada umejikita katika vyama na wagombea wa vyama vya siasa hakuna nafasi ya mgombea binafsi katika Muswada huu, hata hivyo jopo la Majaji wa Mahakama Kuu wanapitia shauri la mgombea binafsi hivyo basi itakapokubalika katika uchaguzi wa mwaka 2010, ina maana sheria hii itapitiwa katika muda mfupi ujao au itasitishwa, nitapenda kupata maelezo juu ya nukta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kichekesho katika nchi inayojenga demokrasia kuwa na mgombea amepita bila kupingwa, bila kutazama mazingira halisi ya kufikia hali hiyo, ni vyema basi wagombea wa aina hiyo wapigiwe kura ya ndiyo na hapana na ili awe mshindi ni lazima apate zaidi ya 50%, jambo hili si geni hata wakati wa awamu ya kwanza, mgombea Uraisi alikua pekee lakini alipigiwa kura za ndio na hapana. Wakati mwingine tunapata viongozi kupita bila kupingwa kwa hilo na wananchi hawana namna yoyote ya kupinga maamuzi ambayo pengine hayawanufaishi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa pia kujua mpango madhubuti wa Serikali wa kuhakikisha Tume ya Uchaguzi ifanye kazi kama Tume badala ya kutumia mawakala ambao ni watumishi na makada wa chama kinachotawala, yapo matatizo mengi mno ambayo yanatosha kuwa fundisho kutokana na usimamizi wa watumishi wa TAMISEMI, Ofisi za Wakurugenzi, Watendaji Kata na Vijiji wanawajibika kwa mwajiri wao, na sio Tume ni lazima tuwe na Tume ambayo ni taasisi kama vile Ghana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika Ofisi ya Msajili itafanyaje kazi katika majimbo yote naomba kupata maelezo. Ni Wakurugenzi ndio watakua wawakilishi wa Tume ya Uchaguzi na wakati huko huo Msajili wa Vyama, naomba ufafanuzi nani atawakilisha Tume katika jimbo na Msajili anawakilishwa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kusema kwamba Muswada mzuri lakini umeletwa bila maandalizi ya kutosha na kupata maoni bora zaidi kwa mustakabali wa nchi hii na kuimarisha na kujenga demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukura sana.

**MHE. MARGARET S. SITTA**: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa kazi kubwa ya kuandaa Muswada huu. Bora tuanze, mapungufu yatakayojitokeza yatarekebishwa. Hongera sana.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa kuleta Muswada sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ya jumla ni kuwa Muswada huu unampa msajili wa vyama madaraka ambayo kwa kawaida hapewi msajili wetu ni tofauti ya wasajili wengine hata hapa Barani Afrika. Kwa mfano, msajili wa Zimbabwe amepewa madaraka ya kusajili chaguzi, vizazi, vifo, masuala ya uchumi na kadhalika. Katika sheria hii msajili wa vyama anapewa baadhi ya majukumu ambayo kwa kawaida ni ya Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Muswada huu, mambo ya kuainishwa ambayo huonekana katika Sehemu ya Kwanza yamekuwa katika sehemu za baadaye, tazama Ibara12(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni katika vifungu vingine ni kuwa Ibara ya 11(5) haina msingi, kwani si kawaida katika chaguzi kutishiwa wanaomchangia mgombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12(3) inaruhusu misaada itakayotolewa kabla ya siku 90 katika chaguzi kuu na siku 30 katika chaguzi ndogo. Si sahihi kwani fedha haramu zinaweza kutolewa kwa wingi tu kabla ya vipindi hivyo.

Pia Ibara ya 13(2) inampa Waziri madaraka ya kuamua viwango vya misaada kwa wagombea, nashauri kuwa Waziri afanye hivyo kwa kushauriana na vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 inaelekeza matumizi ya wagombea yawe na ankra na risiti zinazoelezea vilivyonunuliwa, hili halitekelezeki. Ili mradi mgombea amewasilisha chama ni fedha anayotegemea kuitumia.

Katika Ibara ya 17(3) inaelekeza Bodi za wadhamini wawasilishe kwa msajili matumizi yote na viwango vilivyotengwa kila mgombea wa kila chama. Sioni ulazima wake, kwa kuwa msajili anapewa madaraka ya kukagua matumizi ya kila chama na wagombea. Basi pale penye mashaka, wakaguzi watumwe wakafanye kazi yao.

Ibara ya 18(4) inatoa adhabu kwa chama kisichowasilisha taarifa ya ukaguzi. Taarifa ya matumizi sawa, lakini taarifa ya uchaguzi isitegemewe kupatikana kwa urahisi, kwani siamini kama Mkaguzi Mkuu wa Serikali ataweza kukagua matumizi ya vyama vyote sambamba na shughuli zake za kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 21(1) (a) ifanyiwe marekebisho, kwani hapana mtu atakaekiri kuwa alichokitoa ni kwa ajili ya kushawishi apigiwe kura na Ibara ya 21(i)(b) inatoa adhabu kwa mgombea kwa makosa ya chama chake au mwakilishi *(agent)* wake. Si sahihi na nashauri ibara hii ifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara za 22 na 23 zifutwe kwa sababu zifuatazo; kwanza kutoa chakula na vinywaji kwa wanaokusaidia siyo hongo bali mila ya Kiafrika, pia mara nyingi Serikali haina uwezo wa kusafirisha viongozi na wapiga kura na kule vijijini baadhi ya vituo vya kupigia kura viko mbali na wananchi. Nashauri kuwa mgombea anaetaka kusaidia ipitishwe msaada wake kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri kwenye Sehemu ya Nne ya Muswada inayohusu Makosa ya Adhabu nashauri ziongezwe ibara zitakazokataza majungu na adhabu za makosa hayo kwa wote watakaowasingizia wenzi wao makosa ambayo hayakutendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono. Ahsante sana.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu sasa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zangu ni kama ifuatavyo, tunakubali kuwa kila siku kuna mapambano kati ya demokrasia na nguvu za fedha, lazima kukomesha fedha za makampuni makubwa wasije wakatumia fedha zao kwa kuwanunulia wagombea wetu au wakanunua vyama vya wagombea wetu au wakanunua vyama vya siasa na wakavihodhi. Lazima Sheira hii iwalinde wagombea wetu na vyama vya siasa kutokana na janga hilo la kufanya ufisadi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe fedha za kutosha kuwapa wagombea kwa kupitisha vyama vyao. Lakini vyama viwape fedha za gharama za uchaguzi wagombea, hatua hiii itawanusuru wagombea wetu kutoka katika midomo ya mafisadi, vyama vya siasa vigharimie matumizi ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section 10(i)* katika kupanga ukomo wa gharama za uchaguzi ashirikiane na vyama vya siasa katika kupanga ukomo wa matumizi ya uchaguzi. Kama haiwezekani basi napendekeza ukomo wa gharama za uchaguzi usiwekwe katika *subsidiary legislations* ila kiwekwe katika sheria yenyewe.

*Section 24(2)* naomba kwa vile inawezekana kuwa mtu mbaya naweza kujiita *agent* wa mgombea na wala si *agent* wa kweli, tuwe na namna fulani ya kutambulika kwa *agent* wa mgombea. *Identification of an agent* kwa maana ya kujiandikisha na kupata kitambulusho cha *agent* wa mgombea. *Agent* lazima awe amekubalika na chama cha siasa na mgombea mwenyewe. Hatua hii itawazuia ma-*agent* ambao si ma-*agent* ila ni makanjanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni *weak enforcement of provisions of the act,* Tanzania ina tatizo kubwa la kushindwa kuhakikisha kuwa sheira zilizotolewa na Bunge hili linaachwa bila kufuatwa *(in ability to enforce)* kuna tabia iliyojengeka katika nchi yetu kuwa hatujali kufuata na kufuatilia maudhui ya sheria  zetu. Nomba sana sheria hii ipate heshima ya kufuatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujua ni lini Muswada huu utakapopitishwa na kuwa Sheria utatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutoa tatizo la rushwa wakati wa uchaguzi ni vyema wananchi waupate na wauelewe hivyo ukiwa katika lugha ya Kiswahili utasaidia kuleta tija kwa maana hakutokuwa na rushwa au kutoa kisingizio cha kutoifahamu sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali iko tayari kutoa semina kwa Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji ambao tayari wako madarakani ili na wao waweze kutoa elimu hiyo kwa wananchi wao? Naomba suala la elimu kwa wananchi lipewe kipaumbele cha haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, sheria hii ikisimamiwa nina hakika italeta mabadiliko. Naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wote waliochangia katika kuboresha Muswada huu, hususani naipongeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ya kuupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo machache ambayo nafikiri itakuwa vizuri kupatazama kwa umakini mkubwa zaidi. La kwanza linahusu nafasi ya msajili wa vyama vya siasa katika kudhibiti matumizi ya fedha kwenye chaguzi. Je, itakuwaje iwapo uamuzi wa mahakama juu ya wagombea binafsi utatekelezwa?

Pili majukumu ya msajili wa vyama vya siasa ni kusajili vyama vya siasa na kuvisimamia. Haikukusudiwa kumfanya msajili wa vyama vya siasa kuwa msimamizi wa chaguzi. Inabidi suala hili litazamwe upya na jukumu hili litolewe kwa chombo kinachohusika zaidi na masuala ya uchaguzi.

Kwa mfano, Tume ya Uchaguzi inaweza kuunda kitengo maalumu kwa ajili hii, vinginevyo kiundwe chombo kipya kitakachopewa jukumu hili na kiwe na muundo wa kukiwezesha kufanya kazi zake na kutoa haki kwa vyama vya siasa, wagombea na walalamikaji.

Muswada unaweka utaratibu rahisi mno wa kuwandoa wagombea *(disqualification).* Utaratibu ni lazima uzingatie misingi ya haki. Kwanza uchunguzi wa tuhuma ufanywe, mtahiniwa apewe nafasi ya kujitetea na kusikilizwa na jopo la watu wenye sifa za kuliwezesha kutoa haki *this is a serious matter which must be treated seriously,* sio busara mtu mmoja kupewa mamlaka ya kumfuta mgombea bila hata kumsikiliza.

Aidha, wagombea na watu, wananchi wa Taifa hili. Chama kisikatazwe kusimamisha mgombea kwenye eneo lolote la uchaguzi kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwanyima wananchi wasiokuwa na hatia haki yao ya kugombea kuchaguliwa. Chini ya *Prohibited Practices (Part V)* inazungumzia mtu yeyote, mwenyewe, kwa kutumia watu wengine kwa niaba yake anatoa rushwa atakuwa amefanya kosa. Inawezekana watu wengi wakifanya mambo yanawezekana kuwa miongoni mwa yaliyokatazwa bila mgombea au chama chake kujua.

Aidha, mtu au watu wanaoweza kujitolea kufanya vitendo vilivyokatazwa kwa lengo la kumharibia mgombea. Inabidi Muswada uongeze *with the knowledge or permission of the candidate* watu wowote wanaofanya vitendo vilivyokatazwa wachukuliwe hatua za kisheria na wakipatikana na hatia waadhibiwe.

Mwisho, suala la upatikanaji wa fedha za uchaguzi ni sharti litazamwe kwa uangalifu. Wagombea huwa na watu wanaowaunga mkono (mashabiki). Mashabiki hao huwa tayari kumuunga mkono mgombea wao kwa hali na mali. Mashabiki hao mara nyingi hawako tayari kupitisha misaada yao kwenye vyama vya siasa. Misaada yao ni kwa mtu, sio kwa chama au taasisi nyingine yoyote. Aidha, mara nyingi vyama vya siasa havina uwezo wa kugharamia chaguzi na hutegemea wagombea wajigharamie na hata kukisaidia chama kugharimia baadhi ya shughuli zake, kwa mfano, gharama za usafiri, makaratasi na kadhalika, wanaompa msaada mgombea watambuliwe na taarifa za mapato zionyeshe michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuona umuhimu wa kuweka sheria hii ili iwezeshe kuona kwa uwazi wa fedha ya uchaguzi.

Swali langu ni juu ya usiri wa ushindani. Huu utoaji wa taarifa usipoangaliwa unaweza pia kutoa fursa kwa mshindani kufahamu *weakness* za mgombea mwenzake. Mfano kwa mgombea kama ana shilingi milioni tano, lakini kabla hajataja wazi anaogopwa kidogo, lakini

akishataja, mwenzake anasema ngoja niongeze kidogo tu nitamshinda. Hivyo ni vyema *disclosure* ifanyike kwa utaratibu mzuri kama ilivyo utoaji wa taarifa za mali za viongozi kwenye Tume ya Maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kushauri ni vyema muda rasmi wa kuanza kupita kwenye maeneo ujulikane angalau miezi minne kabla, bila kufanya hivyo Muswada huu utakuwa hauna maana, watu wafanye hayo matumizi mabaya ya fedha kabla ya muda uliotajwa katika Muswada huu ama sivyo itakuwa imevuruga kazi za viongozi waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kwa kuwa unakusudiwa kutekelezwa kuanzia uchaguzi ujao ni vyema basi kwanza utafsiriwe kwenye lugha ya Kiswahili na pia elimu ya kina itolewe kwa wananchi na wadau wote kwa ujumla ili utekelezaji uwe rahisi. Lakini kama ilivyo ada, msisitizo mkuu na mhimili mkuu wa Muswada huu ni vyama vyenyewe na Chama cha Mapinduzi kwa sasa ambacho ndicho kina sehemu kubwa ya wapenzi nchini, na hivyo kushika eneo kubwa la Tanzania, ni vyema ikawa mfano katika utekelezaji wa sheria hii itakapokuwa tayari katika kuunga mkono Serikali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unailetea Tanzania heshima kubwa katika juhudi za kuleta demokrasia na kuboresha utawala pamoja na kukuza maadili nchini. Naamini Watanzania wote tunaunga mkono Muswada huu, na ninaunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mzuri kama utazingatia demokrasia na uwazi. Ni wazi viongozi wengi wamepata madaraka kwa kununua wananchi kutokana ama kwa kutokuwa na sheria au utekelezaji na uadilifu. Katika kifungu cha nne, msajili wa vyama vya siasa ambaye kimsingi ni mlezi wa vyama bado anakuwa tena mdhibiti wa vyama wakati wa uchaguzi. Hili ni kosa na si utawala bora wala utaratibu. Kifungu cha 24(i) kila chama kitamaliza mchakato wa uteuzi siku 30 kabla ya uteuzi hili ni tatizo kwani kila chama kuna utaratibu wa uteuzi wa siku tofauti hivyo kufanya uteuzi kufanyika siku moja ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu 12(i) kumekuwa na *restriction* ya fedha kutoka nje. Jambo hili si baya sana hasa tukiangalia malengo yake lakini cha msingi ni dhamira ya *restriction* hiyo. Kwa nini panakuwa na muda wa siku 90? Yaani ukiingiza fedha hizo ndani ya siku 90 kabla ni sawa hata kama fedha hizo ni chafu! Na ni kwa nini hakuna kipengele chochote kinachoharamisha matumizi ya fedha za ndani zilizopatikana kiharamia au wizi? Fedha zinazotokana na dawa za kulevya na fedha zinazotokana na Mashirika ya Kimataifa yaliyo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wowote ule ili uwe huru na uwazi na ukweli, mawakala ni wa muhimu sana na ushindi wowote ule unapatikana katika vituo vya kura yaani *polling station.* Ni wazi kuwa wizi wa kura umekuwa ukifanywa vituoni na hivyo kupata viongozi ambao sio waadilifu. Hivyo ni lazima Serikali igharamie mawakala hasa ikizingatiwa kuwa vyama vingi au vyote vya upinzani havina uwezo wa kuwagharamia mawakala na hivyo tunaamini bila hivyo wagombea wengi watashinda kwa hila na wale walipaswa kushinda kihalali kushindwa. Kama kweli nia ni kuboresha na kudhibiti fedha zinazotumika kununua wapigakura, basi lazima hili la mawakala lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria bila mikakati madhubuti haina msingi wala mashiko. Ni vyema basi pakawa na utekelezaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, ni vyema basi Muswada huu uyazingatie maoni ya Wabunge hususan yale ya Kambi ya Upinzani ambayo yataboresha sana Muswada huu.

**MHE. GODFERY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu, nadhani utasaidia kuleta nidhamu ya aina fulani kwa wagombea. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Muswada huu utawalenga vipi wale walioanza kampeni mapema, ni dhahiri kwamba Muswada utasitishwa na Bunge lako Tukufu ili uwe sheria na hivyo kwanza kutumika mwaka huu wa uchaguzi sasa na tena kujua Muswada huu utakapokuwa sheria utawahusu pia wale walioanza kampeni mapema. Ushauri wangu mimi ni kwamba sheria ianza kutumika *retrospectively* mwaka 2009. Kwa sababu hicho ndicho kipindi ambacho kampeni chafu, zisizo rasmi zilianza. Vinginevyo viongozi hasa Wabunge na Madiwani waliopo madarakani hawatatendewa haki.

Kuhusu Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa *(PCCB)* ni chombo/Taasisi ambacho kimeanzishwa kisheria ili kupambana na kuzuia rushwa. Jambo linalonishangaza ni kwamba wakati wa chaguzi mbalimbali sioni kama *PCCB* inafanya kazi zake vizuri. Wasiwasi wangu ni kwamba kama *PCCB* imeshindwa kufanya kazi vizuri huko nyuma, tuna hakika gani sasa kwamba watafanyakazi vizuri kwa kupitia/kutumia sheria hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaona sehemu yeyote kwenye Muswada huu kama sasa chini ya sheria hii *PCCB* watafanya kazi vizuri. Wasiwasi wangu watu ni walewale, je, kinachobadilika ni sheria pekee yake na kwa kumrundikia msajili wa vyama vya siasa madaraka makubwa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezo *(capacity)*, je, Serikali kwa kupita msajili wa vyama vya siasa wana uwezo wa kusimamia sheria hii nchi nzima? Hapa nina wasiwasi mkubwa naomba Serikali itoe maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga hoja mkono.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyombo vilivyopewa jukumu la kusimamia rushwa na matumizi ya fedha chafu, vyombo vya Serikali vilivyopewa jukumu la kusimamia rafu zinazofanywa katika majimbo havijawezeshwa kuwa na nyenzo vya kutosha kusimamia rafu hizo pande zote za Tanzania na maeneo yote ya majimbo yetu hivyo kutoa mwanya wa rushwa kubwa kufanyika katika majimbo ya uchaguzi. Serikali itoe maelekezo ni nani atakayesimamia rafu hizi hadi kata kwa madiwani na jimbo kwa Wabunge.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni wa kihistoria. Unajenga msingi imara wa uhai wa nchi au Taifa letu. Matumizi yasiyo halali ya

fedha katika uchaguzi ni hatari hata kwa usalama wa Taifa. Ni saratani ambayo pole pole inaua Taifa. Nampongeza mtoa hoja, nami niorodheshwe kama mmoja wa waliounga mkono hoja hii ya kihistoria.
Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba niwe miongoni mwa wachangiaji katika Muswada huu, muhimu.

Napenda kuwapongeza Waziri mwenye dhamana kwa niaba ya Serikali ili kupunguza tabia chafu zinazotumika wakati wa mchakato wa uchaguzi. Kwa sababu wapo watu wenye fedha nyingi sana na haingii kwenye kugombea ili wawakilishe wananchi waliomchagua na Watanzania wote bali ni kulinda mali zao na hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu hakuna mahali panaonyesha kuwa wenye nia ya kugombea watatangaza nia yao na kugombea kuanzia lini? Kwa mfano hivi sasa wapo watu wameanza kuzunguka kwenye majimbo kutangaza nia wakati kipindi cha miaka mitano cha utekelezaji wa Ilani bado haujaisha je hiyo si fujo? Ni vizuri wenye kutangaza nia wasuburi mpaka mabaraza ya Madiwani na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamevunjwa ili kuondoa uvunjifu wa sheria pamoja na kuwakosesha amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweka usawa kwa wagombea wote basi Serikali ingeweka usawa wa kifedha yaani kuanzia shilingi kiasi fulani mpaka kiasi fulani lakini kusema kuwa kila mtu atangaze fedha atakazotumia, kutakuwa hakuna uwiano kati ya mgombea mmoja au mwingine. Hili ni jambo la msingi sana katika kuleta demokrasia katika nchi yetu, kwa kufanya hivyo tutapata viongozi halisi ambao watapewa ridhaa na wananchi bila vishawishi vikubwa.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, utaratibu na Bunge Mheshimiwa Philip Marmo, na wasaidizi wake wote katika kuuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Muswada huu, pamoja na ukweli kwamba umekuja kwa kuchelewa sana hadi kusababisha wapiga kura hasa kura za maoni katika vyama vya, siasa kujiona kuwa wanapaswa kupewa fedha, wanayodai ni ahsante ya kuwapigia kura wagombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mapungufu makubwa ambayo huwachochea wagombea kutoa fedha (rushwa) kwa wapiga kura ni kutokuwepo kwa wapelelezi wa kutosha na makini, katika kila jimbo wenye uwezo wa kupata taarifa na ushahidi wa vitendo au wa mazingira, unaomruhusu mgombea mtarajiwa au aliye madarakani anayetoa rushwa kwa watu au viongozi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu huu, kila mgombea anajua udhaifu wa mamlaka ya vyama kudhibiti utoaji wa rushwa, kwa kuwa ni mara chache sana watoa rushwa wamebainika kukamatwa. Kutokana na hali hii, kila mgombea huwatilia mashaka kuwa wagombea wenzake watakuwa wanatoa rushwa kwa hali hii, naye atajiona analazimika atoe rushwa ili wenzake wasimpiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kudhibiti ipasavyo utoaji rushwa, wagombea na kupunguza matumizi makubwa ya fedha kuliko inavyostahili Serikali ichukue hatua za makusudi za kuwateua wapelelezi wengi walioandaliwa kwa kila jimbo, nyakati za uchaguzi ili kwa muda wote wawe wanapeleleza nyendo za wagombea wote na kubaini vitendo au nyendo zinazoleta hisia za wazi zinazoonyesha dalili za wazi za utoaji rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa ili wagombea watoe taarifa ambazo ni *consistent* kwa vipengele vyote vya gharama za uchaguzi, Serikali iandae *forms* ambazo ziwe *standard* kwa kutumika kwa kujazwa na vyama na wagombea wote; mfano kama fomu zinazojazwa viongozi wanapotamka mali walizonazo. Pia semina maalum ya kuwaelekeza Wabunge wote namna ya kukagua vipengele vinavyotambulika kama ni gharama za uchaguzi na vile visivyokubalika. Hii itasaidia kulinganisha vizuri zaidi gharama na vipengele vitakavyojazwa na wagombea mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwa kuwa ujazaji gharama katika fomu za gharama za uchaguzi utafanyika kwa mara ya kwanza ni budi itegemewe fomu za wagombea wengi zitakuwa na makosa yasighamiriwe. Kwa hiyo, pengine Serikali kwa kushirikiana na vyama vya siasa vingekaa pamoja na kukadiria gharama za makisio kwa kila jimbo kwa vipengele mbalimbali ili uwe ni mwongozo wa kufuata katika kujaza fomu za gharama mbalimbali za uchaguzi, hata kama gharama halisi zitazidi au zitapungua kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu huu, narudia kutamka kuwa naunga mkono hoja hii.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu na nachangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni matumizi ya Kiswahili fasaha kwa kuwa wadau wengi ni wananchi wa kawaida napendekeza hii sheria itakapoanza kutumika itafsiriwe lugha rahisi ya Kiswahili na Tume ya Uchaguzi ipeleke sheria hii kwa wananchi ili waweze kufahamika na kutendea kazi. Pili, kazi za msajili wa vyama vya siasa, naona kazi yake hii ya kusimamia na kutawala matumizi ya fedha ya uchaguzi ni kazi kubwa kwake na pia kuchunguza ninaona ni vizuri vyombo vinavyohusika vifanye kazi hiyo mfano, Tume ya Uchaguzi, *Auditor General* na *PCCB* ilifaa sana wafanye kazi hiyo kwa vile hao ndio kazi yao ya kuchunguza fedha za halali au chafu.

Msajili wa vyama kazi yake kubwa ni kusimamia na kutawala vyama alivyosajili na kusikiliza migogoro au mafanikio ya vyama hivyo, siyo kufanya kazi za taaluma kama za uhasibu, uchunguzi na kadhalika. Pia msajili wa vyama atakuwa na kazi kubwa ya kuajiri watumishi na kuongeza idadi ya Bajeti kwa kila jimbo la uchaguzi wakati ingefanywa na vyombo husika kama polisi, Usalama wa Taifa, Tume ya Uchaguzi na TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tafsiri ya kipindi cha kampeni, sheria inasema kuanzia siku ya kuteuliwa *(nomination day)* hadi siku ya uchaguzi inayofuata. Katika hali halisi hasa upande wa Rais, Ubunge na Udiwani, utaona baadhi ya wagombea wakishindwa au wengine

wanatarajia kuanza kufanya kampeni za kuvuruga yule aliyeshinda kwa kufanya kampeni kabla ya muda wake mfano kupitisha kwenye makanisa au taasisi za dini na kutoa fedha, michango na misaada mbalimbali kwa lengo kushawishi watu waje kumpigia siku ya uchaguzi na fedha hizi zinakuwa zinatokana na wizi Serikalini au mikopo. Naona sheria ingeangalia kuanzia muda wowote ambapo mgombea anatoa fedha au michango kinyume cha taratibu za chama au sheria.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa haitamalizwa na sheria wala muundo, wagombea na wananchi wawe na dhamira ya kupiga vita rushwa, elimu itolewe. Naunga hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ingawa ningependekeza marekebisho kuwa madaraka na kazi mpya za msajili wa vyama kukagua hesabu za mapato na matumizi ya fedha wakati wa uchaguzi. Kazi hiyo ya mambo ya fedha iende kwenye Tume ya Uchaguzi na *CAG.* Msajili aendelee katika zoezi la kuandikisha.

Pia Sheria hii iambatane kwa pamoja na ile ya TAKUKURU kupambana kwa dhati na rushwa hasa ndani ya vyama. Muswada ujizike kataka chaguzi za kura za maoni. Pesa inatumika zaidi wakati wa uchaguzi ndani ya vyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya wakala anavyotambulika kisheria hasa anapotoa kwa niaba ya mgombea. Kifungu cha 21 (i)(a) – (c) kinamweka wakala bila kuweka namna atakavyojulikana ametumwa na mgombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya kutosha kuelimisha umma kuhusiana na maandalizi ya wananchi kwa kufanya semina/kongamano/mihadhara kwa wananchi. Sheria itangazwe na iwe imechapishwa kwa kiswahili mapema na kanuni zitungwe mapema.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 21(i) (a) – (b) ni vyema sheria itamke wazi kuwa wagombea uchaguzi wawasilishe orodha ya mawakala wao kabla ya uchaguzi ili kuepusha uwezekano wa kufanyiwa vitendo viovu na washindani wengine kwa kutumia watu wengine kwa lengo la kuwapotezea sifa za kugombea.

Kuhusu kifungu (c) – (b) ahadi *(promises)*huwezi kuepuka kutoa ahadi wakati wa kampeni watu watapenda kufahamu ni mabadiliko yapi utakayoyafanya kama utachaguliwa. Kifungu cha 21(2) utetezi wa mtuhumiwa utakubalika kwa urahisi endapo atakuwa amewasilisha orodha ya mawakala wake kabla na wakati wa kampeni sheria iweke ama iwatake wagombea kuwasilisha majina ya mawakala na wasaidizi wake.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kurekebisha sheria mara kwa mara ni jambo jema kwa kuwa mambo yanabadilika kuendana na wakati. Chaguzi za miaka kumi iliyopita siyo sawa na chaguzi za leo, ama za miaka kumi ijayo.

Naomba moja kwa moja nizungumzie upatikanaji wa Wabunge wa Viti Maalum, kwa kuwa sheria hii inagusia kipengele hiki. Naomba sambamba na kuweka taratibu za kuwapata Wabunge wa Viti Maalum, sheria iweke bayana pia mipaka yao ya utendaji kazi wao.

Kuna *clashes* nyingi sana baina ya Wabunge wa Viti Maalum kwa viti maalumu, na baina ya viti maalumu na Wabunge wa majimbo kwa kuwa sheria haiweki bayana mipaka ya utekelezaji majukumu yao na kwa kuwa maeneo ya kutekeleza ilani ya uchaguzi ni yaleyale, tunashirikiana na watu (wapiga kura) ni wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sheria hii ikaweka baya mipaka ya kila mmoja, ama uhalali wa kufanya kazi katika majimbo bila hisia potofu. Sheria irekebishwe kuweka wazi mahusianao ya Wabunge watatu katika Wilaya moja (V/M 2 na Jimbo 1) Wabunge wa Viti Maalum, kwa baadhi ya maeneo, hawana *support* kabisa ya Wabunge wa majimbo. Zaidi sana atakwamishwa asiweze kutembea na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Niabu Spika, hata likiwa jambo zuri kabisa lililogusa maisha ya wananchi wengi, bado haliwezi kutolewa taarifa ipasavyo kwenye vyombo husika kwa kuwa ni juhudi za Mbunge wa Viti Vaalum. Taarifa hii ipelekwe tu UWT. Hii mimi naona siyo sahihi. Juhudi za Wabunge wote zitajwe katika taarifa za Wilaya na Mikoa bila ubaguzi, sheria hii iweke wazi suala hili.

Pili, sheria pia iweke bayana ushiriki wa Wabunge wa Viti Maalum katika vikao vya Halmashauri kwa mfano baadhi ya Wabunge wa Viti Maalum wanaambiwa siyo Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri au Kamati za Ukimwi *(CMAG)* pia hili si sawasawa kabisa. Sheria iweke wazi ili kuepuka uwakilishi mzuri kwenye Halmashauri. Mbunge wa Viti Maalum ni mwakilishi wa wanawake na hivyo ni lazima a-*oversee* miradi yote (Bajeti) ya maendeleo ya wanawake Mkoani/Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo ningetamani mzungumze wote, lakini tumebanwa na wakati na kama ilivyosemwa na wasemaji wengine, huu ni Muswada pekee ambao umeandikwa na Waheshimiwa Wabunge. Nasema ni Muswada pekee ambao Wabunge mmeuandika upya na mpaka ikabidi sasa tuchape na Muswada wenyewe mwingine.

Sasa mimi nadhani ndio maana nayaona kabisa anayejadili vifungu hapa hayupo, mnajadili ubora na madhumuni ya Muswada huu kwamba ni jambo jema. Kwa hiyo. naomba mniruhusu wale waliobakia bado mna nafasi ya kuzungumza kwenye Muswada ule mwingine wa uchaguzi hivyo hivyo, lakini nimuite mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wote waliochangia kwa maandishi na wale ambao walichangia katika ngazi mbalimbali za mchakato wa Muswada huu. *(Makofi)*

Kama ulivyosema wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni Muswada muhimu lakini maandalizi yake yalikuwa magumu sana, kwanza kutunga sera na kutafsiri sera kwenye sheria, ilichukua muda. Katika mikutano mingine kuhusu Muswada huu niliwahi

kusema kwamba japokuwa tuliwaomba vijana wetu wafanye utafiti sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi lakini hatimaye imekuja kujitokeza tu kwamba kazi hii ni kazi ya akili zetu sisi Watanzania, ni matokeo ya kazi ya mikono yetu wenyewe na hapa mwishoni wewe umesema Wabunge ndio wamehusika zaidi kufanya marekebisho makubwa katika Muswada bila kuathiri malengo ya kisera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kabla sijatoa maoni yangu na maelezo kuhusu hoja mbalimbali kuhusu Muswada ulivyojadiliwa na Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu kwanza kwa kuzungumza na baadaye kwa kuandika maoni yao. Na ninawahakikishia kwamba wote hawa maoni yao yataingia kwenye *Hansard* na pale ambapo majibu hayajatosheleza, kuna majibu mengine ambayo yataingia pia kwenye *Hansard* kwa sababu muda hautatosha kutoa maelezo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliochangia kwa kuzungumza ni kama wafuatao, kwanza Mheshimiwa Pindi Chana, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, Mheshimiwa Halima Mdee, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbungwa wa Bububu, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, Mheshimiwa John Cheyo, Mbunge wa Bariadi Magharibi, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe na hatimaye Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliochangia kwa maandishi walikuwa wafuatao, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Castro Ligalama, Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge wa Ileje, Mheshimiwa Said Arfi tena, Mbunge wa Mpanda Kati, Mheshimiwa Magreth Sitta, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Profesa Idrissa Mtulia, Mbunge wa Rufiji, Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Mbunge wa Rungwe Mashariki, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Yono Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, Mheshimiwa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega na Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Mwibara. *(Makofi)*

Samahani sana na hapa mwishoni nimemsahau Mbunge wa muda mrefu Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini; na yeye alichangia kwa kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuahidi mapema kabisa kuwa Serikali itaifanyia kazi michango ya mawazo iliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na yale yote ya Kambi ya Upinzani na Wabunge wote; hasa yale ambayo yanagusa

maeneo ambayo hatimaye yatawekwa kwenye Kanuni zitakazotungwa ili kuboresha Muswada huu utakapokuwa Sheria. Lakini ningependa kutoa maelezo ya awali ya ujumla kuhusu Muswada huu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sheria hii kama zilivyo sheria nyingine zote, haijitegemei. Kuna sheria nyingi tu katika nchi hii ambazo zinasimamia masuala ya jinai, masuala ya rushwa, masuala ya fedha chafu *(money laundaring),* masuala ya dawa za kulevya na kadhalika. Sio kwamba nyakati za uchaguzi matumizi ya sheria hizi yatasimama, matumizi ya sheria hii yataendelea kuwepo na zitasimamiwa na vyombo vya dola. Kwa hiyo, sheria za matumizi ya fedha nyakati za uchaguzi ni sheria mojawapo ya nchi ambayo itatumika wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu hili ambalo limesemwa sana, ambalo ni geni kwa kweli. Nafikiri sio sisi tu, ni maeneo mengi katika Jumuiya ya Madola, tunaelwa tu *nomination day,* katika sheria hii tumeleta dhana mpya inayoitwa *nomination process.* Tulikuwa na maana ya mchakato wa uchaguzi kama inavyojulikana kuanza nyakati za kura za maoni. Na maana yetu ni kwamba sheria hii pia ihusike na michakato nyakati za kura za maoni; sasa ni lini *nomination process* inaanza? Kwa kweli tumesema kwamba tutawasiliana na vyama mbalimbali na wadau mbalimbali ili kuwa na muafaka. Hatutaki kuwa na utaratibu unaofanana kabisa wa uteuzi, lakini angalau muda ambao unakaribiana wa uteuzi katika mwaka wa Uchaguzi Mkuu na wakati inapotokea uchaguzi mdogo. Kwa hiyo, sasa hivi tumejiandaa mara tu baada ya sheria kupita, Msajili ameshaweka watu wake tayari kuanza vikao na wadau. *(Makofi)*

Kuhusu hili pia, wengi hapa na nje, mmeongea kuhusu watu ambao sasa hivi wanajitembeza kwenye majimbo kabla hata ya *nomination process,* sheria inasemaje? Naomba niwaerejeshe kwenye kile kifungu cha 25 ambacho kwa kifupi kabisa kinafanya haramu shughuli hizi za sasa ambazo zinaendelea kwa watu ambao wanafanya kampeni kabla hata mchakato wa kura za maoni haUjaanza. Nisome kwa ufupi sana kwa sababu ukifanya hivi kwa sheria hii sasa ni moja ya makosa moja ya ku-*hibitat practices* ni shughuli ambazo mnakatazwa na sheria hii tafadhali Kiangalieni sana kwa makini kifungu au *clause* ya 25 ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi pia mmeongelea sana kwa kina madaraka ya msajili na pia nafasi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, kwa kweli hakuna mgongano, watu wawili wanatakiwa washirikiane ili sheria hii iweze kutekeleza kwa sababu kuna mahali tu watakutana kwa sababu Mkurugenzi wa Uchaguzi mamlaka yake hasa yanaanza kuchukua nafasi yake halali siku ile ya *nomination.* Sheria hizi pia zitafsiriwe kifungu kimoja kimoja kama zilivyo sheria zote, tunaomba sana isomwe kwa pamoja ili uelewe zaidi. Kwa sababu tumeona kwamba watu wamechukua kifungu, wakajenga hoja kwa kifungu kimoja na kuwa na tafsiri ya pamoja bila kuangalia sheria yote kwa ujumla wake. Tungeomba sana sheria tusome kwa ujumla ili tupate tafsiri sahihi na baadaye itakapokuwa Kamati ya Bunge Zima nadhani tutaelewana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho na  la ujumla ni kwamba sheria hii kama zilivyo sheria zingine sheria sio jawabu kwa kila kitu, sio muarobaini wa kila kitu, binadamu anafahamu kuna sheria lakini huwa anavunja, kwa hiyo, hatutarajii kwamba sheria hii watu wataitii kwa

asilimia mia moja. Kwa hiyo, ni makusudio yetu kwamba hapa iwe ni mwanzo, tufanye marekebisho tuiboresha pale ambapo tutaona kwamba itakuwa na mapungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kusema hayo naomba nijibu hoja nyingine zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge haraka haraka kwa mtiririko kwa jinsi walivyoitoa. Kwanza kabisa Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Halima Mdee, yeye amesema mambo mengi sana, mojawapo ni kwamba sheria hii haichukui nafasi ya sheria nyingine, nikukumbushe tu kwamba sheria hii haichukui nafasi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, sheria ya *Money Laundering* au Kanuni za Makosa ya Jinai. Yeye pia amesema hakuna kipengele kinachoonyesha Serikali itachangia vyama vya siasa katika uchaguzi, Serikali itachangia kwa kiasi kubwa sana, kwanza ulinzi na usalama kwa ujumla wake kuanzia mchakato wa kula za maoni kwa vyama vyote hadi siku ya Uchaguzi Mkuu hii ni gharama kubwa. *(Makofi)*

Pili, Serikali itagharamia kama ilivyosemwa hivi karibuni, matumizi ya vyombo vya habari vya umma kwa wagombea urais na wagombea wenza, lakini pia Serikali itatoa ulinzi wa karibu sana kwa wagombea Urais na wagombea wenza. Hii gharama sio haba, tumeongeza na tunarajia kuongeza vituo vya kupigia kura, kutoka 33,000 mpaka 55,000 wala sio 50,000. Kwa hiyo, idadi hii ya vituo vya kupigia kura sio haba na nyie mnafahamu ufinyu wa Bajeti ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge ameshauri mamlaka wanayopewa katika kupanga kiasi cha fedha kitakachotumika katika gharama za uchaguzi, msajili ashauriwe, kwa kweli viwango vya gharama msajili hawezi akatoa tu kwenye akili yake, kutokana na vikao na mashauriano ya karibu na wadau tunafahamu hapa ni nani, ni vyama vya siasa. Si sahihi kwa msajili kufanya kazi ya Tume, kwa kweli dhumuni la sheria hii ni kudhibiti matumizi ya fedha wakati wa uchaguzi, na hili sio jipya, kwani Sheria ya Vyama vya Siasa inampa Msajili wa Vyama vya Siasa pia majukumu haya. Tume ya Uchuguzi haihusiki kisheria na masuala ya fedha ya Vyama vya Siasa na za wagombea hivyo ni sawa kwa msajili kupewa majukumu na wala si Mkurugenzi wa Tume na hili tumeliongea sana katika mchakato wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima Mdee pia amesema kwamba kuna hii tabia ya kulisha vikundi vya ngoma, hii sijui ni tiketi ya kurudisha takrima kwa mlango wa nyuma. Tunasema kwamba kulisha vikundi vya ngoma na vikundi vingine kama kitendo hicho kitafanyika kwa nia safi ambayo sio kushawishi mtu kupigiwa kura sio kurejesha takrima kwa mlango wa nyuma na wote kwa kweli tutumie nafasi hii kwa dhamira nzuri na sio dhamira mbaya ambayo Mahakama Kuu imeitolea uamuzi.

Maoni ya Kamati ni mengi, lakini naahidi yote kwamba tumeyazingatia, Mheshimiwa Dr. Slaa amesema kwamba dhumuni la Muswada huu ni kudhibiti Vyama vya Upinzani. Mimi naamini kwa mtu aliyesoma Muswada huu toka mwanzo mpaka mwisho hakuna mahali popote ambapo tunalenga vyama vyovyote. Muswada ni wa vyama vyote kwa kweli Muswada huu kwa kweli ni mkombozi kwa watu ambao wana fedha kidogo na vyama vidogo. Sijui kama wenzetu wanaelewa hilo, kwa hiyo sio kweli hata kidogo kwamba tunalenga vyama vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chama kuzuiliwa kuleta vifaa vya uchaguzi siku 90 kabla ya uchaguzi mkuu, naomba hapa tuelewane, tunaongea siku 90 kwa madhumuni ya michango

kutoka nje ya nchi, mgombea wa chama kilicho na fedha zake za kuagiza vifaa wakati wowote inaruhusiwa. Kwa hiyo, kama una fedha zako kama mgombea, kama chama unaruhusiwa muda wote kuagiza vifaa vya uchaguzi katika muda wa siku 90, kinachokatazwa ni fedha kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Ruth Msafiri ametushauri sana kuhusu elimu ya uraia, kuhusu madaraka ya msajili, kuhusu mambo ya rushwa, haya yote tumeyazingatia. Mheshimiwa Fred Mpendazoe, kwamba ofisi ya msajili na ofisi ya mkurugenzi wa uchaguzi na TAKUKURU ziwe huru, Serikali inalizingatia hili na tunakubaliana na yote yaliyosemwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, napenda kumuarifu tu kwamba kumekuwa na ushirikiano wa karibu sana katika kutunga sheria hii na wenzetu upande wa Zanzibar kwa uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na upande wa Wabunge. Kwa upande wa wajumbe na upande wa madiwani kwa kweli mamlaka haya yako chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwapo wataona ni mfano mzuri kuwa na sheria kama hii basi tunaomba waige mfano huu. Lakini kwa sasa wao hawana sheria hii kwa hiyo sheria hii itatumika kwa Uchaguzi Mkuu kwa ajili ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya na Mheshimiwa Zainab Vullu, sheria itafutiwe Kiswahili na tunazingatia na tutajitahidi iwezekanavyo kabla ya Uchaguzi Mkuu tuitafsiri sheria hii kwa lugha ya Kiswahili. Madaraka ya msajili kuwa makubwa katika mchakato huu tumejitahidi sana kuweka sawa madaraka ya msajili na madaraka ya mkurugenzi wa uchaguzi na hapa tulipofikia nafikiri ndio mahala pake kwa sababu lazima awe na madaraka hasa wakati huu ambao mkurugenzi wa uchaguzi hana nafasi wakati mchakato wa kura za maoni.

Kuhusu wagombea kupewa nafasi ya kusikilizwa kabla ya kuenguliwa Mheshimiwa Charles Keenja, naomba nimkumbushe nimpeleke kwenye kifungu hiki cha 20(2) ambacho kinajibu hoja zake. Mawakala watangulie kwa kuweka maneno kwamba anapofanya uwakala lazima *with knowledge or permission of the candidate* yalisemwa na Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia. Mawakala kwa kawaida ndugu zangu wanapewa vitambulisho na Tume ya Uchaguzi, kwa mawakala wetu binafsi ambao tunawatumia sio vibaya wajulikane kwa vyombo vya dola hasa kwa matumizi ya fedha za uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya chini na juu vya fedha vinavyotakiwa kutumika viainishwe kwenye sheria, tumesema haitawezekana kwa sasa kwa vile lazima tuwasiliane na wadau mbalimbali hasa vyama vya siasa na wadau wengine na hili litawekwa kwenye kanuni. Serikali kutoa ruzuku kwa wagombea kupitia vyama vyao, Serikali imeshatolea kauli suala hili kwenye semina na vikao mbalimbali na Serikali haijatenga fedha zozote kwa uchaguzi wa mwaka huu kwa ajili ya mgombea yeyote na katika mchakato wa Bajeti hakuna ishara ya kwamba kutakuwa na fedha kwa ajili ya wagombea wa Ubunge na Udiwani. *(Makofi)*

Suala la Sheria ipewe heshima kwa kufuatilia utekelezaji wake, huyu ni Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, ushauri umezingatiwa Muswada wa Sheria utaje hatua za kinidhamu kwa walioanza kufanya mapema kampeni. Nimeshasema turejee kwenye *clause 25,* inashughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU haikutajwa katika sheria hii anashauri itajwe, namshauri Mheshimiwa Said Amour Arfi kwamba tumetaja kifungu cha 33 kwa marekebisho ya 13(a) kinachofanya marekebisho haya. Lakini pia Mheshimiwa Said Amour Arfi ameongelea mambo mengi ambayo baadaye tutakuja kuyajadili kwenye Muswada unaofuatia wa marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1978. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, wameomba maelezo jinsi msajili atakavyoshughulikia nchi nzima, tunasema kwamba baada ya sheria hii kupitishwa sheria ya msajili na vyama vya siasa na ofisi ya msajili itapewa uwezo wa kusimamia na kufuatilia, inawezekana wakatumia Wakurugenzi, wakatumia Maafisa Tawala wa Wilaya kutegemeana na hali halisi itakavyokuwa wakati huo. Sheria idhibiti matumizi ya fedha chafu ili kupata viongozi safi tunazingatia.

Mheshimiwa Juma Killimbah, amesema sheria idhibiti rushwa katika chaguzi ilikuwa na nyanja sawa kati ya washindani wa kisiasa, tunaafikina naye na ndio madhumuni ya sheria yenyewe.

Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya anaunga mkono hoja yetu anasema Muswada huu ni wa kihistoria, unajenga msingi imara wa Taifa na hili ndio lengo halisi, namshukuru sana kwa kuelewa Muswada. Mheshimiwa Profesa Mwandosya, anasema pia matumizi yasiyo halali ya fedha katika uchaguzi ni hatari kwa usalama wa Taifa, kweli kabisa, matumizi ya fedha yasiyo halali ni hatari kwa usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Amour Arfi, aliendelea kusema kuwa sheria ya gharama ya uchaguzi haijamtaja mgombea binafsi, je, Mahakama itakaporuhusu mgombea binafsi itakuwaje? Nataka kumwambia kwamba laiti kama kungekuwa na mgombea binafsi sheria hii wala haimkatazi, isipokuwa kwa sasa sheria ya uchaguzi hairuhusu mgombea binafsi na pengine aje na hoja hii wakati tukijadili Muswada ujao. Mahakama itakapotoa maamuzi kuruhusu mgombea binafsi Serikali itaweka utaratibu wa kutekeleza maamuzi ya mahakama kwa mchakato wa kawaida wa kubadilisha Katiba ya Muungano na nyie mnafahamu mchakato wa kubadilisha Katiba unavyochukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uwezekano wa kuwa na mgombea binafsi katika hatua yoyote katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu ni mdogo sana na mimi naamini ni kama vile hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Amour Arfi, pia ameendelea kwamba Tume iendelee kutumia Wakurugenzi wa Halmashauri kama wasimamizi wa uchaguzi baadaye kwenye Sheria ya Uchaguzi tutalielezea hili Tume inaweza ikaendelea kuwatumia kwa sababu ndio maofisa tu ambao ni waaminifu, ambao ni waadilifu na unaweza ukawapata wakati wowote wakifanya makosa kuliko mtu wa mitaani ukamuajiri kwa muda mfupi baadaye hujui utampata wapi kwa vile tume kwa sasa haina watumishi wa kudumu katika ngazi za Wilaya.

Kuhusu msajili kupewa madaraka ambayo ni ya Tume ya Uchaguzi, sehemu hiyo kwa kweli imefanyiwa marekebisho makubwa, huyu alikuwa ni Mheshimiwa Athumani Janguo, ukiangalia Muswada wetu kwa sasa umebadilisha eneo hilo. Waziri ashauriane na vyama vya siasa katika kupanga viwango vya misaada kwa wagombea. Eneo hili pia Mheshimiwa Athumani Janguo limerekibishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Athumani Janguo anaulizia uwezo wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kukagua hesabu za vyama kwa wakati kutokana kuwa na majukumu mengi. Hapa tunataka kusema kwamba Serikali yetu itahakikisha na inajenga uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Gideon Cheyo, amesisitiza elimu kwa umma itolewe kutokana na utamaduni wa gharama ya matumizi ya uchaguzi kuwa ni jambo jipya, tumezingatia ushauri huu, kipindi maalum kutolewa kwa elimu hii katika vyombo vyetu vya habari tunazingatia. Mheshimiwa Gideon Cheyo pia amesema ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume ya Uchaguzi ziwezeshe ili kufanya kazi hii kwa ukamilifu na uadilifu. Serikali itawezesha Ofisi ya Msajili pia Tume ya Uchaguzi katika Bajeti ya mwaka 2010/2011. Serikali iwena mipango ya muda mrefu kubeba gharama za uchaguzi, tumezingatia ushauri huu wa Mheshimiwa Gideon Cheyo.

Lakini hapa mwishoni, Wabunge mashuhuri Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Jackson Makweta, Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Habib Mnyaa, wameunga mkono hoja hii lakini pia wametoa hoja nzito. Kwa mfano ile hoja ya siku 30 kabla ya *nomination day* na sisi pia inatupa taabu, pengine itakapofikia wakati wa Kamati ya Bunge Zima, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa amenishauri iwe ni siku kumi na nne au ni siku ishirini na moja kutegemeana na hali itakavyokuwa. Hili ni jambo letu sisi wote tushirikiane ili tupate muda muafaka wa kufikia *nomination day. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshauriwa kwamba sisi tuwe mifano, tusihonge, nakubaliana nao kwa dhati kabisa na nashukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Habib Mnyaa kwa kutukumbusha kwamba Serikali imepokea mawazo na maoni mbalimbali ya kurekebisha maeneo ya Muswada katika yote na katika kufanya hivyo tulizingatia mwelekeo wa kisera ambao tulijiwekea awali na kwa kweli marekebisho yalifanywa bila kuathiri mwelekeo uliokuwa umeainishwa katika sera iliyoleta Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kusema hayo naomba nichukue muda wako mfupi ili na mimi kabla sijatoa hoja nitoe hisia zangu binafsi kuhusiana na Muswada huu. *(Makofi)*

Kwanza mimi najivuna sana kuwa sehemu ya historia hii muhimu ya jitihada za kuboresha demokrasia kwa vitendo katika nchi yetu. Kazi tuliyofanya au tukio hili la leo la kihistoria na pengine jirani zetu watakuja kujifunza jinsi ambavyo tunatekeleza sheria hii mpya na ya kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kwa wananchi wa Wilaya ya Mbulu, ambao nawawakilisha katika Bunge hili naamini kwao huu ni ushindi mkubwa sana, kwa nini nasema ni

ushindi mkubwa, kwa sababu wamenirejesha kwenye nyumba hii kwa ajili ya mashirikiano na mapenzi yetu ya dhati katika kuleta maendeleo katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nyakati zingine nataka kukuhakikishia kwamba kura zangu ziliongezeka kwa ajili ya wananchi hawa kukataa kabisa kununuliwa kwa fedha na hasa hii ilitokea mwaka 2005 ambapo muda wa kura za maoni katika Wilaya ile ulibadilishwa kutoka saa nne mpaka saa tisa na nusu ili fedha zilizoingia Wilayani siku hiyo asubuhi ziweze kugawiwa kwa wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo haikuwaathiri, uchaguzi ulienda vizuri na hii jeuri yao ya kutokudanganyika sasa nawahakikishia kwamba imeongezewa nguvu ya kisheria na anayewasilisha Muswada huu sio mwingine isipokuwa ni Mbunge wao, naomba tuendelee kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na baada ya kusema haya yote na hakika sisi wote ni wazalendo tunajua mwelekeo wa kisiasa wa nchi yetu kwa sasa na nafasi ya Muswada huu katika kubadilisha siasa yetu. Kwa ajili hiyo basi nawaomba sana Wabunge wote pamoja na tofauti zetu za kiitikadi tuunge mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi Mwaka 2009**
***(The Election Expenses Bill, 2009)***

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujapata *schedule of amendment* ya Serikali, naamini kwamba kuna *schedule* nyingine, maana yake tulichonacho kwenye hii tumeambiwa sio *final*, sijui kama tunaweza tukagawiwa ili tuweze kuona mantiki ya maelezo ya Waziri pamoja na hiyo *schedule* ambayo alikuwa anaizungumzia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa labda kwa sababu ni makaratasi mengi tumepewa ile ile asubuhi, tumegawiwa kila mtu yamezagaa humu wote wanakuonyesheni hata nyuma yenu huko.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi tuligawiwa *schedule of amendment* ya *Electroral Laws* lakini labda wengine wanayo sisi huku kama ziko tunaziomba nadhani haina ugomvi wowote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Yaani hawa wamegawa na wameendelea kugawa na *Elections Expenses* wamegawa hiyo naweza kuwa-*defend*.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa inabidi usimame, tuko kifungu cha tatu ambacho kina mabadiliko.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndio tumeona lakini mimi *substantive* badiliko nilikuwa nataka kusema tu kwamba kwa kuwa Waziri ameona kwamba ni vizuri akazungumza na wadau yaani vyama juu ya ku-*fix* maana ya *nomination process* inaanza lini, nitaridhika tu akisema kwamba kutakuwa na *time element either* iseme siku sitini kabla ya *nomination day* au siku tisini kabla ya *nomination day* ili watu kabisa wajue kwamba maana ya *nomination process* iko hivi na hii itaambana na ile *bad practice* baadaye utakapokutana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama mtu anatembea tembea sasa na kabla ya siku ambazo zimetajwa kwamba *nomination process* basi huyo mtu mnaweza kumkamata kwamba ameingia katika *election process* kabla ya *nomination process*. Kwa hiyo, tutakapopata *assurance* tu ya namna hiyo kutoka kwa Waziri mimi nitakuwa *satisfied*.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekeleza ombi la Mheshimiwa john Cheyo, kwa sasa ni ngumu kidogo kwa sababu ndio tunaanza kutekeleza hoja hii kwa mara ya kwanza na baada ya hapa ndipo tutawakutanisha wadau ili tuamue kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu *nomination process* iwe lini. Mimi naamini sasa hivi vyama mbalimbali viko

kwenye mchakato wa *nomination process* kwa tafsiri ya Muswada huu lakini nafahamu kwa wengi ni kama kwenye mwezi wa nne mpaka mwezi wa tano mchakato wao utakuwa umeaanza.

Kwa hiyo, ndiyo maana nasema mara tu tukitoka hapa iwapo Muswada huu utapita basi kazi tutakayofanya ni kuwaitisha wadau na kwa mwaka huu Kanuni iweze kutaja *nomination process* itaanza lini. Na haitakuwa vyema kuiweka kwenye sheria kwa sababu ni mazingira tofauti pengine mwaka 2015 kutakuwa na haja ya kubadilisha Kanuni hizo.

Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa John Cheyo asubiri muda mfupi ujao pengine sio zaidi ya siku kumi na nne tutawaitisha wadau ikiwa ni mmojawapo, ni yeye kama Mwenyekiti wa Chama tuweze kuweka siku ambayo yeye anataka ikubaliwe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliptishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii nianze kwa kuishukuru Serikali katika kuleta marekebisho katika eneo hili ambapo kimezaliwa kifungu kidogo cha (2) ambacho kinasomekana kama tunavyoona kwenye *schedule of amendment.* Lakini kwenye Kamati eneo hili tulichukua muda mrefu sana na Wabunge kama wadau wakuu katika Muswada walisema haitoshi tu kuongelea vikundi vya sanaa. Mgombea anakuwa ana timu yake ya kampeni na timu yake ya kampeni inahitaji kunywa maji, kulala, vyote hivi vina gharama. Sasa tukasema hivi tusifiche fiche mambo kwa sababu katika kifungu cha 22 tutakuta yale ambayo ni makatazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napendekeza hapa nijaribu kushawishi Kamati yako ikubali kwamba katika mstari wa pili baada ya neno *voters* tufikirie kuingiza maneno *including the cost of providing food, drink, entertainment, accommodation or other provisions by a candidate to members of his campaign team. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, hizi ni gharama halali kwa wagombea na hata kama mtu atakuja kusema baadaye kwamba, hawa watu walikuwa wamekusanywa na mgombea kwa madhumuni tofauti, kwa shabaha ambayo ipo katika kifungu cha 22 utasema hapana! Hizi ni gharama halali za mgombea na upende usipende kama unajua biashara hii lazima hawa wale, wanywe, walale na yote hayo ndiyo sehemu ya mahamasisho ya siasa. Mimi nadhani tukielewana na Serikali katika hili, tutakuwa tunakwenda vizuri sana, na hizi zitakuwa *disclosed*, hakuna tatizo kabisa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali isingekuwa na tatizo sana na kuipanua hiyo *sub clause two*, lakini hofu yetu ni kuingia katika mtego ambao Mahakama Kuu iliingilia kati na ukifuatilia sana lugha ya Mheshimiwa Chenge, ni kama sasa kufanya kifungu hiki kiwe *open ended*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili ndilo eneo ambalo lilitupeleka kwenye Mahakama Kuu, likatafsiriwa kama takrima, na ndiyo maana sisi tumeona kwamba ni bora zaidi tujinyime sana kwenda huko kwa sababu ukisoma pale, *all funds used for promotional art groups for purposes of presentation of candidate's voters shall be deemed to constitute election expenses*. Hii yenyewe tungeiachia Mahakama ili baadaye itafsiri kuliko twende mbali na kutaja chakula, maji, malazi na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mwenye hoja nimesahau! Mheshimiwa Chenge mimi nilifikiri kwamba wazungumze halafu utakuja tena.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana nataka nii-*guide* Serikali, naomba sana.

**MWENYEKITI:** Haya sawa!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa Mheshimiwa Marmo, ni Mwanasheria mzoefu kama mimi pia. Napenda tu niisaidie Serikali hapa kama *concern* ni hiyo, tunachoweza kusema hapa *including the cost of providing* … tatata, hayo niliyoyasema *which has been reasonably incurred by a candidate for members of his campaign team. (Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno hayo ni maneno mazuri sana mdomoni, lakini kwa nia ya kutekeleza Sheria hii tunayotaka kutunga yanaipunguzia makali. Nafikiri kwa vile madhumuni yetu ni kukubaliana, na kwa vile kwa maneno matamu sana ambayo nimeyasikia humu jioni hii kuhusu dhamira ya kujenga jamii ambayo inapata viongozi bila hila na jeuri ya fedha, labda ingekuwa vyema tukaweka *limit* ya hiyo chini ya kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtaweka kama Bunge maana yake mimi situngi Sheria, mimi kazi yangu Waheshimiwa Wabunge ni kuwashauri, kuwabembeleza na kuwashawishi. Kama nia yetu ni hiyo ambayo nimeisikia Mheshimiwa Jackson Makweta anasema, zile *pillars* tatu za askari, mtu mwenye akili na askari kama mimi nadhani tungeweka *limit* kwa sababu unaweza kuwa na timu ya kufanya kampeni, wapiga kura wote wa jimbo lako la uchaguzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza tuweke *limit*.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amechukua vizuri hoja niliyotaka kuisema kwamba ni lazima tutenganishe vitu viwili; cha kwanza ni *campaign team* ambayo inazunguka na mgombea  na katika mazingira ya

majimbo ambayo ni makubwa ni lazima wasafiri, na watafika mahali ni lazima wale, walale na wanywe kama alivyosema Mheshimiwa Chenge. Kwa maana hiyo hoja ile bado inabaki *valid*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakubaliana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwamba hiyo *campaign team* ni nani? Kwa sababu hoja inaweza kuwa kweli kwamba hawa wote kwenye kijiji ndiyo *campaign team* yangu na ikarudi kwenye ile dhana. Kwa hiyo, nadhani tuweke tu hata katika *regulations, campaign team* ziweze kutajwa, tujue *campaign teams specifically* ni nani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ni huko Mahakamani baadaye hata kwenye *petition* huwezi ku-*identify* ni nani ambao unataka kuwatambulisha, na dhana ya Mahakama mimi naielewa vizuri tu kwamba, takrima ni ile ambayo unafika kwenye nyumba au kwenye kijiji, halafu wewe ndiye unawanunulia chakula, lakini si kuwalisha watu uliokuwa umewabeba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa hiyo umesemaje sasa? Simama basi useme maana yake sijakusikia!

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana na hoja ya Mheshimiwa Chenge, na tumekubaliana kwamba katika *regulations* Serikali ikubali ku-*specify* ile *campaign team* ni nani. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *scheme* ambayo inaanza kuletwa na … *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba azungumze kwanza Mheshimiwa Chenge!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kwa kutambua tatizo hilo ambalo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelisema ndiyo maana nilitumia maneno *reasonably incurred* kwa sababu tunasema ni Mahakama ambayo ita-*determine* kama kweli kiwango hicho kilikuwa ni halali kwa mazingira hayo!

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wewe ukasema kwamba, kijiji kizima ndiyo umekigeuza kuwa *campaign team* itakuwa ni kichekesho ambacho hakijawahi kutokea duniani hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi eneo hili naomba sana tuwe makini, na Mahakama ilifika huko kwa malengo tofauti na Bunge hili lazima liendelee kutunga Sheria na Bunge hili lazima liendelee kuweka maadili mema katika shughuli hizi za Uchaguzi. Katika eneo hili hakuna Mbunge ambaye anaweza akabisha kwamba, hoja hii haina gharama! Ina gharama na ndiyo maana tunakubali zitangazwe, iwe sehemu ya gharama za mgombea kama *election expenses! (Makofi)*

Mimi hoja ni hiyo tu ambayo naiomba Serikali ilielewe hili, hatupanui lakini nigependa tujikite kwenye maneno *reasonably incurred* na yana-*flow* vizuri tu. Kwa waandishi wa Sheria hii ni *attempt* ya mtu ambaye ana uzoefu kidogo wa masuala haya. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna hoja za aina mbili; mimi nilikuwa nashawishika na ile *scheme* aliyotaka kuileta Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba ili twende kwa kina zaidi kuhusu eneo hili tusije tukawa kwenye mtego.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ili kufahamu na kutafsiri timu hii ya kampeni. Timu hii ya kampeni maana yake ni nini? Na gharama zake ni nini? Pengine tuyahamishie kwenye kanuni na kanuni hizi zitaandaliwa kabla Bunge halijavunjwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa lakini kwenye Sheria itakaaje sasa maana yake Kanuni zitategemea tumeandika nini katika hii *main*. Mheshimiwa Chenge!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana kwa kuliona hilo haraka kwa sababu ni lazima tujenge msingi katika Sheria yenyewe ili tuweze kufika kwenye *regulations.* Kwa hiyo, nilikuwa nategemea, maana na mimi nimeleta *formulation* ambayo nilitegemea sasa kama mtu anataka hapo aboreshe kwenye hayo maneno ambayo nimependekeza kuingiza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge, hebu yarudie tafadhali!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimesema baada ya neno *voters.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kwenye *amendment*, *clause* kifungu b(ii) maana yake nakwenda kwamba, *all funds used for promotional art groups for purpose of presentation of candidates to voters* ndiyo inaingia hapo, si ndiyo hapo unaingilia! Hebu yaseme sasa!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu lilikuwa kwamba *including the cost of providing food, drinks, accommodations, or transportation which has been reasonably incurred by a candidate for members of his campaign team*. Inaweza ikawa *have* lakini Sheria ya tafsiri inasimamia hayo hakuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mapendekezo yangu na kama sasa Serikali inataka kuja na ka-*raider* ku-*deal* na hii lazima iwe kwenye *on a stand alone basis* waanzishe kifungu kingine ili tuone dhana hiyo kama inalinda marekebisho ambayo anapendekeza katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana! *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono dhana ambayo ameleta Ndugu yangu Chenge, lakini akienda kwenye *details* kama chakula, malazi itabidi pia katika hiyo *promotional art groups* tuweke mambo yote hayo.

Kwa hiyo, mimi ningeshauri kwamba, pamoja na ile aliyosema kwamba *reasonable* tungeishia tu kwenye *including expenses* za *campaign team*! Sasa bila kwenda katika *detail*

kama ni chakula au malazi, ulevi, pilau, pilipili tungeishia hapo naona ingeweza *for the …* sasa kama unataka kuipanua zaidi yule mtu wa *regulation* anaweza akafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tushawishike hivyo ili tumalize hii *section. (Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba ulifundishwa na Mheshimiwa Jackson Makwetta, na kwamba unapenda sana demokrasia lakini ninatafuta Kanuni ambayo inatuwezesha kuendeleza mjadala huu, bahati mbaya sijakubuhu katika hili. Lakini nafikiri kwamba *formulation* ambayo Mheshimiwa Chenge, ameileta na ambayo tulifikiri kwamba ingekuwa vizuri tukaifanyia kazi ingekuwa na utaratibu wake wa kuileta, hata hivyo inategemea tu mwongozo wako. Namheshimu sana Mheshimiwa Chenge, amenilea kielimu na pia kwa kuwa king’ang’anizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba kwa heshima kabisa nimuombe Mheshimiwa Chenge, akubaliane na ilivyo sasa na kwa sababu Sheria inazaliwa na inakua, tutaibadilisha kwa kadri tunavyokwenda.

Naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba mimi pamoja na kuwa Mbunge, lakini ni Jaji na naomba tuheshimu nyumba hii takatifu kwamba mwenzako anapozungumza wewe unyamaze tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiria kwamba maelezo ya kusema *costs reasonably incurred* maneno yanayosema *reasonably* ni sawa sawa lakini kwa kweli bila kuweka *cap.* kwa hiyo, idadi tunachofanya ni kuvunja uamuzi wa Mahakama na Mahakama ya Rufani, kuhusiana na takrima, tunarudisha takrima tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kama tunaweza kufanya hivyo, kukubaliana na alichofanya Mheshimiwa Chenge, lakini hapo hapo tukaweka tena *provision* ingawa naona kama Kanuni haziruhusu, ya kusema kwamba Waziri ataweka *cap.* kwenye hii idadi ya *campaigning team.* Kwa sababu unaweza kuwa na Wakurya wote wanakukampenia, jimbo zima sasa itakuwa balaa. Ahsante! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumheshimu sana *Attorney General* ukirejea kifungu cha 55(11) ambapo Mbunge anayetaka kufanya, inaanzia kifungu cha 10 ambapo Mbunge ambaye anataka kufanya mabadiliko au marekebisho katika hoja yake anaweza kumuomba Spika afanye marekebisho au mabadiliko katika hoja hiyo wakati anawasilisha hoja yake bila kutoa taarifa. Kwa hiyo, tunapojadili hapa ambapo hoja imewasilishwa, mimi naamini kwamba ndiyo wakati ambao tunaweza kufanya hayo mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hasa katika hoja ambazo tunajadili kwa muda mfupi, leo tumewasilisha hoja hii Bungeni na hatukuwa na siku moja kabla ya kubadilisha kwa sababu hata *schedules*, hata hotuba yenyewe imetoka leo asubuhi. Kwa hiyo, mimi nafikiri kifungu hiki kinahalalisha mabadiliko yoyote ambayo Mbunge anasimama na tumeshafanya *precedents* tumeshafanya kitu cha namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ili nisirudi tena, narudia kwa Mheshimiwa *Attorney General*, sisi ambao tumekaa kwenye Bunge tunaelewa kwamba, kuna gharama za *campaign team* bahati mbaya katika *interpretation* hakuna neno lolote linalotafsiri maana ya *campaign team*. Kwa hiyo, Rais anapokwenda kwenye *campaign team* hutegemei atasafiri peke yake, Mbunge anapozunguka hutegemei kwamba yuko peke yake, sasa Mahakama ambayo haitaelewa kwamba hiki ambacho mimi na timu yangu tunakula si takrima, nina mashaka pale katika tafsiri. Ninategemea kwamba mimi nitakapoenda ninaenda kutoa fedha za mfukoni mwangu kuwapatia wale tunaowakuta kwenye eneo, tunawapa chakula na vinywaji, pale ndiyo takrima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea nyuma ni kwamba, tulibadilisha kilichoitwa *African hospitality*. Sisi tulitoa kama wageni tunapofika kwenye nyumba badala ya mwenyeji kutupatia chakula, huo ndiyo utata uliotokea. Kwa hiyo, mimi nafikiri hoja inaweza kubadilika hapa kwa kutumia kifungu ambacho nimekisema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ipo Kanuni nyingine hapa kwamba, *actually* ilitakiwa yule mtoa hoja katika hili ingawa alitakiwa kuwa ametoa taarifa kwamba, nitafanya mabadiliko. Lakini *spirit* ya Sheria hii, kwanza tushukuru kwamba kimekuja kitabu kimoja, kama ingekuwa na lile rundo la mabadiliko yaliyokuwepo hata tungekuwa hatuonani, sana sana tungekuwa tunagongana tu, ndiyo maana nimeamua kuwa *very slow* kama tunakubaliana tunafanya, kama hatubaliani pia hatukubaliani. Kwa hiyo, nilifikiri tungeliangalia hivyo, *infact* hata ile *campaign team, somewhere* ingeingia kwenye *definition* ya Sheria. Mtoa hoja, aah, Mwanasheria Mkuu wa Seikali kwanza, au mmekubaliana! *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wote tuna lengo moja na mimi nilifuatilia kwa karibu sana hoja ya Mheshimiwa Chenge, na baadaye hoja ya Mheshimiwa Cheyo. Napata picha kidogo sasa ya mwelekeo. Tukiunganisha hoja ya Mheshimiwa Chenge na Mheshimiwa Cheyo, tukaweka vizuri kwa lugha ya kisheria mimi nadhani tunaweza kupiga hatua.

**MWENYEKITI**: Sasa *meanwhile* watu wenu wangekuwa wanatunga maneno gani yanaweza kuingia hapo, tutarudia. Sasa tumefika pazuri tunaagiza kwamba haya maneno tunayotaka yakae hapo watu wenu wako hapa watusaidie yanaweza kuingiaje hapo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tungemuomba Mheshimiwa Cheyo, hebu arudie pale sikumpata vizuri, alipokuwa anaboresha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama tumefikia hivyo ni suala la kuchukua yale maneno ya Mheshimiwa Chenge, nasema Mheshimiwa Chenge, siyo Cheyo, majina yanafanana. Kwenye *all funds used to promotional art groups for purposes of presentation of a candidate* nimekosea, *to voters including the costs of providing food, drinks, accommodation or transportation which are being reasonably incurred by a candidate for members of his campaign team shall be deemed to constitute election expenses.* *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti, …

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti nini? Kwani ninyi mlileta hoja? *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani sasa?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Hapana! Ni ufafanuzi tu kwamba hiyo idadi ya *campaign team* ni vizuri itazamwe na iwekwe wazi, mtu anaweza kuwa ana *campaign team* kwenye kila kata, nadhani tuwe *conscious* kidogo, nakubaliana lakini kuiacha wazi tu inaweza kutuletea matatizo.

**MWENYEKITI:** Si ndiyo maana tulikubaliana na *definition* ya *campaign team* iwepo na ndani ya *definition* inaweza ikaeleza *who are these people.* Kwa hiyo, tunakubaliana kwamba kwenye *definition* tutaongeza *campaign team* na katika *campaign team definition* ndiyo itasema haya anayosema Mheshimiwa Shellukindo lakini maneno mengine ni kama yalivyowekwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mapendekezo ya mabadiliko kwenye kifungu cha 12.

Kwanza nimependekeza hizi *marginal notes* zifutwe na tuweke *marginal notes* nyingine ambazo badala ya kusoma *Restriction of foreign funding to election expenses* tusome *funds restricted to be used as election expenses.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisema hili kwa sababu tunafahamu kwamba dhamira nzima ya Muswada huu pamoja na mambo mengine ni kupata viongozi ambao ni waadilifu, sasa ni imani yangu kwamba uadilifu wa kiongozi haupimwi tu kwa kutoka au kupata misaada kutoka nje ila inapimwa kwa fedha alizozitumia katika suala zima la uchaguzi, mchakato mzima kuanzia *nomination process* hadi kwenye kampeni kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika mantiki hiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Philip Marmo alisema kwamba kuna Sheria nyingine ambazo zinaweza zikawakamata hawa watu lakini ni muhimu tukafahamu kwamba hizo Sheria nyingine pamoja na kwamba zitawakamata

hawa watu hazitakuwa na uwezo wa kuwa-*disqualify* kuwa viongozi, ndiyo maana tuliweka hizi *restriction of foreign funding* peke yake ikiwa na dhamira kwamba kama mtu akitumia fedha nyingine za ndani zilizochafu yeye atakuwa ni halali hajawa *restricted* moja kwa moja na Sheria ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba mbali na kwamba *marginal notes* ibadilishwe lakini kuwe na kipengele kingine cha pili ambacho kitasema kabisa kwamba; *"All political parties, non governmental organisations, faith based organisations, community based organisation, other bodies or institutions, or any member of such political parties, non governmental organisations, faith based organisation, board of institution are prohibited from using funds that has been obtained by illegal means."*

Kwa hiyo, tukishakiweka hiki kipengele tutakuwa tumewazuia watu wote ambao watakuwa ama wametoa fedha za nje ama wametumia fedha za dawa za kulevya ama wametumia fedha za ndani ambazo zitakuwa zimetokana na wizi wa fedha za umma. Kwa hiyo, kama *spirit* yetu na lengo letu ni kupata viongozi safi sidhani kama Bunge lako Tukufu litakataa kuingiza hiki kipengele. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yeyote anaweza kujibu! Lakini tofauti ya hii huyu Mheshimiwa Halima Mdee amewasilisha hii hoja yake lakini haikufuata utaratibu kwa hiyo hatuipokei kama ilivyo kwa sababu haikufuata *procedure* za ku-*submit amendments* kwa mujibu wa Kanuni, Katibu wala hajajua kama zimegawiwa hapa, Serikali haikupata, mimi mwenyewe nimempa Mwanasheria Mkuu hapa, kwa hiyo nilifikiri utakwenda katika kifungu kinachohusika na utasimama kama kawaida lakini *amendment* hii siyo *official* kwa sababu hatuna. Lakini nakwenda ku-*accommodate* kifungu, utakapofika ukisema tutakusikiliza. Ndiyo hivyo sasa tunaendelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE, PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na dosari hizo za Kanuni, naomba nichukue fursa hii kuelezea Kamati ya Bunge Zima jinsi ambavyo tumefikia hapa kwenye *clause* hii ya 12.

Niseme toka awali kwamba, huu ni uamuzi wa kisera. Mwanzo wa safari tulipokuwa tunaanza safari ya kuwa na Muswada huu, lengo lilikuwa ni kupiga marufuku kabisa moja kwa moja michango kutoka nje ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nirejee tena, mwanzo wa safari wa kuwa na Muswada huu kisera, ilikuwa ni kupiga marufuku michango yote kutoka nje ya mipaka ya Tanzania kwa madhumuni ya kuendeleza siasa. Lakini baada ya kutafakari sana, na kuona kwamba baadhi ya vyama vyetu vina hata matawi nje ya mipaka ya nchi, baadhi ya vyama vina vyama rafiki na urafiki wa karibu sana na wakati mwingine wa dhamira nzuri, wakati mwingine ni urafiki wa damu, ndiyo maana tukaruhusu matumizi ya gharama au fedha kutoka nje, muda wote baada ya kulegeza msimamo wa kisera, muda wote isipokuwa kwa Uchaguzi Mkuu, siku 90 kabla ya siku ya Uchaguzi Mkuu, au siku 30 kabla ya Uchaguzi Mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi hapa nafungwa mikono kwa mapendekezo ya Ndugu yangu Mheshimiwa Halima Mdee, kwa sababu suala hili ni suala la kisera na

tunatekeleza sera ambayo tunataka vyama vyetu au sera za nchi yetu ziongozwe na maamuzi yetu sisi wenyewe bila shinikizo kutoka nje ya nchi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda sikueleweka vizuri kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwanza, sikusema kwamba, kifungu cha 12(1) kiondolewe, sikusema hivyo! Na vilevile sidhani kama maamuzi ya kisera yanakuwa na mantiki kama yanaruhusu fedha za ndani chafu ama fedha za ndani ambazo zinatokana na dawa za kulevya na vitu vinavyofanana na hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi dhamira yangu ni hiyo hiyo moja ya kusema kwamba tunajaribu kujichuja, kuangalia ni aina gani ya viongozi tunaowapata. Ndiyo maana kwa kuzingatia mantiki hiyo ya upande mmoja wa sera kifungu 12(1) sijakigusa kwamba kitolewe kwa kutambua hivyo vitu alivyovizungumza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba tunaingiza kipengele cha pili tunakuwa na *sub-section two* ambayo pamoja na mambo mengine inazikataza hizi taasisi zote kutumia fedha ambazo zimepatikana kwa njia  zisizo halali, hiyo ndiyo hoja yangu tu nyepesi sana. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Mdee yana lengo la kubadilisha kifungu hicho kuwa kifupi kuliko ilivyo na kushughulikia mambo machache kuliko ilivyo kwenye kifungu halisi. Unapozungumzia fedha chafu na nafikiri Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha alisema, unajua fedha haiwezi kuwa chafu mpaka umejua ni chafu. Kwa mfano, ukiwa na fedha ya rushwa hakuna mtu anajua utanunua kila kitu hapa, lakini tukishajua kwamba huyu amepatikana na fedha chafu vyombo vingine vitakushughulikia na ndiyo msingi wa pendekezo la Waheshimiwa Wabunge watatu waliochangia kwamba Sheria peke yake haitoshi isipokuwa lazima kuwa na usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alitaja Sheria kwa mfano, unazungumzia *Money Laundering*, pesa inaweza kuwa chafu kwa sababu unai-*launder* pesa inaweza kuwa chafu kwa sababu una-*deal* na *drugs*, na kama unavyofahamu Mheshimiwa Mdee, sura ya 95 ya Sheria zetu yaani Sheria ya *Drugs and Prevention of Illicit Trafficking in Drugs Cap. 95* na sheria iliyotungwa na Bunge hili mwaka 2006, *The Ant Money Laundering Acts, 2006* ambayo ni *Cap. 422* au *Act No. 12,of 2006* inazungumzia  hayo mambo.

Sasa kwa vile ni mwanasheria na sisi tunaheshimiana sana kwenye *profession* hii, nisingependa uwa-*mislead* Wabunge kwa kusema kwamba zile Sheria nyingine hazitawahusu au hazitatumika wakati wa uchaguzi, ndivyo unavyosema katika hoja yako au kama sivyo unavyosema basi kwa maneno ambayo ungeyasema ndivyo inavyoelekea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unaweza kusema hapa *by words* unaweza kusema pia *by conduct* kisheria na wazo lako ni zuri sana kwenye mabadiliko haya lakini tatizo langu mimi, *this law does not deal with illegal means* na *actually* lugha hiyo ya *illegal means* siyo ya kisheria kwa sababu hata kama ungekuwa  unataka *illegal means* ungekuwa ume-*refer* zile Sheria ambazo zinahusiana na *money laundering* au *drugs trafficking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mdee, uhafifu wa pendekezo hili ni kwamba unapunguza mipaka ya *coverage* yaani badala ya kwenda Musoma kupitia Arusha, wewe unataka uende kwa ndege kwa hiyo hutaona vitu vingine vya chini au sungura walio chini hutawaona. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba, hivi kifungu kilivyo sasa hivi na kina *cover* hii *restrictions* ya hapa ni *foreign funding*. Ile *marginal notes* kama nilivyokwambia wakati tukiwa kwenye Kamati kule, wewe ni Mwanasheria unajua sana na umemaliza shule hivi karibuni, kuliko mimi ambaye nimemaliza miaka mingi iliyopita, kazi yangu pia ni kutoa elimu, *marginal notes* inakusaidia tu kuelewa kifungu. Inasema *restriction of foreign funding to election expenses,* unachoongezea hapa ni *illegal means.* Sasa *illegal means* kama ile *foreign funding* inatokana na *illegal means* itashughulikiwa na zile Sheria nyingine ambazo nimezitaja na pia mfumo mzima katika uchaguzi. Makosa mengine ambayo yanatolewa na Sheria nyingine hayafutwi na Sheria hii, samahani sana kama nimekukwaza. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 14(2) kinazungumzia kwamba kutakuwa na *uniform regulations,* sasa ninachotaka kiingie kwenye *Hansard* ni kwamba hizi *uniform regulations* hazitakuwa na maana ya kugeuza Katiba za vyama mbalimbali. Sasa nataka hiyo *assurance* tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana nae kwamba...

**MWENYEKITI:** Kwamba...!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutazingatia Katiba za Vyama. Kwa vyovyote katika hali halisi hatuwezi tukafanya kila kitu kinachofanana kwa sababu ya tofauti zetu, ndiyo maana tutakuwa pamoja wakati wa kutengeneza Kanuni. Kila atakayekuja pale atakuwa akizingatia itikadi yake, atakuwa akizingatia Katiba ya chama chake, ndiyo maana nimesema tutazingatia.

*(Kifungu kilichichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 15

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, kifungu gani unasimamia?

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 15.

**MWENYEKITI:** Haya endelea kifungu cha 15**!**

**MHE. DR.WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka *assurance* kidogo kwenye kifungu cha 15 hasa pale anaposema *whether the gift loan advance deposit or donation shall be paid to the political party concerned and not otherwise and the political party shall disclose…* na asubuhi nilipochangia nilisema naona kidogo maneno yanayogongana ambapo mahali pengine pia *candidate* anaruhusiwa sasa kupokea. Sasa hapa inasema *shall be paid to the political party concerned and not otherwise*, kwa hiyo, nilitaka uhakika kama na *individual candidate,* je, anaweza kupokea? Na kama anaweza kupokea haya maneno *and not otherwise* maana yake nini?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kinahusu *political party* na kwa hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, ile Sura ya 258 kifungu cha 14 na 15 cha Sheria, fedha ambazo zinatolewa kwenye vyama zinakwenda kwenye akaunti za vile vyama na hapo ndiyo *provision* isemayo; *"not otherwise"* kwa maana hiyo hazitapelekwa kwa mtu mwingine isipokuwa chama chenyewe. Kwa sababu *the ruling words all funds provided by an association, or group of persons, or by any person for the nomination process or election campaigns of a political party' so are talking about political party.* Ahsante!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 kimeandikwa vizuri sana lakini ningeomba kwamba yale maneno ambayo yako kwenye kifungu namba 16 yanayosema; *"or some other evidence of payment"* yaongezwe kwenye hiki kufungu cha pili mwisho pale.

**MWENYEKITI:** Sijui mmemuelewa au arudie! Mheshimiwa Shibuda hujaeleweka.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha pili kinasomeka pale mwisho kwamba; *"a financial statement of all expenses incurred together with all receipts"* sasa nilikuwa nasema tuchukue ile *quotation* ya kifungu cha 16 ambayo ina nyongeza inayosema; *"or some other evidence of payment"* kwa sababu kuna mahali pengine risiti hakuna. Kwa hiyo, maneno haya *or some other evidence of payment* iwe nyongeza hapo,

kwa sababu wanasheria wana matatizo yao na tunapambana na kuandikiwa na taarifa za uzushi kwenda kwa msajili. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna matatizo na hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, yataongezwa maneno hayo; *"or some other evidence of payment."*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha pili (2) kinatoa siku 180 kwa *political party* ambayo iko *audited*. Sasa naomba twende *practically* kwamba, tunamaliza *elections* zetu takribani mwezi wa kumi, wakati huo tayari *financial reports* za mwaka 2009/2010 zitakuwa tayari katika *process* ya kuwa *audited*. Hapa ninataka ku-*capture* dhana moja kwamba, kama unataka *CAG* aweze ku-*audit* hizi *expenses* ni afadhali ukazihusisha na wakati ule ambao kufuatana na ile *article* nyingine tutakayoisoma ambapo *CAG* anapaswa ku-*audit* hivi vyama kufuatana na *Political Parties Act* itakuja huko baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vyama vinakuwa *audited within a financial year*, sasa ukiweka hapo hapo katikati siku 180 tunam-*commit CAG* ku-*audit in between the financial year*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa ndiyo nauliza, *one*, ile *work load* kwa *CAG* ni *problem* ya kwanza na *problem* ya pili *the real cost involved* katika kufanya hivyo vitu ambapo hii tungeihamishia kwa kusema maneno ambayo Mwanasheria atanisahihisha kwamba, *financial year following the election, then expenses* zote hizi zinge-*fall in within a normal time table* ya *CAG* na haitakuwa *an extra load* kwa *CAG* kufanya *a special report*, hiyo ndiyo dhana ambayo najaribu kui-*capture*.

Kwa hiyo, kama mnaweza mkasaidia kuondoa hizo siku au mkai-*phase* iwe *related to a financial year* mtakuwa mmeisaidia Serikali ku-*save* fedha nyingi sana na pia mtakuwa mmefanya utaratibu uwe wa kawaida na *according to the law which is in a Political Parties Act.*

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Cheyo, huoni pale ni maneno *within those days*!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni tatizo la *180 days* kwa *scheme* ya Sheria hii. Kwa sababu kuna *mischief* ambayo unataka ku-*cure* na sioni njia nyingine ya kuondoa hiyo *mischief* isipokuwa kufanya hii *audit* mapema zaidi, kwa sababu ina *implication* pia kwa huyo mtu ambaye anakupa hiyo taarifa *(audited report) integrity* ya chama chenyewe na *integrity* ya *candidate*. Nafikiri hapa twende *fully photo* kwa sababu hii vita siyo rahisi. Nafikiri Mheshimiwa John Cheyo, tuiache tu ilivyo, kama uzoefu utatupeleka mahali pengine ambapo tutaona kwamba hapafai basi hatutasita kuleta mabadiliko kwenye Bunge hili tena. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kiliyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 21

**MHE. CHARLES M. KAJEGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na tatizo katika Kifungu cha 21 (1)(a) na (b). Katika (a) nashindwa kujua *qualifications* za huyu mtu ambaye anaweza akamfanya *candidate held responsible*, huyu mtu anayeitwa *by any other person on his behalf*, ni *qualifications* zipi ambazo zitafanya huyu mtu kweli akifanya hicho kitu basi huyo *candidate* awe *held responsible*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu katika (b) kuna huyu mtu anaitwa *agent* anasema; *"every person who directly or indirectly by himself, his agent"* sasa nikiangalia katika *definition, definition* ya *agent* haipo. Kwa hiyo nilikuwa nafikiri kwamba huyu *agent* vilevile tuweze kuweka *definition* yake kwamba, yupi atakuwa ni *agent?* Na tukishafanya hivyo nilikuwa nafikiri kwamba, katika ile (a) tuondoe huyu *by any other person on his behalf*, vilevile tuweke *agent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu labda kwa wengine ambao hawana *experience* ya Mahakama, mimi nilikuwa *causalities* wa vitu kama hivyo, watu walichomekea watu wakasema kwamba mawakala wa Kajege ambao mimi nilikuwa siwafahamu. Sasa na hili linaweza likatokea hata kwenu ninyi kama hatutakuwa waangalifu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara hiyo hiyo sehemu (c) kuna kitu kinaitwa *promise*. Hiki vilevile wakati wa semina nilikizungumzia, hakuna kampeni ambazo unaweza ukafanya bila kuweka ahadi na uchaguzi, *campaign is all about promises*. Sasa tukishatoa hizi ahadi sijui tutakwenda kufanya kampeni za namna gani! Sasa nilikuwa nafikiri labda tuangalie ni ahadi gani tuweke ambazo zina *qualify* na zipi ambazo hazi-*qualify* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nianze na hili la mwisho kuhusu ahadi. Tunapoenda kwenye kampeni *menu* yetu iliyopo ni *manifesto* ya chama ambacho kimetudhamini au kwa lugha nyingine, Ilani ya Chama kilichotudhamini. Sasa kama kuna mambo mengine ambayo hayalingani na Ilani hiyo, basi kuwe na maelezo kwa sababu hapa unataka kumvutia mpiga kura akupigie kura wewe na chama chako kutokana na Sera na Ilani ambayo unawapelekea kuwauzia. Kwa hiyo, mimi hapa sioni tatizo, ahadi hapa naitafsiri kama Ilani ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale (b) hapa na (a), nyakati za uchaguzi kuna watu wa aina mbalimbali lakini bora hawa watambuliwe na vyombo vya dola kwanza kwa maana ya Sheria. Pengine Mheshimiwa Kajege anaongea juu ya Sheria zingine, kwa maana ya sheria hii ni bora watu hawa wajulikane kwa sababu pia watakuwa wakipokea fedha halali ambazo baadaye zitatolewa taarifa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kajege, angetoa tafsiri ya wakala hapa kwa maana tofauti kabisa na Sheria nyingine. Kwa maana ya Sheria hii ni wawakilishi ambao wanajulikana kabisa kwa sababu wanawajibika kwa fedha, siyo tu kwa sera, lakini pia kwa fedha ambazo baadae zitatolewa taarifa.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sasa mimi nilitegemea Mheshimiwa Waziri atueleze kwamba kwa mfano huyu *any other person* au *agent* ni yupi katika Sheria hii kwa sababu na yeye ameicha iko wazi na sisi hatujui kwamba huyu *agent* na *any other person* ni yupi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ahadi kwa mfano, huko kwenye kampeni ananyanyuka mpiga kura anakwambia Mheshimiwa mimi nina tatizo la mashamba yangu nimenyang'anywa muda mrefu; je, tukikuchagua wewe kwa kufuata Sheria unaweza kunisaidia mimi nipate mashamba yangu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo ahadi? Lakini haiko katika *party manifesto*, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hilo! *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kajege pole sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria kwa kweli haiwezi kutungwa na ika-*provide* kwa kila *eventuality*, mambo mengine tunaziachia Mahakama likitokea suala. Nafahamu kuna Waheshimiwa Wabunge humu ndani wana uzoefu mkubwa sana katika matumizi ya maneno haya kule Mahakama.

Lakini kuhusu hii *any other person on his behalf*, usisome tu *any other person*, malizia pia na *on his behalf*. Na kunaweza kuwa na *agent* ambaye umeishamu- *identify* na kila mtu anajua kwamba ndiye *agent* wako, lakini pia kunaweza kuwa na watu wengine ambao wanafanya vitu kwa niaba yako. Hapa maneno yanayotumika na ambayo Bunge linataka yatumike, *that other person must be acting on your behalf*. Kwa hiyo, ina maana kwamba, utakuwa umemwambia afanye hivyo vitu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege, huwezi kurudia mara nne, ukisharudia mara mbili basi. Nilimuona Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na tatizo dogo hapo kwenye hilo jambo la *promise*. Nilidhani ingekuwa vizuri kama tungelitolea *definition*. Kwa sababu gani? Tunatunga Sheria lakini ni vizuri pia tusisahau kujiuliza

yanayotokea wakati wa uchaguzi. Ni kweli unakwenda kwenye uchaguzi ukiwa na *manifesto* ya chama chako.

Lakini nadhani tulipomaliza uchaguzi ziko ahadi zilizotolewa nje ya *manifesto*, hizo nazo tunazi-*account* namna gani? Kama mnakumbuka tulikuwa tunasema kuna ahadi zilizotolewa kwenye Ilani lakini zipo ahadi ambazo Rais alizitoa anakwenda anakuta Watanzania hawa wana shida ya maji lakini kwenye *manifesto* hatukuiweka anasema, tutafanya hiyo. Je, hii inachukuliwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano thabiti ni daraja la Esimiwa, amefika pale daraja limeanguka kwenye *manifesto* hakuna, akasema chama chetu tukishinda tutajenga daraja na tumejenga. Sasa je, hiyo nayo tunaichukuliaje?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, *campaign is about promises*, lakini *promises* ambazo hazi *induce corruptly* msiseme kaneno kale *promises*, msome sentensi zote. Hapa kwamba, kuna *promise* nyingine ambazo uki-*promise* mahakama inatoa tafsiri kwamba hapa nia yako ilikuwa ni udanganyifu au kurubuni watu. Kwa mfano; umekwenda mahala daraja limeanguka, ukasema kwamba nikipata Ubunge nitajenga daraja hilo, sasa hiyo hiyo *promise* kweli una-*corrupt* watu hapo kweli. Lakini ukisema kwamba nikiwa Mbunge hakuna mtu atalala njaa hapa nitakuwa nawapa vyakula kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Jaji nita-*interpret* kwamba hapo unawa-*corrupt* watu. Sasa nimesema mwanzoni kwamba hatuwezi kutunga Sheria na tukaanza kutafsiri kwamba *promise* hii iruhusiwe, hii isiruhusiwe tutakuwa tunakwenda kufanyakazi ya kutafsiri Sheria ambayo si ya muhimili huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mongella! Ambao hawakusimama hawasimami tena kwa sababu tayari tuliwaandika. Tusiwe tunaanzisha mjadala, walisimama tukawatambua.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nadhani bado sijaridhika na maelezo ya kifungu cha *other person* kwa sababu mimi nimeshaona kwenye kampeni hizi unaweza ukatoa hotuba nzuri sana kwenye mkutano wa kampeni, mtu usiyemfahamu akafurahi akaenda kunywa kwenye baa akasema kunyweni yule mama hatari kweli kweli. Sasa mimi sikumjua si nitafikishwa Mahakamani bure. Mimi sikumteua, kwa hiyo, *other person is a very dangerous statement. (Kicheko)*

**MWENYEKITI:** *Acting on your behalf*, sio kwamba *any other person* tu. Rudia kidogo wanasema haijakuwa *defined.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tunalopata hapa sasa hivi ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wanasahau kwamba hatujadili Sheria zote za Uchaguzi hapa. Eneo hili liko hapa kwa madhumuni ya Sheria hii ya Matumizi ya Fedha Nyakati za Uchaguzi. Sasa maelezo yanayotolewa pengine yangeeleweka vizuri zaidi katika Muswada

ambao unakuja kuletwa baadaye, kwa sababu madhumuni ya sheria hii na lugha yote iliyotumika ni kwa madhumuni ya Matumizi ya Fedha Nyakati za Uchaguzi na tunadhani maneno yaliyotumika ndiyo maneno yanayofaa zaidi.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kusaidia Serikali kuelezea…..

**MWENYEKITI:** Kusaidia kutunga Muswada bwana wewe.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Kuelezea *concern* ya Wabunge kwamba imeshughulikiwa vizuri sana Muswada huu kwenye ukurasa wa 17 kifungu kidogo cha 2 ambapo kinasema hivi *"Where it is alleged that the act constituting prohibited practice was committed by an agent or any other person on behalf of the candidate." It shall be a defense for the candidate if he proves that it was committed without his knowledge, consent or approval or that of his agent."*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kwanza Mheshimiwa Kajege ameshinda kesi kwa sababu watu walikuwa sio watu wake.

Waheshimiwa Wabunge kutumia kifungu cha 56(8) inachoniambia; "Ikiwa muda uliotengwa umekwisha wakati Bunge liko kwenye Kamati ya Bunge Zima kujadili Muswada wa Sheria au katika Kamati ya Matumizi kujadili Makadirio ya Matumizi ya Serikali basi Mwenyekiti bila ya kulihoji Bunge ataongeza muda usiozidi dakika 30 kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kupitisha ibara za Muswada wa Sheria, kwa hiyo nitaongeza dakika 30 baada ya 2.45.

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 24(1) kinasema "Vyama vitakuwa vimemaliza mchakato wao kabla ya siku ya *nomination days* ambapo ni siku 30 kabla ya *nomination day*. Mimi naona hakuna haja ya maelezo makubwa, lakini ieleweke kabisa kama tutafuata hii na uki-*assume* kuwa kwamba tarehe 16 Agosti ndiyo itakuwa *nomination day* ndio kusema ni lazima kila chama na kila mmoja wetu hapa awe ameshapata kibali kutoka kwenye chama chake kwamba anagombea. Wakati ule ndio wakati wa Bajeti na kama unasema hivyo ndio kusema siku zingine 30 nyuma ya tarehe 16 lazima kila mmoja awe ameshapitapita kule kwa mambo yake kuhakikisha kwamba anachaguliwa.

Sasa *automatically* hiyo iko kwamba hatutakuwa hapa na Bajeti. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri hiyo siku 30 *is in practically* haiwezekani. La pili kama kuna haja ya hii

kuwepo na siku basi labda ingekuwa *within 30 days or within 14 days* badala ya neno *before I mean 30 days a nomination date*.  Hiyo ndilo tatizo langu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge nilisema kwamba eneo hili linataka uangalifu kwa sisi wote na tuwe makini wote kwa sababu tukipitisha bila uangalifu yatakayotusibu ni wote ni mabaya kwa sababu ya athari zitakazotokea kabla Bunge halijavunjwa.

Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema kwamba tusaidiane siku muafaka ni ngapi.  Maana awali ilikuwa 14 wakati Muswada wa awali ulipotolewa ilikuwa 14 tukawa *flexible* ikaongezwa ikawa 30.  Sasa twende siku 21 kwa sababu kwa hili sote tuna *stake* kwa hiyo, tusaidiane.

**MWENYEKITI**:  Pendekezo lake kwamba *within I don't know what he said.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE 9MHE. PHILIP S. MARMO):**  *Within 21 days or three weeks.*

**MWENYEKITI:**  *Within what now?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**  Ni sawa sawa Mheshimiwa Mwenyekiti, *withini 21 days.*

**MWENYEKITI:**  Nilimwona Mheshimiwa Dr. Slaa ilikuwa hiyo hiyo?

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:**  Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho, kifungu kidogo cha 4 ambapo kinazungumza kwamba *"a candidate who or a political party which is disqualified may apply to the registrar for review of his decision."*

Tatizo langu ni kwamba kama ilivyo kwenye kifungu nafikiri cha *7*; *"Upon disqualification of a candidate or a political party the registration shall inform the Director of Elections."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifikiri kwamba ingekuwa haki zaidi wakati nilipokuwa *disqualified* na *registrar* ambaye kabla hajani *disqualify* alikwisha kunisikiliza kwa mujibu wa kifungu cha 6.  Maana yake yeye ndiyo ana-*raise objection and hear representation by a candidate his agent or it political party.*  Tukizingatia kwamba muda wa Uchaguzi ni mfupi sana na kwamba akikukatalia hapa huna nafasi nyingine tena mpaka Mahakamani wakati wa *petition*.

Mimi nilikuwa nafikiri huyu aliyenisikiliza kama niko bado *aggrieved* mahali pekee pa kwenda zaidi ni kwa *National Electoral Commission.* Sasa sijui Serikali itanisaidia hapa hii *purpose* ya hii *review* wakati amekwisha kunihukumu baada ya kunisikiliza, hii *review* itasaidia nini. Najua Mahakamani ni *process* ya kawaida kwamba Hakimu au Jaji wanaweza kumtaka aka-*review* yeye mwenyewe, lakini *procedure* za Mahakamani ziko *very elaborate* na zinajulikana.  Kuna *orders* na kuna taratibu zingine zote ambazo zimewekwa.

Mimi nilifikiri hapa tungeruhusu ili haki itendeke ili mgombea asije akapata athari ni vyema sasa baada ya kuondolewa rufaa yake iende kwe *NEC* badala ya kwenda kwa *review* ya mtu huyo huyo ambaye alishamwondoa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kimefanyiwa marekebisho nafikiri kiongozi wangu wa roho wa zamani alikuwa hajakiona. Ile *concept* ya *registrar* ku-*disqualify candidate* imeondolewa.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *observation* moja kwenye 24.1. Kwa sababu Kamati yako haijaamuliwa *whether* siku 30, ndani ya siku 30 au 21. Lakini wote tunafahamu *nomination day* inategemea lini Bunge linavunjwa na ukishajua tarehe ya Bunge kuvunjwa Sheria ya Uchaguzi inakwambia *nomination day* itakuwa si chini ya siku tano na si zaidi ya siku 25 tangu Bunge livunjwe ndiyo itakuwa *nomination day na* sasa nimejaribu kulielezea hili kwamba baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Spika, juzi akisema *Inshallah* Bunge tutamaliza Bunge la Bajeti tarehe 23 Julai, lazima sasa akili yako ikutume. Mwenye mamlaka ya kuvunja Bunge atakapoamua lazima na yeye ahakikishe kwamba anafuata na anazingatia sheria inavyotaka na kwa sababu vilevile ukishaipata *nomination day* lazima ikupeleke kwenye siku ya uchaguzi ambayo haitakuwa si chini ya siku 60 na si zaidi ya siku 90 baada ya *nomination day*.

Sasa hayo yote nasema Waheshimiwa Wabunge tulione hili hata mtakapokaa kwenye vyama ukweli wa sheria utabaki ni huo huo *unless* Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ubadilishwe usiwe unafanyika katika tarehe ambayo tumekuwa na mazoea nayo yaani Jumapili ya mwisho ya kila mwezi Oktoba katika mwaka huo wa Uchaguzi Mkuu. Hiyo ni *observation* naitoa ili wote tuifahamu.

La pili, kwenye kifungu kidogo cha 2 hili ni ufundi tu uandishi. Kwenye mistari wa tatu kutoka juu maana hapa tunatoka *the candidate awe political party*. Sasa tumesahau ile ya *a candidate,* kwa hiyo, tuongeze maneno *lender himself or itself*, utakuwa ume-*capture* zote mbili, sasa nadhani Mwanasheria Mkuu hili ataweza akalisemea. La mwisho, kwanza niishukuru sana Serikali eneo hili tulihangaika nalo sana kwenye Kamati. Serikali imekuwa sikivu imekuja na utaratibu ambao ni mwanana, mimi nauunga mkono na kusema kweli unaeleweka vizuri sana, lakini la mwisho kwenye Ibara ndogo ya tisa, uchaguzi huu unahusu pia Madiwani. Nadhani hapo kuna *lapse* kidogo tumesahau tu kuingiza iwe sheria ya *Local Authorities Elections Act.*

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwenye mstari wa pili kutoka chini baada ya neno *Election Act* tunaweka *comma* halafu tunaingia maneno *The Local Authority Elections Act* halafu inaendelea *all the prevention* kama ilivyo. Sasa kama Mwanasheria Mkuu atakubali huo ndio mchango wangu katika eneo hili. Nakushukuru sana Mwenyekiti.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Andrew Chenge. Tumekubaliana kwamba kwenye 24(1) tutasema *within 21 days* na mapendekezo yake kwenye Ibara ndogo ya pili kwamba tuongeze neno *himself* na *himself* ina *include herself.* Nakubaliana naye na haya mapendekezo ya Ibara ya tisa ambayo

sasa ni Ibara ya nane kwenye marekebisho haya nafikiri ni kweli kwamba tumesahau *Local Government* tutayaweka hayo maneno.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 25

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nipate ufafanuzi tu kuhusu hiki kipengele cha 25 naona kama kina *nullify* kwenye ile *campaign period*. Kwa sababu ukisoma kwenye *campaign period* wanasema *means the period commence immediately after the nomination day up to the day immediately proceeding election day*, lakini ukisoma Ibara ya 25 inasema *prohibition of prohibited practicse period to the nomination process*. Maana yake kwa nini hiki kipengele ni kama ninaiharibia *campaign period*. Nilitaka nipate ufafanuzi tu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kinawa-*cover* watu ambao sasa hivi wanajipitisha kule na wanasema kwamba wanatangaza nia yao ya kuwatoa kwenye nafasi hizo mlizonazo, ndiyo maana yake hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 32

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nisaidiwe ufafanuzi katika hiki kifungu cha 33

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tuko Ibara cha 32.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Ohoo !!!!!!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 33

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisaidiwe kupata ufafanuzi kwa kuzingatia kwamba katika siasa kuna *political vendetta* na hapa pana kipengele ambacho sasa kitalinda watoa habari lakini ukweli ni kwamba katika siasa huwa pana makandarasi wa kuzusha uongo. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, patakuwa na utaratibu gani wa kufanya *verification,* Msajili afanye *verification* badala ya kupokea tu na kusema wewe nakufuta nimepokea taarifa za watu 30 wamesaini kwamba umefanya tabia za hujuma.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona hofu ya Mheshimiwa Shibuda na Waheshimiwa wengine kuhusu eneo hili. Lakini tukumbuke kwamba hatutumii sheria hii bila ya kulinganisha na sheria zingine zilizopo kusema uongo au kuhujumu au kufanya makosa kwa kulingana na sheria zingine, sheria ya ushahidi. Kwa hiyo, tusome kama nilivyosema pale awali sheria hii pamoja na sheria zingine ili haki iweze kutendeka. *(Makofi)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri sana, lakini hatokuwa kila jimbo. Sasa kule busara inaweza ikatumika tafsiri ya utashi binafsi ya kumfuta mgombea, ndiyo maana nilikuwa nasema basi niwaombe wataalamu watuwekee angalizo la sheria itakayoongoza maamuzi kule, kifungu cha sheria kitakachowaongoza wawakilishi wa Msajili katika maeneo ya uchaguzi. Bila hivyo patakuwa na tafsiri za utashi binafsi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakutakuwa na tafsiri ya utashi wa mtu mmoja mmoja kwa sababu kama ni mtoa habari anaongelea juu ya rushwa wale wa TAKUKURU watatafuta ushahidi ili kuthibitisha kama haya yanayoletwa na *whistle ball blower* kwamba ni wa kweli au la?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema kama sheria zingine zilizopo zinatumika ikiwa ni pamoja na sheria ya ushahidi. Kwa eneo hili kwa kweli ni makosa yanayohusiana na rushwa zaidi na nafahamu mtu hawezi akapelekwa Mahakamani mara moja kwa sababu tu mtu mmoja ametaja kwamba fulani ametoa au amepokea rushwa lazima uchunguzi ufanyike na kuwe na kesi ambayo inaweza kuwa na sura ya kupelekwa Mahakamani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge linarudia)*

***(Muswada wa Sheria wa Gharama za Uchaguzi***
***(The Election Expenses Act, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Zima imeupitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara pamoja na marekebisho yake na kuukubali bila ya mabadiliko naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 (*The Election Expenses Act of the year 2009)* pamoja na mabadiliko yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huu Muswada umesafiri kwa shida kweli kweli na umefika. Napenda kusema kwamba na hii ni kwa faida ya wenzetu wanaojua kuandika maneno kwa umma. Kazi ya Wabunge ni kutunga Sheria na safari hii wamethibitisha kwamba wametunga Sheria, na wenyewe ni mashahidi kwamba imebidi uchapishwe upya, hiyo ndiyo kazi ya Bunge. *(Makofi)*

Sasa mimi napenda Waandishi wa Habari, ofisi yetu iko wazi kama kuna jambo mnaona hamna uhakika na kusema basi mnapiga simu mnauliza. Maana wanasema Muswada uliingia ndani ukatoka, haukuwahi kuingia humu ndani, kwa hiyo, ilikuwa bado katika kazi zetu za *committee* na Kanuni zetu zinaruhusu kwa kukaribisha watu hata wa nje ya Wabunge wenyewe kuweza kusaidia kutoa maoni.

Kwa hiyo, Muswada huu haukuwahi kuingia Bungeni na kutolewa ulikuwa bado kwenye hatua zake mbalimbali za Kamati ambayo ndiyo kawaida yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoona tungesema wote tuwe tunakaa humu tunatunga hii sheria tungekuwa hatufiki, ndiyo maana tunapokuwa kwenye Kamati wanaweza kuchambua mtu anaweza kuzungumza hata mara ishirini mara ngapi mradi wakubaliane lakini nako huko wanapitia kifungu kwa kifungu, kwa hiyo tuna utaratibu mzuri.

Mimi nasema Waheshimiwa Wabunge nawapongeza sana kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kupitisha Muswada huu kwa kuridhika kwamba hapa tulipofika hebu tujaribu kuupitisha, lakini mmefanya kazi, jambo ambalo mimi napenda niwapongeze hasa wenzetu wale ambao wamebobea katika vifungu hivyo wametusaidia sana kwa hiyo tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Tunawapongeza pia na Serikali yenyewe kukubali Muswada waliouleta wenyewe uchambuliwe na uletwe katika mfumo uliokuwepo hapa. Sasa mimi naomba nitangaze yafuatayo maana sasa watasema baada ya kupitisha Muswada wakaenda kujipongeza, si kweli. Tulikuwa na mwaliko toka juzi kwamba timu yetu ya mpira imeshinda ni timu bingwa katika timu za Wabunge za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tulikuwa na pongezi hiyo, kwa hiyo, hiyo pongezi itafanyika leo hii, ilikuwa tuanze saa 1.45 usiku. Bahati nzuri kuna mgeni wetu na yeye alikuja kwa shughuli zake hapa Mheshimiwa Rais, hawa Waheshimiwa Mawaziri ilikuwa sasa hivi waende kwenye *cabinet*, lakini Mheshimiwa Rais ameridhia kwamba hata Mawaziri waende kwenye hafla hiyo wakashirikiane na nyie Waheshimiwa Wabunge na yeye mwenyewe pia tumemkaribisha ashiriki katika hili na amekubali kushiriki. Kwa hiyo, sio hafla peke yetu na Mheshimiwa Rais atakuwepo, yeye ni kiongozi mkubwa katika Afrika Mashariki lakini Wabunge mfike mapema kwa kujua kwangu shughuli kama hizo Wabunge wengine *interests* zao ni ndogo sana, mimi naomba mfike tu mara moja pale halafu mtaondoka kwa wakati wenu. Mwenyekiti wa sherehe saa ngapi? Mimi nafikiri mngeenda moja kwa moja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima ya mgeni rasmi katika shughuli hiyo ningeomba sana tunapomaliza shughuli hizi na utakapoahirisha hili Bunge Waheshimiwa Wabunge wangeelekea moja kwa moja kwenye uwanja wa shughuli ili kuifanya ratiba iendane na wakati na kumpa nafasi mgeni rasmi kuhudhuria shughuli hii na kwenda na shughuli zake nyingine kadri atakavyokuwa amepanga.

**NAIBU SPIKA:** Ipo kwenye sehemu ya ukumbi wa sherehe kule, sio hapa chini. Kule kwenye uwanja wa sherehe wa siku zote.

**WABUNGE FULANI:** Wapi?

**NAIBU SPIKA:** Wapi vipi nyie hamkujui, tunasema hivi hapa Bungeni tuna eneo letu huwa tunapofanya sherehe za wazi. Ni baada ya pale Ofisi za Spika kule nyuma kuna ukumbi kule nyuma, inaonyesha wengi huwa hamuendi sasa mnasema wapi tena, kwa hiyo, mnakaribishwa wote asiyekujua ataelekezwa, kwa hiyo, tunaomba tukiahirisha hapa wengi muende kule kusudi tumkaribishe mgeni wetu.

Baada ya kusema haya muangalie kwenye *Order Paper* na huu Muswada mwingine nadhani itabidi tuufanyie kazi kesho.Kwa hiyo, kesho tutakuwa na Miswada miwili lakini *Order Paper* itatuelekeza zaidi. *(Makofi)*

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi ya leo, niwatakie jioni njema na naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.59 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 12 Februari, 2010 saa tatu asubuhi)*